# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, GANZE CONSTITUENCY HELD AT GANZE PRIMARY SCHOOL

ON

**Monday, 6th May 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, GANZE CONSTITUENCY, HELD AT GANZE PRIMARY SCHOOL – KILIFI ON MONDAY 6TH MAY, 2002.**

**Present:**

Com. Abida Ali Aroni
Com. Dr. Abdirizak A. Nunow

**Secretariat In Attendance:**

| | |
|---|---|
| Mr. John Watibini | Progrmme Officer |
| Hilda Miranga | Assistant Programme Officer |
| Gladys Osimbo | Verbatim Recorder |
| Rose Samba | Sing Language Interepresnter |

**Committee Members:**

| | |
|---|---|
| Jeffer Kingi | Malindi District Co-ordinator |
| Susan Mbiria | |
| William Pola | |
| James Gisau | |
| Martha Salama | |

**Meeting started at 10.00 a.m. with Com. Abida Aroni in the Chair.**

**Muslim Prayer (Muslim Dialect)**

**Com. Abida Aroni** - Basikwa ku Asante kwa dua yako na tungependa kujijulisha sisi wageni wenu kwa siku ya leo, kabla hatujaanza shughuli zetu, tuko hapa wanatume wawili. Mwenzangu ni Dr. Abdirizak Nunow Mimi naitwa Abeda Ali Aroni , halafu tuna wenzetu kutoka katika secretariat ya tume, tuna Bwana John Watibini, na nitamwomba Bwana John Watibiri atujulishe wenzake.

Asante na tumekuja na co-ordinator ingawa si co-ordinator wa upande wa huu lakini ni co-ordinator katika mkoa huu wa Pwani, ambaye ni Bwana Kingi amekuja kumsaidia co-ordinator wa upande huu ambaye ameelekea upande mwingine wa Ganze. Bwana Kingi.

**Bwana Kingi**: Hamjambo? Kama mujuavyo katika kila constituency, tuna wanakamati. Katika hapa upande wa Ganze, tuna wanakamati ambao ndio hawa, hapa tuna;

Bwana James Gitau Philip, yeye ni mwanakamati wa-tume, hapa tuna Susan Mbilia, yeye pia ni Mwana Kamati, pale tuna Martha salama ni mwana kamati, William Mpola, yeye pia ni mwanakamati. Hawa wanawakilisha upande wa Ganze, katika shughuli ya kikatiba.

**Com. Abida Aroni -** Asante Bwana Kingi. Nafikiria baada ya kujuana kwa vile hatuwezi sisi, tutawajua mtakapokuwa munatoa maoni, hatutaki kupoteza wakati mwingi, na tutakwenda moja kwa moja kwa watu ambao wamejiandikisha – eh – tutawapa watu ambao wanataka kuzungumza dakika kumi ambao watakuwa wameandika na nakala ambazo wangetaka kuzipendekeza, tutawapa dakika tano, ili waweze kusummarize au kufupisha ikiwa watataka, na mtapata nafasi ya kujiandikisha tena kwenye register yetu ambayo iko hapa, ambayo ni register maalum itawekwa katika Maktaba ya Tume na pia tunaa tungewaomba mtakapokuwa munazungumza mwanze kwa kutoa majina yenu kwa sababu tuna record. Tuna record ya – ambayo lazima tuipeleke na itakuwa ni bora mtu akijijulisha ili katika mazungumzo yako utabulike ni mtu gani ambaye amezungumza. Kwa kuanzia, tuna Bwana Jonathan Ngare Kombe. Nathania una written memorandum sio? Tutakupa dakika tano. Summarise.

**Jonathan Ngare Kombe**: Habari zenu? Kwa jina najulikana kama Jonathan Ngare Kombo, mimi ni mgiriama mzaliwa wa Ganze. Siku kama hii ya leo tumeingojea watu wa Ganze maanake kusema ule ukweli , wa-Kenya, katiba ambayo imekuwa/vikitutawala kutokea kitambo ilikuwa ni katiba iliyokuwa imeandikwa na mkoloni, si yetu.

Imetugandamiza tunataka tuibadilishe iwe yetu, iwe yaweza kusaidia sisi wananchi. Kwa hivyo mimi sitasema mengi kwa sababu mengi nimeandika lakini sana swala muhimu ambayo ningelitaka kuliongea hapa kabla niondoke ni kuhuzu maskwota.

Naonelea, sijui kama inawezekana vipi mtu azaliwe mahali, babu yake azaliwe pale mahali, halafu yeye baadaye anakuwa ni skwota. Hili jambo inatakikana kama inawezekana, hiyo katiba mpya basi jamaa tui hakikishe kwamba itakuwa inaweza kumsaidia ili swala la maskwota., mzaliwa wa Kenya hawezi kuwa skwota. Kenya hii.
Kwa hivo mengi mimi nimeyaandika kwa hivo nafikiri yatakuwa ni muhimu ikiwa ya kuokonya hizo makala zangu.

**Com. Abida Aroni** – Asante Bwana Kombe pengine tungempata sasa Bwana Ramadhani K. Mbaya.

**Ramathani K Mbaya**:- Habari Zenu. Ningependa kuzungumzia kuhusu ile katiba vile ambavyo iliandikwa ambayo inatumika katiba ya Kenya.

Naona kama mwenzangu alivyo zungumza hapa, katiba iliyo andikwa, haikuandikwa kuwa ni wakenya wenyewe walishirikisha isipokuwa iliandikwa na mwingereza na kama vile alivyosema mwenzangu kuwa wakenya wanagandamizwa , basi hiyo ni kweli na ni lazima tuwe tutasimama tuhakikishe kuwa hii katiba inabadilishwa ili vile vipengele ambavyo vinagangamiza wa Kenya viwe ni vyenye kuondolewa, kwa hivo, sisi tumeandika katika karatasi mengi yatakuwa huko, yataonekana huko, lakini nitazungumzia jambo mawili hivi.

Kwamba kama sisi waislamu, tunasema kwamba waislamu wasi-ingilie, wasiingiliwe, au kulazimishwa kubadili katiba ya Allah ambayo ni Koran na hadithi ambazo zime ongozwa na mtume Muhamed Zlahazwa salaam.

Na jambo lingine tunasema kwamba Rais wa nchi akiwa mkristo au wa dini yeyote au asiwe na dini, makamu wake awe muislamu au Rais akiwa muislamu basi makamu wake asiwe kuwa muislamu. Kwa hivo mengi tutayaona huko kwenye karatasi ambayo tumeandika. Asante.

**Com. Abida Aroni** Nickson Zai**?** Bwana Nickson Zai.

**Nickson Zai:** Habari ya asubuhi? Maoni yangu nitayatoa kwa lugha ya kingereza tafadhali. Majina yangu Nickson Karisa Nzai. Nimeandika lakini kuna machache ambayo ningetaka ku "highlight on".

The first thing is that the question of the Constitution of Kenya should have a preamble which should outline whose constitution it is because the current constitution does not have that in place. So we should have a constitution that has a preamble that should show whose it belongs to, and within the preamble we are supposed to have the political, economic and social objective that should be expressed in simple language understood by everybody. Not the kind of Law Jargons that ar e used by our "Learned friends".

Then I also want to talk about the powers of the President. The President enjoys too much powers especially according to the current constitution, and I have the opinion that the powers of the President should be cut that we should have of course separate powers between the Executive and the Legislature as well as the Judiciary, and that the President should not be the head of the government and at the same time the Head of state and also he should not be the person who makes all the appointments especially for those that are Heads of parastatals, or corporate institutions of the government. We should have these particular people appointed by the Parliament so may be, whatever should be, the President is supposed to endorse, but all these people, names of these people be presented to Parliament, discussed and then, the President has to endorse. They should present at least three people or at most three people and then out of the three people, the President therefore makes of course a choice out of those three.

Then another thing is the issue of corruption. I think Kenya is rated as one of the most corrupt country in the world and I think corruption should therefore be addressed especially in this current constitution that we want to come up with, that any public office bearer who is found to have engaged in corrupt deals should forthrightly lose that particular post and then he should not be allowed to take any office any longer and he should of course face the law. So we are saying that the law of the country, the constitution that we are drafting right now, it should be the supreme law and everybody is supposed to be subject to that particular law.

Then I also want to talk about the President also in terms of right now when we are going for elections any moment or say by the end of this year. I think it is important that anybody who is supposed to come to become the president should have a Vice President in place so that there isn't going to be that power vacuum. Right now we are left not knowing who actually is supposed to be the Vice president. So I think in our constitution, there has to be clear indication of the position of the Vice President so that should anything happen, then we know who exactly is supposed to take over power from the Head of State; and last but not least, I want also to air issues concerning the levies that the government collects, the road levies and let me say the revenue that is collected from every region for that case, or every Province for that matter.

We realize that we have a policy of bottom or top bottom kind of development policy which we find that everything is collected through the Central Government and then from there, now is distributed. But many a times you find that the kind of policies that are drawn right there do not therefore meet the needs of the people at the grassroots. So I think we should have a different outlook all together where development of course people are supposed to be – you know – they are supposed to be involved in coming up with some development projects that are beneficial to the people other than having this top - bottom kind of development policy that we have at the moment. So the revenue that is collected in every region, I think it should be made to develop that particular place, other than having to please the economy of that particular place and then the money is taken to the Central Government and more or less that money does not therefore come back to develop that particular place. So I think in the constitution that we aare coming up with, it should address those particular issues. Well, I have been given only 5 minutes and I have quite a lot of things to present here. So what may be I'd say is that I want now to humbly submit this

particular document and I believe that, whatever you come across here, it is of course my opinion and I feel that should these things be – they should also appear within the new constitution that we come up with. Thank you very much.

**Com. Asante Sheikh Omari. Ndarusi**

**Sheikh Omari Ndarusi**:- Kwa Jina naitwa Sheikh Omari Ndarusi, ni mwalimu hapa wa madarasa, na ni imamu. Kwa niaba ya waislamu wote wa Ganze, na nikiwa mimi ni mwenye kiti wa baraza la maimamu huko katika sehemu hii ya Ganze branch, maoni yangu, tunasema katika mahakama ya Kadhi mkuu na makadhi, ipawe majukumu kamili ili waweze kushughulikia matatizo ambayo inawakhumba waislamu. Na ndipo posa tukaona kwamba, mahakama ya ma-kadhi na kadhi mkuu, haikufaa.

**Com. Abida Aroni -** Tafadhali watoto kuna shughuli hapa muhimu mukae hapa bila kupiga kelele au tutamwambia mwende darazani. Endelea tafadhali.

**Sheikh Omari Rarusi**: - Ndio nikaona kwamba hawana uwezo wa kuweza kuwatumikia wananchi ipaswavyo kwa sababu hawakupewa uwezo katika mahakama hiyo. Na kile kifungo cha 14 (a) – Kifungo cha 14 (a) ambacho kifungo kile kinaeleza kuwa Rais yuko juu ya sheria tunasema kifungo hicho katika katiba hii unayokuja kiweze kuondolewa kwa sababu aliye juu ya sheria tunajua katika dini zote, tumeambiwa yule aliye juu ya sheria ni Mwenyezi Mungu peke yake.

Neno la mwisho, ni hali ya kifungo kinacho wapa uwezo madiwani, kuwa – teuwa ma-meya and wenye viti – wa mabaraza basi twasema katika katiba hii inayokuja kifungo hiki kiondolewe wapa wananchi wenyewe wachague ma-meya na wenye viti wa mabaraza.

Na la mwisho kuna madiwani maalum na wajumbe maalum huchaguliwa, basi twasema kwamba katika katiba inayokuja, mipango hii waweze kuchaguliwa viongozi wa makanisa na ma-imamu wa Miskiti maanake ma-imamu pamoja na viongozi wa makanisa ni watu ambao wafanya kazi kushinda watu ambao wachaguliwa tu ki – holela holela kupewa kazi zile na hawana sifa za kupewa vitu kama hizi. Asante.

**Com. Abida Aroni -** Abdallah Bashora: Mzee?. Tafadhali jiandikishe hapa.

**Abdallah Bashora**: Hamjambo nyote?

**Com**. **Abida Aroni -** Jambo?

**Abdallah Bashora: -** Kwa jumla kwa majina ninaitwa Abdallah Hidhawo Bashora, na mimi ni imamu katika upande huu wa Ganze hapa musikitini. Kwa hiyo katika maoneleo yangu ama mapendekezo yangu, nitakapendekeza katika upande wa

biashara. Nitakapendekeza katika upande wa biashara ndogo ndogo. Kwa sababu hata hivi nivyo hufaa pia nionekana hata ukiwa ni mu-islamu na waislamu pia vile vile unaruhusu kufanya biashara. Kwa hiyo biashara, katika upande wa biashara ndogo ndogo ili watu wawe huru. Wasi- tozwe ama kukatiwa leseni kwa kiwango ambacho kwamba hakistahili kutozwa mtu huyu, kwa sababu ni mtu ambaye kwamba anaanza sasa. Wapewe muda ambayo kwamba wanaweza baada yake kuja kukata leseni hizo wakiwa watajiwezesha wao wenyewe.

Na pia vile vile wafanya biashaa wawe watapewa mafunzo. Wajue ile kazi wanayofanya wapate kufaidika. Pia vile vile ninapendekeza kwamba upande wa kadhi. Mwenzangu hapa ameelezea katika upande wa kadhi - mi, mimi mapendekezo yangu ni kwamba Kadhi achaguliwe na ma-imamu au na waislamu. Asichaguliwe na mtu ama asichaguliwe na chama, ama asichaguliwe na mbunge wala Rais. Asanteni.

**Com. Abida Aroni -** Asante. Nehemia Nyambu?

**Nehemia Nyambu**: Mimi ninaitwa Nehemia Zombo Nyambu, mumesema, dakika tano tafadhali nitaka angaa nane.

kwanza uraia:- Uraia wa Kenya uwe ni wa Mkenya mwenyewe, na mzaliwa wa Kenya akiwa wazazi wake ni raia wa Kenya, basis apewe uraia wa Kenya.

Uraia namba 2; mgeni ana-ingiya Kenya anapopekuliwa aonekane hana nidhamu ya kutosha, aweza kuwa tu mkimbizi, wala asipewe uraia wa Kenya.

Raia namba 3 Wwakenya waendelee vile vile kupewa vitambulisho vyao vya kawaida.

Namba 2; Ulinzi na usalama wa taifa (i) Raisi abaki vile vile mkuu wa majeshi akizidi kuzipiga darubini vyombo vyake via usalama kama ziko imara. Vyombo vyake vya usalama ni nini? GSU, Polisi, Askali Jela na mabahari ya majini, Airforce angani na wengineo. Wasilale tu fwa halafu twavamiwa, tunama-lizwa, kwa hivyo abaki vile vile amri jeshi mkuu wa majeshi na silaha.

Ulinzi namba 2 (someone is talking this side) Lakini wananchi wakiwa wamelemewa na uchokozi wa majirani tunapo muliza hebu tupambane na hawa wanaotuchokoza.

Majirani azungumze nao welewane waache uchokozi. Kama hawata-acha uchokozi, uturuhusu atupe silaha tung’ang’ane.

Namba 3 Vyama Vya Kisiasa - Vyama vya kisiasa hutekeleza jukumu kubwa sana ki Democrasia, kwa mfano; mtu yeyote anasema kutizama kuungwa mkono au kupingwa, anapopingwa ndipo naye hujiuliza kosa liko wapi? Hapo ndipo hujirekebisha.

Vyama vya Ki-siasa 2 wabunge ni watu wazima, na ni waheshimiwa. Hatutaki makonde bungeni, hatutaki makelele bungeni. Speaker akimwona mtu nje, huenda akimtoa mtu nje kwa kwenda kinyume cha tabia ya bunge, mbunge huyo huyo asiachwe, apelekwe kotini.

**Com. Abida Aroni -** Tafadhali karibia microphone.

**Nehemiah Nyambu:** Vyama vya kisasa namba 3 vyama vipunguzwe idadi ya vyama; iwe nusu ya vyama vilivyoko 2002. Sijui ni kama hivi gapi. Kama ni hamsini, vipunguzwe viwe 25. Kama ni 41 vipunguzwe viwe 21 mwaka wa 2003, na kuendelea, kwani mapanya wengi hawachimbi shimo.

Muundo wa aina ya Serikali (i) Serikali ya Kenya iundwe na muundo wa majimbo, ambapo mamlaka ya nchi na bunge yatagawanya baina ya serikali kuu, bunge yagawanywa baina ya serikali kuu na majimbo maalum. Kwa mfano, Rift Valley Province, North Eastern Province, Nyanza Province, Central Province, Eastern Province, Coast Province, lakini namba 2, kila jimbo liweze kujipatia percentage ya nafuu ya wafanyi kazi. Kazi inapo patikana katika province fulani, ichukuwe wafanya kazi wengi zaidi. Kwa mfano, kazi ikiwa itapatikana Rift Valley, Nakuru kule, wao kama ni watu mia moja wapate watu 40. Halafu kuna watu wa Nyanza Province kutoka Kisumu wawe 10 halafu kuna watu wa Central Province kutoka Nairobi wawe 10 Halafu kuna watu wa Eastern Province Kitui wawe 10, halafu kuna watu wa Coast Province kule wanapatika, Mombasa, wawe 10 na kuwe na nafasi kumi za wale wageni – wa Tanzania, na wa Uganda.

Miundo ya Aina za Serikali namba 3 - vile vile serikali hiyo kuu itakuwa na wabunge kutoka kila mkoa, wakirundi mikoani kwao watakuwa wamekwisha peleka mikoa yao yasema aje? Na wakirudi walete serikali kuu yasema aje? Kwa mikoa, kwa wilaya, kwa mitaa au kwa taarifa( someone is talking this way);

**Com. Abida Aroni -** Mzee endelea. Hao ….. sisi ndiyo wenye kusikia.

**Nehemiah Nyambu:-** Bunge bunge namba 1- Bunge ibaki kuwa na waskali maalum. Huwapatia wabunge kuja kuwa na wakenya wanawakilisha kuchukuwa maoni na kupeleka maoni bungeni.

Bunge namba 2- Wabunge wafanye kazi kulingana na matakwa ya wananchi. Washauriane. Watafute ni lipi bora, na kutimiza badala ya wabunge, kwenda wakiongozwa na mawazo yao peke yao: hapana.

Bunge namba 3 - Chama kilicho na wabunge wengi, tafadhali, kwa mimi binafsi naona , wacha kiunde serikali .

Bunge namba 4 - Kuwe and mubunge wa kutoka kila chama katika viwango vyote vya serikali, majimboni, wilayani, kwenye

serikali kuu, kwa wakilishi watatu katika kila chama.

Mamlaka Ya Nchi

1. Raisi abaki na vipindi viwili, ya uongozi nchini, vya miaka mitano , mitano.

2. Ikiwa Rais in ua la waridi, la inchini, uaminifu wake na heshimu yake – uaminifu wake ni heshima katika nchi nzima. Jambo la aibu huyu Rais, anapolifanya hapo hadharani atakuwa ameihaibisha nchi na wananchi kwa jumla. Itambidi ajitetee kweli kweli au ----------------------

3. Mamlaka ya nchi, Raisi yampasa awe mbunge. Awe ana kura yake. Akipigiwa kura naye apigie kura wenzake ikiwezekana.

Mahakama - kwanza majaji wa mahakama wawe mahali fulani kwa muda fulani. Wabadilishwe badilishwe- transfers si saa zote ako Mombasa miaka 12 -- hakuna hio.

Mahakama namba 2: Maofisa mahakamani wastaafishwe kama wafanyi kazi wengine wafikiyao umri wa kustaafishwa kazini.

Mahakama ha haa! Ndugu sasa kadhi mkuu na makadhi wawachiwe nafasi ya mahakamani. Ma-kadhi na kadhi mkuu waendeshe kesi za waliooana kwa dini ya ndugu zetu waislamu. Wanapo hizi matatizo ya walioana yasi ----- yako kinyume cha ndoa yao iko nje na ndoa ya kiislamu basi wawache wahakimu mahakamani waendelee.

Sita - Mahakama ya kadhi kunakooneka uamuzi ungekuwa si wa kadhi, basi mahakamani basi tunawaomba wandugu waturuhusu, wahusika wanao pambana wakubali na katiba ambao tunataka ikipitwa kutaka rufani kwa mahakama wa mahakamani hakama kuu.

Mwisho - Serikali za mitaa - Meya achaguliwe and wananchi. Si madiwani. Kama Rais wa nchi anavyo chaguliwa na mwananchi.

Namba 2. Mishahara na malupulupu ya madiwani, shauri hilo liwachiwe wananchi wenyewe kulingana na hali na uchumi wa mitaa yao. Usiseme diwani kule elfu kumi na saba; sisi hatumuwezi. Elfu Kumi na saba tutatoa wapi? Tuwachieni wenyewe.

Namba 3 - Madiwani wateule wachaguliwe kwa njia ya mlolongo wa wananchi wa mitaani. Si mtu au watu, wachache fulani waseme tu ya kuwa tumemchagua ….

Nasikitika kumtaja huyo, Professor Yash Pal Ghai la la la la . Ni huyo, huyo Professor Yash Pal Ghai asimame, asimamishwe na wenzake, kama wananchi tunamtaka tutamininika nyuma yake bila wasi wasi, atapita. Mwisho.

**Com**. **Abida Aroni -** Sorry –

**Nehemiah Nyambu -** Waziri wa serikali ya mitaa anapotosheka na fujo na aibu inayo onekana magazetini, aibu inayo sikika, marandioni akusanye aibu hizo zote akamweleze Rais, aombe kibali cha kuivunja baraza ya mtaa huo huo. Kwani yeye mwenyewe peke yake kuivunja, sisi wananchi tutajiuliza amefuate fitina za miji mingine- fitina za watu fulani wanaotaka kuwatia aibu wenzi wao.

Muundo wa utaratibu wa uchaguzi:

i) Kenya naiomba kufuata mfano huo huo wa wakilishi katika uchaguzi.

ii) Mwenye kura nyingi abaki huyo ndiye mshindi lakini,

iii) Sehemu za wakilishi anapokuwa, inapokuwa wakipigiwa kura wakiwa na wanaume, na wanawake, mwanaume akiwa karibu au kukaribiana sana na mwanamke basi mwanamke apewe yeye ushindi. Haia- ai ai ai! Kwa mfano, hapa tunapiga kura, Kamau amepata 7,000, Karisa amepata 6,000, Kazo amepata 6,800, John amepata 5,500, huyu Kazo kwa kuwa amekaribia tumpe nafasi, yaani nayo twende mbele. Hawezi kushinda na (Giriama translation) basi hawezi shindana. Basi Kazo ahesabiwe mshindi – ikiwezekana.

iv) Kwa kuteteya hali ya uchumi nchini mwetu Kenya, ingelipunguza gharama kama uchaguzi utafanywa pamoja, kwa mfano mpiga kura apewe kadi tatu za rangi tatu, tofauti. Rangi hii ni kadi ya uraisi, rangi hii ni kadi ya mbunge, rangi hii ni kadi ya udiwani. Masanduku yawe vile vile ifuate zile kadi. Mimi nikienda, nikitia huyu ndiye Rais hapa, huyu ndiye mbunge huyu ndiye diwani rangi yake ni hapa najua kusoma sijui kusoma haya Rais, haya Rais, haya Rais. – Uhesabu wakura uanze masanduku ya madiwani, yamalizike, matokeo yatangazwe. Halafu masanduku ya mabunge yamalizike yatangazwe, halafu masanduku ya ma – Rais yamalizike yatangazwe.

v) Mwisho, mchunjo watakao chaguliwa, huwa na vituo kadha ya sehemu za kuwakilisha, kutumiwe muundu wa mlolongo. Mchaguliwa au wachaguliwa wawekewe siku za kufika kwenye vituo hivyo. Wasimame nyuma zao hata wehesabiwe. Mchaguliwa Jumatatu aende kwa mfano Kangundo – Alhamisi, Jumatatu, Jumatano; sikuitaja jumatatu, jumanne sikuitaja; apumzike. Jumatatu aende Kangundo akapate watu 300, Jumatano aende Mwala akapata watu 210, Alhamisi arudi Machakos Township hapo ajulikane apate 100, Jumamosi arudi Tala Market apate 100, ten thousand, na mwenzake kama amempita yeye ndiye atakuwa lakini kwanza kabla hajakuwa mbunge ama hajakuwa Diwani azunguke kwanza.

vi) Mchaguliwa, anapo ardhiwa alipe kiwango cha haba, walipa wasimamiaji wa uchaguzi kwani atakuwa amesaidiwa na wale wasiosimamiwa mlolongo na wakaanguka, wakati wa mchujo. Kwani mtu huwa kati ya watu wakusimamiwa mlolongo lazima awe ametoa TKK. Ametoa kitu kidogo kwa serikali. Wewe huwezi kuja

kusimama mlolongo tu bila serikali haijapata kitu! Lazima.

Haki za Msingi:

i) Hukumu ya kifo aha! Hukumu ya kifo itupiliwe mbali. Kwa sababu anayeweza kuwa ni yule anaye weza kujiua mwenyewe. Mtu kama hivyo huwa anajiona hana mbele wala nyuma. Badalaya kujiua akikashirishwa kidogo, amepata nafasi ya kuua. Anakuua, kwa hivyo si asiuawe? Afanywe je?

ii) Wanao-oneza ukimwi makusudi in wale wanaujuwa tu watakufa, watakufa. Kwa hivyo wanataka kuja na wenzi wao. Ameuua si usimuuwe? Umfanyeje?

iii) Kwa hivyo kama kuna katika, katiba ya kulinda haki za uhai – Kenya na iwe ya kwanza ya kujenga jela ya kipekee ya wale wanao ua wakae humo jela, wakifanya kazi za miradi tofauti, ama wawe na mashamba yao, wapike wenyewe, wale wenyewe, wauane humo humo jela. Hakuna halafu umeachiliwa; Kaa humo humo. Huawi.

iv) Kumtia mtu jela huwa mwamwonyesha mwingine huwa akifanya kosa kama hili na yeye atakuja ndani. Maanake yule amefanya, amefanya umfunze usimfunze kwake ni sawa. Asha ua asha ua. Auaye kwa nini?Kwa nini wasitengwe na watu maishani? Wao wote, wasiuawe.

v) Mwisho- Elimu ya bure , Haki za kimsingi . Elimu ya bure imekuwa 'headache' kwa wazazi, kwa pesa kidogo kidogo, zinazofukuza wanafunzi, kwa shule za msingi. Watoto wa darasa la kwanza mpaka la nne wasiulizwe hata shilingi moja ya choki ya shule. Wasome bure. Ki kweli! Si endeni nyumbani mkalete pesa za 'Watchman' huyu twataka kimlipa watchman nei nei si endeni nyumbani makalete pesa za anayepika hapa chakula cha mchana nei nei Shule za pesa za mjengo endeni mkalete – tuje tujenge hapa. 'One' mpaka 'four' waachwe. Darasa la Kwanza na la nne hawana utamu wa mwingi kwa kusoma. Mimi sijui ni kwa nini, sijui mwingine angesema nini mkioko hapa. Ama ni hawa ndugu sitaki kuwataja hapa. Hawatii utamu kwa watoto wa darasa la kwanza mpaka la nne? Mtoto wa darasa la Kwanza, la tatu asema a a a (Giriama translation).

**Com. Abida Aroni -** time? Nimekupa zaidi ya dakika kumi na kama una nia ya kutupa hiyo 'Memorandum' twakuhakikishia tutaisoma.

**Nehemiah Nyambu**- Basi, namaliza ya mwisho.

**Com: Abida Aroni** - Asante.

**Nehemiah Nyambu -** Thank you, Thank you. Asante sana.

i) Haki za makundi yanayoweza kuhudhurika, matatizo ya kinyumbani ya bwana na bibi yachunguzwe na wazazi wa bwana na mzazi wa bibi.

ii) Wazazi waitatue kasoro ipatikanayo, badala ya uchunguzi wa pande zote mbili abaye anasababisha matatizo hayo, kujulikana mara moja. Lakini haisikizi, – hazikizi ya pande zote mbili. Mke au aweza kuwachwa; arudi kwao, mume kama hataki kusikiza, apelekwe mahakamani. Nimemaliza ndugu.

**Com. Abida Aroni -** Asante tunashukuru.

**Nehemiah Nyambu** - Sikumaliza lakini ---------

**Com: Abida Aroni** - Tutasoma hiyo karatasi yako . asante.

**Nehemiah Nyambu** - Thank you very much.

**Com. Abida Aroni -** Zendele Charo Ngutu (Giriama Dialect) (Ngoja subiri mama)

**Zendele Charo Ngutu** - (Translator) Huyu mama anasema amekuja hapa kutoa maoni yake kuhusu haya mambo ya katiba. (Giriama translation) Anasema maoni yake yote yako hapa kwa Memorandum' Hii ni swahili. Anasema madiwani wanaochaguliwa katika kila eneo elimu yao kiwango cha chini kabisa iwe ni 'Form four' "O-Level". Hilo ni oni lake la kwanza.

Anasema katika mamlaka anayopewa Rais ni katiba awafikirie pia walemavu wasiojiweza katika jamii. Hilo ni oni lake la pili. Na hii 'memorandum' amesema atawapatia ili muweze kusoma lakini hao ni maoni yake huy u mama Zendele. Asanteni.

**Com. Abida Aroni -** Kaka Kingi Masha?

**Kaka Kingi Masha**- (Giriama Dialect - Translator) Anaitwa Kaka Kingi huu mama jina lake. Huyu mama anasema kulingana na maoni yake 'education' ya wasichana, elimu ya wasichana, katiba hiyo mpya inayokuja izingatie sana, kwa sababu wakienda mahospitali wanazalishwa na waume mara nyingi, watoto wetu wakike wasomeshwe kwenye jamii zetu.

Oni lake lingine la pili, anasema katika hiyo katiba mpya, inaokuja, kuwe na kipengele, wanawake watambuliwe na wawe na haki sawa kama waume – kama vile kuchaguliwa ma 'DO', kuchaguliwa polisi, ma –nurse wawe na nafasi nzuri kama vile waume kama ni 50/50 kwa waume na kwa wake pia. Asanteni. Anasema maoni yake ni hayo tu.

**Com. Abida Aroni -** Robert Toya Mwamure:

**Robert Toya Mwamure** - Mimi kwa jina naitwa Robert Toya Mwamure. Yaliyo nileta hapa ni mambo ya kibinafsi, ambazo- kitu ambacho ninaomba ni kwamba kuwe na urekebishaji juu ya malipo ya pesa za uzeeni, kwa wale ambao wana acha makazi. Kwa sababu utaona ya kuwa kuna muda mrefu ambao mara nyingi unachukuuliwa bila mtu kulipwa na ile inasababasha matatiso kuhusiana na mambo ya kinyumbani, mambo ya kielimu kwa watoto, yote yanamkumba yule mzazi ambaye kazi ameacha na pesa haupati kwa muda mfupi ambao unawezekana.

Kwa hivyo kitu cha pili ambacho ni naomba ni kwamba ma ofisi yale ambayo yanahusiana na mtindo ule ule ulipaji pesa za uzeeni yawe yataletwa karibu na mikoa yetu, ambavyo hakutakuwa na usafirishaji wa kusafiri na kwenda kuangalia malipo, utakuwa uko raisi kuliko kama hapa na Nairobi kuna ugumu kwa kusafiri kwa sababu ya mtu anakwamiwa kabisa na pesa mfukoni hana na inambidi asafiri aende kule kule na mapeni atakuwa hana, inambidi atakuwa anabaki vile vile. Nikitoa mfano ni kwamba kama mimi mwaka huu wangu ni wa sita na nimestaafu na sijapata malipo yoyote kutokana na pesa za uzeeni. Kwa hivyo hiyo ni jambo ambalo ninaomba tume hii ambalyo imekuja iweze kuingilia kitu hiki na kuwa cha shuluhisha jambo hili ili mtu kama mimi na wenzangu pia wengine wako, ambao, kama wako hapa ama kama hawakuja pia waweze kutekelezwa jambo hili ili waweze kuwa katika hali nzuri kama wenzao. Mambo yangu ni hayo ndiyo yalionileta kwa leo.

**Com. Abida Aroni -** Asante mzee. Reverend Philemon Ngona,

Mgona? Joseph George Kenga?

**Joseph George Kenga -** Mimi jina langu ninaitwa Jospeh George Kenga. Ah nina maoni kuhusu huu urekebishaji wa katiba, ama katiba mpya ambayo tunaitazamia tuwe nayo baadaye.

Kwanza, maoni yangu mimi, ninatake tuwe na serikali ya majimbo ambapo mamlaka ya wananchi na bunge yagawanywe baina ya serikali kuu na majimbo maalum.

Pili - Mambo yote, yafanywe katika mikoa, wilaya, kila jimbo litengeneze mambo yake na huduma ziwe zina patikana, katika – e – kama kwa e - - urahisi mikoani na wilayani.

Tatu - Serikali isiweze kuchukua ardhi ya mtu binafsi kwa nguvu. Maanake hivyo hufanyika na ni jambo moja ama lingine la kunyanyasa yule ama wale ambao kwamba huwa wamechukuliwa ardhi yao. Na ikiwa kuna umuhimu wa mahali hapo, kwa mfano iwe shamba yangu halafu papatikane kuna gold ama mafuta chini, kama serikali pale mahali inataka kuchukua,

maelewano yaweko ili kwamba niweze kulipwa.

Jambo lingine, serikali ya mitaa, isiwe na uwezo wa kuchukuwa ardhi za watu, kufanya wao ni wadhamana, wadhamini wa hizo shamba ama hiyo adhi, kwa vile mara nyingi huwa inanyanyasa wananchi. Na ikiwa ni lazima mahali kama sisi wenyeji kwa mfano hapa Ganze tumetenja mahali kama pale tutatengeneza mahali ya biashara yetu kuuza vitu vyote, tumejenga pale mahali. Serikali ya mitaa ikiwa inataka pale mahali, itabidi ielewane na sisi, na inunue kwanza, bei ambayo kwanza itaturidhisha sisi wenyewe, na baadaye ndiyo wapange mipango ya kutoa viwanja halafu watangaze watu wanunue hizo viwanja au wajenge mambo ya biashara zao. Maana bila hivyo mara nyingi serikali ya mitaa huwa inasema, hapo mahali tutalipa na hawatalipa wanatoa viwanja halafu watu wanalipa kwa County Council ama Serikali za mitaa na wale wenyewe pale hawapatiwi chochote. Na huu ni unyanyazaji wa watu. Kwa hivyo ikiwa sisi tuko kwenye Kenya, na tuko Kenya huru, na kila mtu alindwe na hii Katiba kwamba mahali kama hapo akiwa ni kwake, asinyang'anywe ama kuziingiwe wizara ama serikali ya mitaa kuchukuwa mahali hapo.

Jambo lingine- Katiba hii mpya tunayo iunda, ilinde sana wanawake kwa sababu mimi mwenyewe binafsi, nikiangalia hivi huwa naona kwamba kuna wonevu fulani kwa wanaume fulani huwanyanyaza wanawake fulani. Na hii si sawa. Kwa hivyo katiba hii ilinde kabisa wanawake. Yaani Wanawake watajwe kama mtu mwingine hapa Kenya. Sababu dhamana ni hii; mimi nitaoa bibi yangu kwa kupendana. Nikimweleza baba mtoto huu wa fulani ndiyo bibi yangu, baba ataenda kwa mzazi wa yule msichana waelewane kivyao. Atatoa mahali pale ampatie yule kiuele chake. Yule bibi yangu atakuja kwangu nikiwa nimemuoa kwa kupatana tu, yeye na mimi; lakini ile mahali ambayo imetolewa na baba kwa mimi mvulana. Yule msichana hatapatiwa hata ngombe moja. Atatoka kule akija kwangu ananifuate mimi kama ni mumewe na tunapendana. Tutakuja tutazaa hapa, watoto kama ni watano ama ni sita ama zaidi, ama hata wawili. Lakini baadaye, kwa sababu nyingine inaweza kutokea pale sababu ya mimi na yule mwanamke kuwachana – na hivyo huwa mara nyingi vina fanyika. Sasa yule mwanamke atarudi kwao. Wale watoto aliyo wazaa yeye na mimi, ikiwa damu yangu, yai langu na lake zimeungana zikazaa watoto ama mtoto. Sheria hasa hapa, nikisema hasa kwa miji kenda, wale watoto, yule mama wote anamwachiya bwana. Sasa hapo kwa unyanyazi umefika. Yeye na mimi tumejalika, tukapata watoto wawili au watatu. Tumesinyana sasa na tunataka kuachana. Kwa nini yule mama asipate angalao watoto wawili, au watatu? Kwa nini watoto wote wanaawachiwa bwana? Huko si kunyanyasa kivipi? na hawa watoto tumezaa mimi na yeye mwanamke. Kwa nini? Tena zile kazi zote alizo nifanyia huko kwangu nyumbani, yeye hakupewa hata dururu kule, alikuja kufanya kazi kwangu nyumbani, labda amemaliza karibu miaka kumi, akirudi kwao, ile mali nilio ipeleka kwa babake, ninaidai kwamba hiyo mali nirudishiwe; kwa sababu bibi tumeachana. Hizo kazi zote alizo fanya hapa alilipwa mshahara gani? Eh –hakuna mshahara wowote. Kupiga pasi, kunipikiya, na mambo mengine yale munayo yajua yote aliyafanya yeye. Halafu ile mali inarudishwa, watoto wanabaki hapa, yeye anaenda kubaki peke payke, bahati mbaya hatazaa tena kule, anaangalia tu watoto wa wenzake, hata mimi nilizaa kwa bwana Kenga, nina watoto kama wale. Hii si dhuluma hii? Kwa nini iwe si dhuluma? Hapo ndipo sababu nikasema katiba hii mpya ya Kenya ambayo kwamba tunataka tuiunde Wanawake iwalinde kabisa. Kama ni hivyo basi tumeachana, watoto wagawanywe. Yeye

apate wawili na mimi nipate wawili. Maanake tumewazaa zote.

Kuna jambo lingine ambalo mimi, ninaomba. Kuwe na haki ya watu wote. Sababu hii nikisema ni kwamba, mara nyingi, watu wanakosa haki zao. Kwa mfano mimi hapa leo nizushe vita, niangushane na huyu nimukate kate nimuue.Nishaa ua. Basi nataka katiba hiyo tunayo iunda iwe inalinda ile masilahi ya wale watu wanacho uawa. Kwa sababu mimi nitashikwa, niende gerezani, nimeharibu sheria, ni kweli umeua, ndiyo. Ok utafungwa miaka thelathini. Kazi yako ni kukata magogo huko na kufanya hivi na vile. Ni sawa. Nitakaa huko miaka thelathini natumikia serikali ile jasho langu lote linalotoka kule faida ina ingia kwa mkono wa serikali. Ni hivyo ama sivyo? Lakini ajabu ni kwamba yule niliyemuua hana chochote atakachopata . Halipwi chochote. Mimi naomba kuwe na ridhaa. Kama mtu ameua mtu mwingine ile familia yule aliye uawa ilipwe ridhaa, ili angalao ipanguze machozi kidogo kwa sababu mtu wao amekufa, mali inayotengenezwa na yule muuaji inaenda serikalini wao wanabaki kitupu. Hii naona hii – kama ni urafiki – na tunatengeneza katiba ya kweli, hapa kuwe na ridhaa ya kulipa yule ambaye kwamba mtu wake atakuwa ame uawa. Hayo ni maoni yangu. Na kama tunataka kutengeneza katiba ya sasa, nafikiri hapo inaweza kuwa sawa.

Jambo langu la mwisho ni hili. Hapa kwetu pwani wengi wetu hatujasoma sana. Lakini ile elimu yetu kidogo kidogo, wale walimu wa kilimo, walikuja hapa kutuelimisha kwamba tukizingatia jembe, ukulima unaweza tukafaidika. Hivo tumefanya, tukapanda mimea ambayo hiyo ni mimea iliyo ina mazao ambayo mazao hayo yanatusaidia sisi kupata chakula, kupata pesa za kusomesha, kupata pesa hata zakutengeneza mambo mengine. Ukitunza sana hata gari unaweza kununua. Lakini ubaya sasa, inasemekana kwamba si halali. Ki vipi? Na sisi wenyewe tumelima; tukapanda, na mazao yanatoka, tunaambiwa kwamba hiyo si hilali. Mumea huu ni mnazi. Mnazi umepandwa mwingi sana hapa Kenya hasa sehemu ya Pwani. Na huu mnazi hugemwa. Ukigemwa, unatoka tembo. Tembo lile ni nzuri kuliko 'beer'. Kama mtu ameoja mnazi hivi inavyo semwa, anasema yule mzee anasema ukweli. Lakini sasa tukiangalia hivi, kule kugemwa kwake ni kwa wasi wasi . Kule kuuzwa kwake ni kwa wasi wasi pia. Kwa nini katiba isiiweze kutulinda sisi na mimea yetu na vitu vyetu? Tembo hii ya mnazi kwa nini iitwe si tembo halali. Inaitwa tembo haramu kivipi? Kwani wale walimu wa Kilimo walipotufunza kwamba tupande minazi walikuwa na wazimu? Na kama sivyo, hivyo, si walikuwa wanasema tupande minazi ije ituokoe? Ikiwa ni kutuokoa mbona upande mwingine tunalaliwa? Hii sheria hii iko wapi hii? Hii sheria hii ni kutuumiza sisi watu wa pwani hapa, na hali hilo ni tegemeo letu kubwa. Tafadhali hii katiba kama inawezekana na tunaunda katiba ijayo ya haki na ukweli, hapa hakuna mwingereza, ni sisi waafrika wenyewe. Sasa vile vipengele vya mwingereza tunasema hizo tuondoe tuweke vyetu. Hii katiba iwe inalinda hii minazi na mazao yake ili kwamba tukigema mnazi, uuzwe bila matatizo. Ikiwa hata ni kuwekewa vilabu kama bia inawekwa kilabu unenda 'bar' kuna watu wanakunywa, wanakunywa bia, na tembo nyinginge ile ambayo kwamba ni mpaka uchanganye na nyingine ndiyo uweze kunywa. Munazi, ukigonga mnazi ni kwao kabisa. Unakunywa . Lakini inasemekana kwamba si tembo halali kwa vile nafikiri ukipita Taita huko mbele hupati minazi. Hii ndiyo inasemekana kwamba si sawa. Mimi ninaomba kama mwanakenya ninataka katiba iwe itulinde kwa minazi yetu tukigema turuhusiwe tugeme na tuuze tembo letu sawa sawa. Kwa hayo mengi, na hata kama mengine yako, pengine wanatazamia hapa nawapatia nafasi waje wazungumze lakini mimi yangu yalikuwa ni hayo .

Asanteni sana.

**Com. Abida Aroni -** Asante mzee Kazungu. Konde.

**Kazungu Konde**: Hamjambo wenzangu huko! Mimi nilikuwa nataka tu kuongea ama kuunga mkono hasa serikali ya majimbo.

Katika serikali ambayo tunayo sasa hivi, ama zile serikali ambazo zimeelezwa katika miundo ya serikali, tumepata ya kwamba nina matatizo kidogo. Kwa hivyo mimi kwa upande wangu ama maoni yangu, inahusiana na ------

Mimi nilikuwa nasema kuhusiana na muundwa wa serikali.

**Com. Abida Aroni -** Endelea tu.

**Kazungu Konde**: - Muundo wa serikali, nilikuwa nina unga mkono muundo ya serikali ya majimbo. Hiyo ndiyo maoni yangu.

**Com. Abida Aroni -** Shem Nyale?

**Shem Nyale:** Basi mimi kwa majina yangu ninaitwa Shem Icharo Nyale. Ni mwenyeji wa hapa Ganze, nimezaliwa hapa hapa, na hapa ni kwetu.

Basi mimi ninamachache tu ambayo ningetake kuwaeleza, juu ya Katiba hii mpya. Kwanza tunaweza kuwashukuru hasa wale ambaye walio shughulika miaka hiyo ya nyuma hiyo, wakishughulika na ile katiba ambayo imetwendesha kwa miaka thelathini na minane hivi sasa pia wale nao tusiwaache nyuma, twendelee kuwakumbuka. Sasa basi umefika ni wakati wetu ambao sisi nasi tunataka tupate katiba mpya ambayo ingetulinda , katika vizazi vijavyo.

Mimi kwa upande wangu ninasema kwanza, dola hii yetu ya Kenya iendelee kuitwa dola ya Kenya. Isibadilishwe jina lingine. Iendelee kuitwa dola ya Kenya.

Pia vile vile kuna uraia. Siku hizi uraia umekuwa wa kielevu sana. Unaweza ukapata mtu kwa vile ambavyo anajua jina kiswahili ukamwona na akasema mimi nimezaliwa hapa kwa kuwa amepata kitu kinachoitwa birth certificate. Sasa birth certificate ile, ameenda kule kwa watu wa Immigration wale ameonyesha na ameonekana ni raia wa ukweli na amepata passport na sasa huyu hatuwezi kumwondoa mahali hapa. Tunasema huu uraia atakaye kuupata akiwa hakuonyesha birth certificate ya kutoka 1963, basi tu ameonyesha birth certificate ile passport mpya na anataka uraia wa Kenya, awe ataonyesha birth certificate ya nyanya yake, au ya babu yake, basi huko mbele kuanzie kufuatwa fuatwa mpaka pale mahali alipofika. Asijipatie tu hivi hivi. Ni upande wa uraia huo.

Tunakuja kwa upande wa usalama. Tukisema vyombo vya usalama hapo, kuna jeshi letu kubwa, kuna jeshi la polisi, kuna prison na kuna wale watu wa immigration. Hivi tunasema ya kwamba katiba iwaothoreshe hawa, wawe watakuwako, waendelee , kama ilivyo hivi sasa. Hapo tunakuja tena.

Tunasema siasa. Katiba hii mpya naiongeze siasa ikiwa ni ya siasa, hata kama ni vyama arubaini. Wale na waendelee. Wasikatazwe na mtu. Mwisho watachoka na watavyacha. Wataacha kile chama kinacho tawala, kitawale, lakini mtu anaye piga kelele hata mimi nikitoka na bibi yangu, kesho nikisema mimi chama changu kinaitwa Ganze, basi niandikeni: Niendelee kupiga kelele humo Ganze. Nisikatazwe, maana nina uhuru.

Pia Serikali yetu sasa hapo pasikilizeni vizuri basi.. Serikali hii yetu ambayo ingetawalwa na Katiba hii, mimi ninapendekeza kwamba, iwe na Rais, na mamlaka yote, awe nayo. Mpaka akipita hapa tuwe tunaona gari la Rais anapita. Mimi ninataka serikali hiyo iwe na Rais mdogo. Tukisikiya Rais mdogo ndiye atakuja kutuchangisha Ganze tujue Rais mdogo anakuja. Mimi ninataka serikali hiyo iwe na mtu ambaye anaitwa Prime Minister. Waziri mkuu ambaye tutakwenda tukimtuma huko tukimwambia nenda kule Tanzania, nenda uganda, nenda huku ukashikane na wenzako ulete mashauri mazuri mazuri.

Prime Minister aweko - Pia huyu naye awe na mdogo wake. Tunakuja upande wa Bunge. Bunge liendelee vile vile, labda hata kama kukitokea mahali pengine ambapo kuna upungufu, basi hapo mwenye kiti yule wa tume ya wabunge, huyo aangalie akiambiwa maneno kwamba hapa mahali panaweza kuongezwa mbunge, na aongeze. Lakini mamlaka yale ya bunge yasitolewe yabakiye vile vile ilivyo.

Hapa tunakuja mamlaka ya nchi - Mamlaka ya nchi ni kama hivi leo. Tumetayarisha katiba yetu. Katiba yetu ina vifungo kadha wa kadha ambavyo tumesema zimewekwa. Lakini hapo hili bunge nalo, linafanya fanya kule na kubadilisha ile ambayo tunasema. Kwa hivyo hii bunge, ina – ‘amend’ kifungo fulani ambacho bado hawaja ruhusu kwa serikali. Ni lazima sisi wananchi kwanza tuhusishwe, kwamba kifungo fulani kinabadilishwa basi kila mmoja sisi watu wamashinani tujue kwamba kifungo kile , kinabadilishwa. Maana hii Katiba ambayo sasa inatulinda hii wakati huwa tunaambiwa kwamba ilibadilishwa mara saba. Lakini sisi hatukwambia. Hivi sasa ikitaka kubadilisha basi tuwe tunahusishwa , tujue tutakubali hatukubali. Hapo mwenye kiti ningali naendelea kidogo! Tunasema upande wa mahakama . Hizi mahakama na ziendelee kama zilivyo. Lakini kuna mahakama moja hapa ambayo, kama ingewezekana inge-ondoka. Maana hii inaonekana kwamba haimfai mtu kabwera kama mimi. Kwa mfano, kuna mamlaka yale ambayo ni ya kizazi. Nikwa nini zote tunalindwa na katiba na huyu awe ana mamlaka yake? Unaona kwamba mimi nikiwa nimeoa msichana wa Kigunya, na jua huyu ni muislamu, Na nimekaa naye. Amezaa watoto. Mimi ni Mkristo na yeye ni mwislamu lakini hatugombani maana sisi tumeoana. Dini hazitutenganishi. Lakini yeye akitaka kuondoka pale, haendi kushitaki kule kwa serikali kwa mahakama ya kweli. Anaenda kwa Kadhi mara siku nyingine tunaona hivi vitu vyangu vyote vinakuja kuchukuliwa vinaenda huko. Na nikienda kotini kule siwezi kujua kwamba nitasema – hata nikiwa na wakili, wakili wangu hatanisaidia lolote. Kwa hivo hii mahakama ya Kadhi iondoke. Katiba hii iwe haiko.

Serikali za mitaa - Hizi serikali za mitaa, wale madiwani wenyewe, watang'ang'ania kule, huko na huko. Bi mwenyekiti kuna wakati, wengine walisoma, wengine hawakusoma, huku kwetu. Na wananchi wanampenda haiwezekani. Ukisema anapigiwa kabisa vigelegele, na yeye hajui kusoma. Tunasema huyo anaye jua kusoma, na yule asiyejua kusoma, hawa wote wachaguliwe. Wakienda kule wanapo kwenda kule katika 'council' hebu natuwaache wenyewe kule wang'ang'aniye. Lakini watafute yule ambaye alikuwa amesoma na amepata kura. Basi huyo awe mwenyekiti wa 'council'. Kuhusikana na wale ' nominated councillors' wale, wale hatuchagui sisi. Wakati mwingine wetu wanatafuta 'record' ya mtu ambaye amefanya vizuri kwa serikali – amefanya kazi jema na huyo mtu sasa wakati wake umekwisha, amewacha kazi. Ni juu ya serikali yenyewe kuangalia huyu mtu tumfanye je. Tutampa ubalozi, tutamfanya aje? Na tumpe huu nominated huu. Kwa hivo hiyo kitu hatuwezi kusema awe atapigiwa kura. Huyu asipigiwe kura, na apewe. Tunarudi tena hapo?

Uchaguzi - Huu uchaguzi tulikuwa tukiufanya kwa mlolongo. Tunasema kwamba amepita kwa mlolongo. Lakini wakati mwingine unaleta shinda kwa jamii, maana bibi yangu yeye anamtaka yule, hamtakaye, lakini yuko pale anakondoa macho anasema – he – kama si huyu, ningempigia huyu. Tunaseka uwe wa siri. Uchaguzi na uwe wa siri.

Tunakuja upande wa ardhi- Utanisameheya kidogo, Bi mwenye kiti hapa. Wale watu waliotoka Mascat miaka hiyo ya nyuma 17 centuries huko. Walikuja hapa baharini hapa pwani hapa wakawapata babu zetu wamekaa pale. Wanalima, wanapanda minazi yao, basi wakaja na watu wanaitwa wa Mazrui.

Walipofika hapa, wale Mazrui walichukuliwa na hawa wa Muscat kule kuja hapa kwa sababu ya askari. Wale walikuwa ni askari na wale Muscat wakiluwa wale ni ni- ndiyo wafalme. Basi hawa askari walipokuwa hawana mashamba. Sisi hatujui, wao wana silaha sisi hatuna, wagiriama. Basi kutoka pale Lamu, Kiambooni mpaka pale Vanga wakaangaliya huu upande wa msha wa juwa wakasema hawa watu na tuwabulute waondoke hapa. Basi hapa waka tuburuta mpaka maili kumi. Halafu walituburuta maili kumi hapo, hapo mahali pakaitwa Mwambao wa pwani. Jina hili limekuwa zimezeoleka sana hata hivi hata hawa watabiri wa hali ya hewa nao wanatabiri baadala ya kutwambia Kenya zima wanatwambia mwambao wa pwani na utakuwa leo kutanyesha mvua. Kwa hivyo walipotufukuza pale walitwambia nendeni huko nyika. Basi tumekuja huku nyika lakini sasa kule hatuwezi kurudi tena. Tukifika wanasema hapa ni kwa Bin Salim. Hapa ni kwa fulani. Tunataka hivi leo katiba hii ukitoka hapa mwenye kiti uwaambie kwamba watu wa Ganze wamekataa pale kuitwa Mwambao wa pwani. Ukiitwa, na uitwe Mkoa wa pwani. Lakini kule kuitwa mwambao wa pwani hilo jina tunataka liondoke. Tukirudi tena hapo kwenye ardhi, hapa kwetu kuna tabia moja, tulikuwa tanaendelea vizuri. Lakini hive juzi juzi kulikuja kamati moja ambayo inasemekana hii inatumwa na – imetumwa na - imetokana kwamba hawa na kamati ile ya mashamba. Hii kamati ya mashamba haijui chochote. Anayejuwa chochote Bi mwenye kiti ni Mzee wa kijiji. Huyu ndiye anaweza kujua kwamba ni Shemu pamoja na babu yangu na nyanya yangu, tumekuwa hapa toka 15 century tuko hapa. Maana aliambiwa ambiwa akambiwa mpaka tumefika sasa. Lakini huyu tu anakuja na zile sheria ehe! Nionyeshe ehe! Nionyeshe. Mti yule, mti yule na mwisho tunabakiya tunazozana hapa. Tunataka hii kamati hii yamashamba hii iondoke. Isiwepo katika katiba hii mpya. Mzee wa kijiji na awe

ndiye mwenye kuangalia hiyo mambo ya ardhi hizi zetu hizi. Tukirudi tena hapo hapo, tunataka hiyo serikali itwangalilie, itafute pesa kwa uharaka, maana tulipo amwiwa twende huko nyika, basi huko nyika hatukuja gawanywa, hata sasa. Tunataka huku nyika tugawanyiwe kila mmoja apate mahali naye, apate kitu ingalao anaweza akaenda akatowa mahali kikamfaa. Imekua nyika na hatungawanyiwi. Kwa hivyo kwa katiba mpya na iwe na ugawanyaji wa mashamba huku tuliko.

Katiba hii tunataka ilinde wale watu wadogo wadogo. Kwa mfano juzi ulikuwa Bamba kule Bamba huko mbele huko karibu na Tsavo National Park huko, Kuna kabila moja inaitwa "Wariangulo" ni wachache sana wale. Lakini nao wana mbunge wao in Mheshimiwa Waziri Noah Katana Ngala - Lakini ni wachache. Hawawezi kumpata hata councillor ni wachache. Lakini tunataka pia hao nao wajulikane kwamba wako kule Dede. Hawa Wariangulo hawa, ili nao wapatiwe kuwamo dani ya katiba wawe wanajulikana - Tunawaita Wasanya wako kule ndani huko. Basi hii katiba mpya nao wawemo. Katiba hii mpya muwe na mlemalo viwete. Katiba hii mpya muwe na wale wasiyojiweza. Wote wote wa kila aina wawe wote wanaweza kulindwa na katiba hii. Basi ninaendelea kidogo, utanisamehe Bi Mwenyekiti.

**Com. Abida Aroni** -Maliza mazungumzo yako sasa.

**Shem Nyale**: Nafupisha sasa. Tunataka hii mali ya siri kama pembe za ndovu, kama mawe yaliyopatikana , basi serikali itunze vizuri ili kwamba hizi zikipatikana zinaweza zikaleta ushuru ili ushuru ukaweza kuwafaa wananchi.

Tunasema tena mazingira. Tunasema mazingira, katiba hii mpya iwe na kifungo kinacho sema kila mwananchi aweze kupanda miti mahali alipo ili kwamba miaka ijayo kila mmoja ajipatie, miti ya kutosha, ya kuuza ya kufanyia ya kuuza ya kuni imfae.

Hapa kunakuja shirikisho. Shirikisho hili tunataka serikali yetu iwe na ushirikiano wa siku si ----watu wote, hata kama ni wale North Korea. Tunataka tukimutuma pale Prime Minister wetu kufanya kazi, kwenda kuzungumza mkutano ule na aende na wakapatane huko huko. Serikali yetu iwe na shirikisho na kila mmoja. Uhusiano uliyo mzuri.

Uridhi: - Uridhi na uandikwe kila mmoja ikiwa ana haki ya kupata uridhi, hebu kifungo hiki na kiangaliwe na uridhi uwe uweko. Basi Bi mwenyekiti ninaondoka maana nimekula wakati mwingi kidogo. Mimi ninataka vitabu hivi vyenu ambavyo manvyoandika hivi sasa mtakwenda kuviandika huko Nairobi. Tunataka kuwe na ofisi kamili na ofisi kamili hiyo, si muwe mumeandika na mwondoke? Hebu nakuwe na ofisi ambayo itavilinda mpaka Yesu aje, analinda hizo vitabu vyenu hivi.

Hapa kuna tatizo lingine. Sisi tuwazee lakini tunaambiwa twende hapa Kilifi twende tukatafute pension yetu kama wale ambayo wamefanya kazi ya serikali- ukifika vizee haviwezi kusimama, na inaambiwa bado, bado pesa zenu kuja, kinashika mti kinakungua pale kinaanguka mara mnakimwagia maji; tunasema kwamba hii ofisi, hii pension itumwe hapa kwa Divisional

Officer tupatiwe ofisi, ili twende hapa tukachukuwe badala ya kwenda Kilifi, pesa si nyingi tena zinamalizika na hawa wenye magari na kule napo kuna shinda ikawe siku mbili, wiki mzima uko pale una zingonja. Tunataka zije hapa. Basi kuna kitu kingine ambacho vile vile kinatuhangaisha.

**Com. Abida Aroni -** Asante Mzee. Lazima sasa nikuombe uondoke tafadhali.

**Shem Charo Nyale** - Basi nilikuwa na moja.

**Com. Abida Aroni:** Asante tungempata Lucas Mangi Ngota, na kuanzia sasa , nitakuwa strict na time kwa sababu kuna watu ambao watakosa nafasi, ikiwa mtu mmoja atachukuwa zaidi ya nusu saa. Dakika kumi tafadhali mzee.

**Lucas Mangi Ngota:**- Basi mwenye kiti, pamoja na wote ambao wamehudhulia hapa, bila shaka nafikiri kama umesika mambo mengi kwa watu wote waliosema hapa, sio kwangu, maanake najua wazi kwamba, maneno mengi sio kitu, isipokuwa ni kuangalia vile ilivyo.

**Com. Abida Aroni –** Majina yako tafadhali.

**Lucas Mangi Ngota**: - Mimi ninaitwa Lucas Mangi Ngota, kutoka Dungisha Location Division ya Ganze. Nimekuja hapa langu ni kuwapeni shukrani sana kwa jinsi mnavyo tatua mambo ya katiba. Basi mimi langu ni hivi. Sina mengi.

Kenya ilikuwa juu ya mukoloni ikatawala miaka mingi sana. Tulipoona wazi kwamba tunanyanyaswa na wazungu tulijaribu kutafuta njia ya kupata uhuru wetu. Tumefanya kazi ya kutosha. Tumeunda vyama, vingi, katika Kenya. Baadaye, ikawa lazima tupate mwanzilishi wetu alikuwa ni Mzee Jomo Kenyatta ambaye ni hayati akawa alishikwa, akapelekwa huko Kapenguria kwa jela na wazungu, lakini wazungu walipotuona vile tunavyo fanya sisi wenyewe mmoja wapo ilikuwa Nyiko, tulikuwa tukipigana na kupigana kwetu kulikuwa ni kla ---- sasa hii ni nini? Kila mtu kwao. Kama ni hivyo kila mtu kwa, mzungu kwao na kila mkenya akae katika nchi yake kwao. Hio ndiyo jambo letu tuliyooanza mpaka mzungu alipo piga picha, akaona hawa watu wanasema kweli. Wakakataa kutupa sasa uhuru. Wakatupa nafasi sasa ya uhuru wale viongozi wetu wakashirikiana kwamba sasa hatuwezi kuanza kuchukuwa madaraka na mzee wetu aliye mwanzilishi yuko ndani. Tukakuwa tumefanya vibaya sana. Waliongozwa na roho mtakatifu, hawakuwa wachoyo. Wakafanya bidii, wakaenda wakatoa maoni kwa wazungu na wazungu wakamtoa mzee Jomo Kenyatta aliyekuwa ndiye alianzisha hiyo kazi. Wale wenzangu ambao wana umri kama wangu, wanajua, watu wengine walipata hata vyama huko vinaitwa mau mau, vyama vingi sana vilipatakina. Basi tulikuwa tuna chama chetu katika pwani,

**Com. Abida Aroni**: - Excuse me. I am in charge here. What's the problem? Kuna nini? Wacha mzee azungumze, what's the problem?

**Lucas Mangi Ngota -** Kule pwani kulikuwa tunao chama chetu cha KADU, na huko bala kulikuwa kuna vyama vingine,

lakini mzee alipotoka jela, akatupa nafasi sasa yakwamba, tuunde chama kimoja kama tunataka uhuru kamili, wenye furaha ambao una baraka. Viongozi wetu wote wakuwa kakubaliyana na mzee vile alisema. vyama vyote vikavunjwa, tukachagua chama cha KANU kuwa chama cha Kenya. Kitu ambacho nataka nimalize tafadhalini poleni sana. Tena sana sana – tena mjifikiriye sana. Baada ya kupata chama cha KANU serikali ikaundwa, tukaanza kuendelea na serikali takatifu. Hali na wasiwasi. Wenzetu wa bala, hawa ndiyo walituomba tuvunje vyama vyetu tuunge chama cha KANU wakaanza kukiacha chama cha KANU na kuunda vyama vingine tena. Vyama hivyo vilipoingia, kumeanza kutokea mambo mengine ambayo hayana umuhimu wala hayana imani. Basi, haya tumeyaona, na sasa kama tunataka katiba mpya, tunataka Kenya irudi kuwa na chama kimoja cha KANU. Wote wawe na chama kimoja cha KANU. Rais awe mmoja na tuwe tunaendelea na taratibu zetu. La sivyo, basi tupate serikali ya majimbo. Kila jimbo lijitawale lenyewe, liendelee na mambo yake. Sitaendelea na mambo yoyote mengi isipokuwa hayo muyapate, mwende nayo na muya fikiririe sana. Asante sana.

**Com. Abida Aroni**: Asante . Kazo Kangu Kiti?

**Kazo Kaingu Kiti:** (Translator) Jina naitwa Kazo Kaingu. Mimi sina maoni mengi. Yale yote yalisemwa na wenzangu waliyotangulia nayaunga mkono. Mimi nasema kwamba wale wanao tudhulumu waache maanake hata mimi niliyosomesha watoto wangu, wakamaliza darasa la nne lakini ile kazi wanayofanya si – ni kazi ya hapa na pale. Kwa hivyo hii Katiba ambayo twaiunda nataka iwe Katiba nzuri maanake mimi bwanangu hawezi kufanya kazi yoyote kwa hivo a – a niko na mashaka tu. Kwa hivo Katiba hii itatuwe tabu zote tuione ni katiba mpya kabisa tuionee raha. Hayo tu ndiyo yangu.

**Com. Abida Aroni:** David Mwaringa?

**David Mwaringa: -** Basi asante sana Bwana Mwekete, mimi kwa jina ni David Kamuto Mwaringa. Basi mimi nitaanza tu kufuatiliza wenzangu lakini, kitu ninacho anza sasa ni uongozi. Kwa sababu sisi hatuna mfalme, tuna viongozi. Hatuna mfalme Kenya. Tuna viongozi. Kwanza nitaanza na elimu ya msingi. Kama inawezekana katiba hii, elimu ya msingi iwe ya lazima na iwe ya bure. (clapping) Elimu ya Msingi iwe ya lazima na iwe ya bure, na ikiwa ya bure , iwe ya bure kikweli. Isiwe ya bure hapa na pale. Iwe bure ya kikweli. Yakukanyanga sawa sawa chini. Kwa sababu hutambua elimu ni ya bure, kesho mtoto ameenda – ameeambiwa aende, kesho kutwa mtoto anambiwa aende na elimu ni ya bure. tunataka ikiwezekana katiba hii ya Kenya, elimu ya msingi, iwe ya bure, bure ya kikweli. Sibure ya kubandiya. Mmeshika hapo?

Kuhusu Rais tunataka katiba hii ya Kenya yetu ijayo iwe na Rais mwenye nguvu. Rais ambaye ana mamlaka ya kila kitu. Majeshi aandike mwenyewe, mawazili ateule mwenyewe, ma Permanent Secretary andike mwenyewe, kila kitu aangalie mwenyewe. Makamu wake wa Rais achaguwe mwenyewe, kwa sababu kuna kipengele hapa cha uraisi. Kila mkoa wa Rais hupata percentage fulani ya kura. Na akipata zile, huwa ndiyo amepata. Anaweza akaongoza. Na huo mtu akifika hapo, ni kama amependwa na Kenya nzima. Hakuna haja ya hapa na weza hapa hawezi. Hiyo itakuwa ni kama jimbi lilotolewa minyoya huku nyuma. (Giriama translation) Tunataka Rais wa nguvu. Rais ambaye akipita hapa anaonekana amepita Rais.

Akisema kitu Rais amesema – ni basi – lakini si Rais wa kule anafika kule hafiki. Sasa lile suluali atakuwa amevaa huku ni fupi huku ni ndefu. Itapendeza ya hali namna gani? Hiyo katiba ijayo iwe na Rais. Rais ule wa nguvu za kutosha. Makamu wa Rais achaguwe mwenyewe, mawaziri aandike mwenyewe, ma Permanent Secretary aandike mwenyewe- Rais wa nguvu. Si Rais wa kwenda mnyonge mnyonge tu. Na amechaguliwa ni kila mkoa. Maanake hawa ma rais kila mkoa anapata kula fulani ambapo mpaka apate hizo, ndipo awe Rais. Kwa nini sasa amepata zile, kisha awe Rais wa pole pole? Hatutaki Katiba ya namna hiyo. Tumepita hapo?

Kipindi cha kuongoza: Kipindi cha kuongoza ile miaka mitano anatosha kabisa. Lakini si kwamba mtu akimaliza miaka 5 hawezi kuwa kiongozi. Tunataka kama ni mke, kama ni mtoto, kama ni mzee, akipendwa na watu, aongoze. Sio akiongoza miaka 5 ile kipindi inatosha, lakini akimaliza ile miaka 5 aje tena kwetu; aje aombe kura. Tukimpenda, aongoze tena. Hakuna maximum ya kuongoza. Maanake maximum ikiwekwa – Katiba ikiweka maximum, kutakuwa na ufisaji ambao hautakuwa na mpaka. Maana akijua mwaka huu ndiyo wangu wa mwisho huu, nikitoka hapa nitaenda nyumbani, anaweza kufanya mambo makubwa sana. Anaweza kuchukua laslimali ya hapa Kenya nzima akaipeleka mahali pengine. Anajua hakuna kitakachopita, ikizidi sana – nifungwe tu. Lakini akiwa amefungwa na watu wa Kenya wanasumbuka, hiyo ni namna gani? Kwa hivo kutawala hatutaki kuwe na mpaka sisi. Tunataka mtu atuongoze, kwa kura. Maanake sisi hatutaki kutawaliwa tunataka kuongozwa. Sababu hatuna mfalme sisi. Awe mke, awe mtoto, awe mzee, akipendwa na kura, atuongoze. Nimepita hapo.

Waziri mkuu: Mambo ya waziri mkuu huku kwetu haifanyi kazi yoyote. Ile mambo ya waziri mkuu ile, ni mambo ya kuingiza, ni mambo ya wageni, (Giriama dialect, translation) sijui kiswahili itaeleweka hiyo? Tonzi ya kuigiza haiwezi kufika hapa mdomoni. (Clapping) maanake wewe imeigiza mwenzako vile anavyofanya na pengine wewe hutaviweza, sasa ikifanya hivi ukifanya hivi, inavunjika hapa kama ni maziwa, yakuchafua, kama ni mchuzi wakuchafua, kama ni kunde za kuchoma, kama ni poja, zakuchoma, mambo ya waziri mkuu sisi katiba yetu hatuna aja nayo. Tunataka Rais na makamu wake. Rais na makamu wake ndiyo aongoze nchi hii. Nimepita hapo.

Nimekuja majimbo: Majimbo imefika wakati wake. Majimbo imefika wakati wake!. Kwa hivyo serikali ya majimbo iweko! Maanake wakati wake umefika. Ukizaa mtoto, akiwa ni kama yule, basi atakuwa mkubwa hasa akiwa mkubwa, hasa mambo ya vile alivyofanya, hafanyi tena. Kwa hivo majimbo imefika wakati wake. Lakini majimbo ile tunayotaka si ile ya mtu wa bara kwao, muzungu kwao, mjaluo kwao – ala – hatutaki hiyo. Tunataka majimbo ya kuangalia hilo jimbo, hata kama ni mzungu yuko, kile tutakachopata cha kijimbo, kikigawiwa naye apate. Kwa sababu yuko jimbo hii. Lakini tunataka vile vitu – yale mapato ya majimbo kama vile Kilindini pale, kama mtu atajenga mtambo wake, iwe first stage ya majimbo, ipite. Ikiwa iwe tupate 75% na 25% iende kwa serikali kuu. Halafu serikali kuu itachanganya na majimbo mengine. Hatutaki yale majimbo ya

mtu wabara kwao, mwarabu uende hivi, hiyo katiba haitafaa kitu. Italeta vita bure. Lakini majimbo imefika wakati wake. Na hapo nimepita, sasa nitaongeza ongeza kidogo. Kwa sababu ya kusema majimbo imefika wakati wake hata ule mji wako, unaweza kuwa una watoto 10 na ni watoto wako, amri wanachukuwa kwako, lakini chakula mtu anapika na bibi yake, na watoto wake. Lakini ikiwa ni mashauri ya kufanya kitu, haya, ataita watoto wake awachanganye. Kwa hivo majimbo si kwamba iwe inapinga serikali, serikali tunataka ile kuu ya Rais mmoja, lakini majimbo iweko. Mambo ikitoka kule tukishagawiwa tukiambiwa jimbo la pwani mapato yake ni haya, tugawiwe, watu wote ambao wako jimbo lile. Bora tuwe na nyumba yake. Asante ni kwa kunisikiliza. (clapping) Naenda kwangu.

**Com. Abida Aroni:** Joo huku mzee kujiandikisha. Asante. Karisa Kahuho (Maandishi hayasomeki vizuri, kwa hivyo kama kuna mtu ana jina ambayo linafanana na hilo- ) Karisa Kagohu.

**Karisa Kagohu:** Mimi Karisa Kagohu. Haya (Giriama Dialect) Translator – Mimi naitwa Karisa Kagohu. Nataka katiba ambayo tunataka kuiunda iendelee kwa uzuri. Isiwe na katiba ya fujo yenye kuingiliana hapa na pale. Sina zaidi ni hayo tu.

**Com. Abida Aroni:** Bahati Charo Ngutu? (Giriama dialect)

**Bahati Charo Ngutu** (Translator) Jina langu naitwa Bahati Charo kutoka Petanguwo. Maoni yangu kwanza kabisa kuhusu hii katiba mpya tunayaunda ni kwamba elimu ya msichana iendelee bila wasiwasi. Isiwe kwamba msichana ameenda shule wewe mzazi unatafuta mtu wa kumwozesha. Mimi Mzazi unatafuta mtu wa kumwozesha. Mimi mzazi wa kike nikisikia kama hayoo, yatanikera maanake umemwozesha mtoto wangu wa kike. Kwa hivo nasisitiza wavulana na wanawake wawe na usawa na wasichana wasiuzwe. Mimi kama mwanamke nataka pia niridhi mali ya baba, nisiwachwe nje. Kwa hivi, hivi sasa, najua hapo nyumbani babangu ana, mali kwa hivo nitasumbua nikiwachwa nje. Rais wetu apate mamlaka . Basi.

**Com. Abida Aroni:** Asante mama kwa maoni yako. Raphael Nyesi?

**Com: Abdirizak A. Nunow**: James Kahindi? Ok.

**James Kahindi**:- Habari zenu. Basi nashukuru kwa kupata nafasi hii. Ningependa nitoe maoni yangu kidogo sana. Kwanza, ningependa kutoa maoni katika katiba hii ambayo tunaitayarisha kwa wakati huu. Kwamba, ikaweze kuzingatia zaidi kwa kila mwananchi ila akaweze kuinuka ki maendeleo. Mimi nimewahi kutembea katika nchi hii ya Kenya na nimeona kwamba kuna sehemu nyingine ambazo kwamba hazishughulikiwi ki sawa sawa. Utaona kwamba sehemu nyingine zimeachwa nyuma tena sana sana, na kuzifikia zile zingine, ni hali ambayo, kwanza itakuwa unaweza – ni – vingumu sana. Kwa hivyo, katiba ambayo kwamba inaondoka sasa inaonekana kwamba ilikuwa haizingatii sana usawa katika sehemu kama za mabarabara hivi, sehemu za elimu, utaona sehemu za misaada inayotoka kutoka ng'aambo utaona kwamba, ilikuwa haizingatii sana sehemu zote.

Ilikuwa inazingatia sehemu chache tu.

Pili: Nilikuwa ningeyapenda pia kutoa maoni yangu kwama katika ile katiba ijayo ikaweze pia kutetea yule mzee ambaye amestaafu. Maanake kwa wakati huu, ile katiba ambayo iko na sithani kwamba inatetea yule mtu amestaafu kwa sababu unaona kwamba anayule mwajili anajua kabisa kwamba huyu mtu atastaafu wakati fulani. Lakini mwajili ataendelea mpaka mstaafu atakapo wacha ile kazi basi ataweza kukaa muda mrefu sana bila kulipwa. Na ni matatiso kabisa katika yeye na familia yake.

Pia vile vile kuna sehemu fulani ambayo kwamba tunayaona yana endelea katika katiba ilioko sasa. Sehemu ile ya uteusi wa wale eh wabunge – wale kumi na wawili. Mimi ki maoni yangu, ningefikiria kwamba ingeongezwa. Badala ya kumi na mbili (12) ingeongezwa kufuatana na zile Districts ambazo ziko hapa Kenya. Kila district ipate mmoja. Maanake inaonyesha kwamba kila district haikosi mtu ambaye kwamba ana uwezo wa kuteuliwa. Kwa hivyo, unaona kwamba watu kumi na mbili ni wachache sana, na inakuwa vigumu sana watu kuwa wataweza kupata eh – kitu kama hicho. Pia vile vile nilikuwa nataka kuzungumza – kutoa maoni yangu katika katiba hii ambayo inakuja sasa.

Kuna sehemu moja tunamwita e – e – ya yule tunayemwita public trustee. Huyu mtu nafikiri madaraka haya yangeondolewa kwake. Maanake kwa sasa utasikia sana DC, bwana DC, na pengine mustaafu ameaga dunia. Utaona kwamba zile pesa zake kuzipate ni hali ngumu sana, zinapitia kwenye mikono mingi sana njiani, mpaka zikimfikia yule mwadhiliwa basi huwa imechukuwa muda mrefu sana. Kwa hivyo nilikuwa – ki-maoni yangu, ingekuwa sehemu kama ile ingepelekwa kwa chifu direct. Nafikiri ingem saidia sana wale ambao wameadhiliwa na hali hiyo.

Na huu utawala wa mikoa mimi naona ni mzuri ingeweza kuendelea isipokuwa pengine uwe na marekebisho machache tu. Na marekembisho yale ni kama wale wazee wa vijiji pia, wakawe wata e - watatajwa katika katiba hiyo mpya ambayo kwanza tunayo iuunda ili wakaweze kusaidia katika hiyo kazi wanayoifanya. Ni kazi nzuri sana. Mimi ndivyo ninavyoona. Kwa hivyo hawa wazee wa kijiji wasiachwe nyuma, waweze kuendelea. Pia vile vile ninge – ungana mkono wale wenzangu waliyotaja upande wa akina mama – wawe – ile katiba iwe itawasaidia sana. Wale kina mama, ingechunguzwa vizuri na kuona kwamba matatizo ambayo kwamba yanaendelea kwa sasa, hata ikiwa mabaya zaidi sana kwa hivyo tunge --- ingekuwa vizuri wawe wataangaliwa katika masilahi yao pia. Kwa hayo, asante ni sana.

**Com. Abdirizak Ali Nunow -** Asante sana mzee Kahindi. Na sasa namwita William Chengo?

**William Chengo**: Asante sana (Giriama Dialect) Asante sana, kupata nafasi hii, kuja kuhudhulia pamoja na nyinyi hapa. Mimi nina furaha kwa sababu kati ya katiba mpya hii ni kitu mpya. Kwa hivyo wazee wanatatizika sana.

Tatizo la William Chengo: Mimi kwa jina ninaitwa Willian Chengo Kalama. Wazee tunatatizika kwa sababu ya ugonjwa huu ambao uko sasa. Kwa sababu hiyo kitu inatatiza wazee kabisa. Na ningeomba katiba mpya hiyo, ichunguze kabisa hapo ndani kwa sababu, mzee tuseme ana mtoto yake anafanya kazi nje, atakuja, akija, amepatwana na ile ugonjwa unaona! Amepatwa na ile ugonjwa. Sasa hakuna, hakuna , njia yoyote ya kufanya kwa sababu yeye alikuwa nje. Hivyo sasa tumengo– naomba hiyo serikali iingilie hiyo kabisa. Ingelifaa kama daktari watakuwako ku – nyumba kwa nyumba kuangalia hawa watu – wagonjwa waweze kuwekwa hospitali moja ili wasizidi kuambasa. Hii hii laini mpya itakuwa sisi tunatatizika. Sisi tunatatizika. Naomba hii katiba mpya, ichunguze kabisa hapo. Inakuta mtoto, ameondoka, kuja akifikaa nyumbani hapo amekonda konda hivi, hivi, hivi sasa hata hakuna – hiyo ninaomba kama serikali itachunguza hiyo. Hiyo katiba mpya ichunguze kabisa hapo. Eh – mimi sina mengi. Yangu ni hayo. Asanteni(Clapping).

**Com: Abida Aroni**: Bwana Katana Ngowa Zero?

**Katana Ngowa Zero**: Hamjambo! Mimi maoni yangu niandika. Kwa hivo sina hapa ya kuzungumza. Nimeandika hapo kwa karatasi. Kwa hivyo nitapeana.

**Com. Abida Aroni:-** Asante. Benson Baya Mwanyoke au Mwanyole? Benson Baya Mwanyale.

**Benson Baya Mwanyale:** Kwa Majina naitwa Benson Baya Mwanyale eh , kuhusu mambo ya katiba yetu hii, naomba:

Yakwanza mambo ya barabara. Sisi tayari hapa ukitoka – Kilifi kuja huku, huwa tunapata shida sana hasa watati wa mvua. Nafikiri hata wageni wetu ambao mumekuja hapa, mumeona barabara vile ilivo, na mambo ya madaraja Mvua ikinyesha, huwa tuna maafa mengi sana huku. Hiyo imepita hiyo.

Pili: Mambo ya mashamba. Sisi, mambo ya mashamba yetu huku toka tupate uhuru wetu, tunapata shida sana. Tunasikia mambo ya Title Deed, tunafanya kuisikia, hutuioni. Hata kwa mikono tukashika angalao mtu mmoja wa Ganze awe ana title deed ajitetee. Hatupati, tunasikia hiyo imepita.

Mambo ya shule: Shule zetu huwa tunajitegemea wenyewe sisi raia wa Ganze hapa. Watoto wetu wanapita vizuri, lakini hatupati angalao kujengwa university. Tunasikia ma university huko, huko juu juu. Lakini sehemu hii ya pwani hakuna hata chuo kimoja. Kama mimi naongea vingine, kila mtu atajuwa. Lakini mambo ya mashule yetu, watoto wetu wanasoma wanapita lakini hakuna mtu ambaye ana jiendeleza. Tunasikia mambo ya Nairobi wengine wetu hatujui Nairobi iko wapi.

4. Mambo ya wanawake: Wanawake huwa tunawadhulumu. Mimi tayari nitaoa, bibi nikae naye, nipate watoto, badala ya tumesikilizana vizuri tunao watoto wetu tukikosana, watoto nampokonya, anaenda kukaa kwao, bila kupata hata mtoto mmoja. Hiyo imepita.

5. Mambo ya Walemavu. Hao walemavu ni watu kama sisi ambao tunajiweza. Lakini tukiangalia mambo ya katiba yetu huwa wale watu, walemavu,huwa hawapati haki zao sawa na sisi. Vile ilivo. Huwa hawapati haki zao. Kama mtu hawezi kutembea vizuri, katiba kama inaweza kumpatia kama nikitu gani kinamsaidia, naye akajisikia yuko sawa kama anataka pahali kama Ganze pale, anapata msaada kidogo anaenda, halafu anarudi nyumbani kwake, huwa wako wengine kama viwete hawawezi wako hapa hapo, nyumbani kwao – Hiyo imepita.

Iko mambo mengine na kuhusu uridhi wakina baba zetu. Mimi ni mume ninahaki ya kupewa uridhi wa baba. Lakini kama nimezaliwa na mtoto wa kike, huwa yule mtoto hana haki ya kupata uridhi kutoka kwa baba. Hiyo mambo hiyo iachike kabisa. Kila mtu awe anahaki kutoka kwa baba yake pale mashinani kwake kila mtu awe na haki yake. Si ati amechukuliwa dadangu amepelekwa mji mwingine pengine ni maskini huko, hawana pahali ya kukaa, hatapata haki yake. Nafikiri hapo sina mengi zaidi Na sina la kuandika ni hayo. Asanteni (Clapping).

**Com. Abida Aroni**: Harrison Mangi

**Harrison Mangi:** Kwa majina naitwa Harrison Mangi kutoka Dungishe location. Eh – katika marekebisho ya katiba kwanza mvumo wa serikali.

Tungetaka kuunga mkono hawa wenzetu ambao wametaja majimbo. Majimbo haya tunahitaji kwa hamu sana yakaweze kutekelezwa katika hii serikali mpya ambayo tunayoiunda na katika majimbo haya, tunakuta kwamba kuna hili jimbo letu la pwani ambalo lina rasilmali ambazo kwa hakika tukiwa tutapewa uwezo wa kuzimiliki sawa sawa, rasilmali hizi zinaweza

kutengeneza mambo kama barabara. Tumesikia mambo ya barabara yakitajwa hapa na ni kwa sababu pesa zinazo patikana katika jimbo hili zinaenda katika serikali kuu. Na hii imekuwa ya kikazo kabisa cha maendeleo ya pwani. Tumekuwa tumelaliwa sana na wenzetu wa kutoka huko sehemu za bara. Hao wana mambo yao kama kahawa, majani chai, wananufaika kabisa. Lakini sasa kwa jimbo hili la pwani tumekuwa na matatizo kabisa.

Hasa kwa upande wa vijana wa namaliza mashule wanakosa makazi hiyo ni tatizo moja wapo imesababishwa na zile rasilmali ambazo tunazipata zinaenda kwa serikali kuu na serikali kuu ndiyo ambayo inagawanya sasa kwa majimbo. Hasa tunakuta unakuta kwamba jimbo la pwani halina uwezo, haina mamlaka ya kujitengeneza mambo yake yenyewe. Kwa hivyo tunataka mamlaka sasa kwa majimbo.

Tunakuja kwa bunge: Tunakuta kwamba bunge, ndilo ambalo lina e - linawasilisha mambo ya sheria, wanakaa wanaunda sheria hawa ndio wanawakilisha wananchi wa sehemu mbali mbali. Sasa unakuta hata mishahara yao tukiangalia tukimiliki sana, unakuta kwamba mishahara yao imepanda juu kabisa. Halafu tunaona kuna mfanya kazi wa serikali amelaliwa kabisa. Anapokea shilingi elfu mbili kwa mwezi, tena hapo ana nyumba, huyu anakaa Mombasa, anakaa Nairobi. Sasa unakuta hajiwezi kabisa. Kwa hivo tunakuta kwamba mishahara mikubwa inatengenzwa sehemu zile za bunge wanakaa, wabunge wanapazisha kwamba kila mmoja atakuwa akipokea kama shilingi mia tano elfu. Mbunge mmoja anachukuwa hizo pesa. Halafu kuna mfanya kazi wa serikali wakiwango ya chini kabisa anapokea elfu mbili, hasa hapo tunakuta hakuna usawa hapo. Kwa hivo mambo hayo pia yakaweze kauangaliwa.

Uwezo wa Rais Rais apewe uwezo wake kulingana na hali ya sheria, lakini sasa kuna mahali pengine ambapo napatilia shauku sana. Katika hali ya uwezo wake una – kuta kwamba kuna wengine husema kwamba, barabara hii itiwe lami mara moja. Halafu pengine hata ile wizara pengine haijafadhiliwa vilivyo. Halafu unakuta matatizo yanaingia ndani.

Kwa hivo aanze kwanza kuasiliana na wizara: Ajue kwamba Wizara ina pesa zakutekelesha jambo hilo. Ndiyo atamke hadharani sasa kwamba basi hiyo barabara itengenezwe mara moja. Kuna zile zinazoitwa directives. Hizi directives, hizi kuna zingine zinatia shauku katika zile wizara.

Kuna wizara nyingine huwa pesa hazitoshelezi zile directives zinazo toa – na zinazotolewa na rais. Hasa inakuwa vigumu kutekeleza yale ambaye rais amasema hasa unakuta wananchi wananungunika sasa Rais amesema iwe hivyo. Kwa nini haiwi? Pengine tatizo zimeingiya hivyo. Kwa hivo, hizi Hizi directives, hawezi kuzi- control yule rais atakayekuwako. Haweze kuzicontol – asitoe tu directive hive – awe ashaawasiliana na wahusika.

Tunakuja elimu ya msing. Kuanzia darasa la kwanza hadi la nane – mimi ningetoa maoni sehemu hii iwe free ama isiwe la kutozwa kitu kabisa. Halafu hapo awali kulikuwa Kenya School Equipment Scheme. Irudishwe mara moja. Mambo ya vitabu, mambo ya kalaamu, hayo ile idhara ambayo inahusiana na elimu iweze kupatiwa pesa za kutosha, ili kwamba mahitaji madogo madogo kama kalamu, vitabu, na mambo mengine, kama kuna hata rula tulikuwa tukipata wakati huo. Lakini sasa hakuna kwa hivyo tuangaliye sana hapo, hii Kenya School Equipment scheme irudishwe, halafu wazazi wawe wanajukumu ya kutoa eh – nguo za mtoto na kwangalia majengo ya shule. Lakini mambo haya madogo madogo ya sijui michezo, pesa za michezo hii iondolewe katika ile katiba mpya ambayo tuna – tunaiunda sasa.

Na kuhusiana na uhaba wa kazi, kama nilivyo tangulia kusema, uhaba wa kazi. Vijana wetu wanamaliza kabisa shule, zaupili halafu kupata kazi inakuwa vigumu. Sasa hii katiba mpya, tunataka hii katiba iangaliye sana tatizo hilo ambalo limekuwa tatizo la kitaifa, vijana wengi wanamaliza mashule halafu hawapati kazi. Wanaranda randa. Wengine wanakuwa tempted na wanakuwa waizi, wanaiba, kwa sababu kazi hakuna. Na tukiangalia hivi katika jimbo hili, tuna sehemu nyingi sana ambazo hawa vijana wanaweza kuajiliwa, lakini kwa vile hakuna taratibu maalum ni posa unakuta vijana wetu wanaranda randa hapa na pale. Kwa hivyo katiba yetu mpya nataka iangalie hata yule mwananchi wa kawaida, Mashinani kabisa kule, ili iweze kumsaidia na yeye.

Kuna hawa matajiri ambao wame jitajirisha kwa njia nyingine au njia hii ama nyingine. Ingekuwa vizuri hawa matajiri ma-tycoons waweze kueleza utajiri wao maana wengine wameiba pesa za mali. Wameiba, wamejipatia utajiri kupitia kwa wizi. Wametajirika wengine wamepeleka pesa zao ng'ambo na wanaishi hapa, Kwa hivo hawa, kuwe kuna uchunguzi ili wapatikane kwamba kuna mali nyingi ya uma ambayo imechukuliwa na mtu binafsi . Kwa hivyo tukiwa na kuelezwa, utajiri wa mtu kama huyo tutaupata kipengele kama hivi kwamba ameiba mali ya uma na hakufanywa chochote, hakupelekwa wapi. Hasa mali kama hiyo inaweza kusaidia sasa, katika hali ya kuendeleza nchi yetu, na kufikiriya kwa yule mwananchi wa kawaida.

Kuna upande wa kilimo. Tumetajiwa kwamba sehemu hii ya pwani kuna mnazi na mkorosho. Hili ni tegemeo kubwa sana la watu wa pwani. Tumetegemea sana mimea hii miwili. Lakini sasa shauku ni kwamba, haitiliwi mkazo katika serikali ama katiba iliyokuwako. Hakuna kabisa mkazo, katika mimea hii. Tunazosikia tu maredioni kwamba kuna mkahawa, majani chai, tunayasikia yanatiliwa mkazo wengine yanaenda nchi za nje. Watu wa kule wananufaika, lakini watu wa pwani, na mnazi wao, na mkorosho wao hawana kitu. Wana tu hivyo. Wakijaribu kujiendeleza, wanarudishwa nyuma. Laiti tungepata. Utafiti, juu ya mnazi, matunda yake yote, yanayopatikana, kama vile tembo ya mnazi, tunawezewa tu kutengenezeo tafiti ili kwamba ikapatikana kitu kingine cha tamani juu ya mnazi, na ikawa sasa ni utajiri wa watu wa, pwani. Maana pwani imepanda mnazi

kwa wingi zaidi ya sehemu zile nyingine. Kwa hivyo, watu wa pwani hatuna kitu cha kujivunia. Tuko hivi lakini hatuna kitu cha kujivunia. Maanake wenzetu wana majani chai, wanajivunia, sisi tuna mnazi . Ukionekana una mnazi unashikwa na polisi. Unaenda jela kama huna pesa z kutoa kitu kidogo unaenda ndani. Na ule mnazi ambao umeupanda. Kwa hivyo hapa tunaona kwamba katiba hautu tunzi vilivyo, kwa hivo tunataka katiba ya kutufunza na mali yetu. Tuweze kutajirika na matunda haya, nayo tunayapanda hapa pwani.

Usalama: Tunakuta kwamba katiba ambayo iko pengine mambo hayo huenda yakawa yako lakini sasa hayaitiliwi mkazo. Unakuta kwamba askari wanashika watu wetu, halafu pengine ameonekana saa tatu za usiku ama saa nne. Anaulizwa kitambulisho. Jinsi anavyo toa kitambulisho, wakati anavyotoa kitambulisho hivi, kabla haja toa, unakuta kwamba anapigwa kofi mpaka anaanguka. Je kuna sheria gani ambayo inasema hivo? Kwa hivo tuwe na katiba ya kutulinda wakati wowote. Kwanza askari awe mkarimu aulize mtu ambaye pengine amemwona kwa masaa yasiyo takikana kwa njia ya taratibu. ' Je kijana vipi? Unaenda wapi? Toa kitambulisho" yaani lugha ambayo itajaribu kumvuta yule awe hatakuwa na woga. Anakwelezea anakupatia kitambulisho, unajua kwamba huyu anatoa kitambulisho ni raia wa huku. Sasa unaenda wapi saa hii? Hasa anakuelezea halafu unampata unamzidikisha kusudi ili asipatwe na wakora. Hiyo ni njia moja ya kusaidia. Lakini sasa wewe unampiga. Halafu unamuweka pingu tayari na mwingisha kwenyenini – kwenye gari yako – unampeleka – am unamzungusha usiku. Yaani usiku mzima unamzungusha.

**Com. Abida Aroni:** Time tafadhali.

**Harrison Mangi:** Nataka kumaliza kitu kidogo.

Utekelezaji: Wakati huu tuna unda hizi sheria, lakini sasa isiwe tunaunda hapa halafu ziwe tu kama mambo ya kuangalia. – lakini hayatekelezwi. Tunataka sasa katika hii katiba hii iweze kutekelezwa vilivyo. Isiwe tu kwa jina. Lakini iwe itapewa kipao mbele, iwe itangaliwa vizuri, iwe itangaliwa kabisa, iwe huwa yakutekelezwa. Ni hayo machache tu.

**Com. Abida Aroni**: Asante. Kabuda Kenga? Baada ya

kumkaribisha mheshimiwa na dhaniya tungeendelea na shughuli

zetu. Ha - Kabunda Kenga?

**Kabunda Kenga:** Mimi naitwa Kabunda Kenga. Sina zaidi nimekuja kusikiliza katiba mpya. Mimi natoa shukrani kwa yale yote yamezungumzwa na wale waliyo tangulia. Sina mengi.

**Com. Abida Aroni:** Kibibi Toya

(Translator) Mimi naitwa kabibi Toya Mramba. Nimekuja hapa kutoa maoni yangu kwamba wanawake, watoto wa kike wasome wawe makarani. Si na mengi ni hayo tu.

**Com. Abida Aroni:** Mark Mangi?

**Mark Mangi**:- Habari zenu. Mini yangu nafikiri mengi nimeyaandika kwa hivo sioni aja yakuwa nisome halafu tena nitampatia hivo. Unaweza ukaweka.

**Com. Abdirizak Nunow:-** Do you want to highlight them?

You have 5 minutes to highlight eh?. You can highlight the key issues.

**Mark Mangi:-** Nafikiri nitaanza kuongea kuhusu uchaguwaji wa wanachini wa Rais. Ningeliona vizuri kwamba kama ingelikuwa Raisi anataja mtu jina la mtu, linapelekwa bunge, halafu bunge Wajadilia ikiwa watamkubali, sawa, wakimkataa, achague mtu wa pili. Akikataliwa mpaka mara tatu, atakuwa na makosa naye. Anaweza akatolewa.

Kitu ingine ni kwamba mambo yakupiga campaign kutumia pesa. Kama vile mtu anapiga campaign anagwawanya maleso, unga, hiyo ni kuonyesha wazi kuwa mtu hakufikirii maisha yako vile yatakavyokuwa kwa sababu yeye anataka kura yako apate kile kiti, na aendelee na mambo yake.

Ingine ni siku kuu ambazo ni za chama, kama madaraka, Kenyatta National, na Moi day. Kwa sababu ni kitu inayohusu chama si muhimu iwe ya nchi nzima. Itangazwe kuwa leo ni madaraka kila mtu asifanye kazi. Ibaki kwa watu wa KANU kama ni ya KANU. Na kama ni ya DP, iwe tu ya watu wa DP.

Kuhusu kazi ninaonelea kwamba kazi za serikali zikiwa ziko kama pwani, uhakikishe angalao asilimia sabini na tano wanayofanya kazi za serikali wawe ni watu wa pwani. Halafu asilimia ishirini na tano munaweza patia watu wa bara.

Ingine ni kwamba, sababu za kutoa kama in mbunge ama diwani tuseme kama vile mmechaguwa diwani, diwani amechaguliwa amekaa muda mrefu hana lolote alilofanya, haiti mkutano, kama yule tunaona ni afadhali atolelewe. Na njia ya kumtoa kama inawawezekana, watu watafute asilimia angalao thelathini ya wale waliopiga kura wandike majina yao, na watie sahihi halafu mwandike barua kwa Electoral Commission of Kenya, kwamba mtu huyu hatumtaki kwa sababu ya hii na hii. Halafu ichukuwe hatua. Pia njia hii unaweza wakayatumia hata kwa mtu wa bunge.

Kitu ingine nayaonelea kwamba mtu kama anataka kura, isikiye itafute njia, kama ni karatasi, mtu yote atakayo gombea kura ni

udiwani ni mbunge aandike mapendekezo yake akisema mimi nitamtengenezea barabara maandishi yale yaandikwe, yapelekwe kwa GK. Ikiwa amepewa kura na hizo vitu hakufanya anafwatwa kwa sababu atakuwa ame danganya watu. Ametumia njia mbaya kupata cheo na hakufanya chochote (clapping).

Na kitu ingine ni kuhusu mbunge kwenda bunge. Nafikiri mtu akienda bunge, ni mathumuni ya mbunge kufika bunge akafanye kazi yake. Yuko hapo kutoa motion ama ku-support motion. Sasa unakuta kuna watu wengi kwenye mbunge wako huko na hata hatuwajui wanafanya kazi gani, watu kama wale wanafaa watolewe. Afadhali tubaki na wabunge kidogo lakini ambayo wanafanya kazi yao bunge.

Kitu ingine ni kwamba kuchaguliwa kwa ma rais na kwa mawaziri na Permanent Secretaries. Tafadhali wawe professionals. Hatuna haja yakuwa tuwe na Permanent Secretary katika Ministry of Agriculture na mwenyewe anaweza kuwa ni Engineer. Hana kitu anachojua pale. Ili yako hapo, yuko na madereva watu wengi ambao wanamfanyia kazi, ni pesa ya serikali inaenda. Kitu ingine ukija kwa waziri unakuta ni hivyo hivyo. Hiyo pesa yote sioni ukiwa inatumika vizuri.

Na pengine ningehusia kuhusu biashara. Kuna biashara zingine ambazo ziko kusaidia watu katika pengine majimbo – jimbo lao yaani province yao. Sasa utakuta kwa sababu competition iko juu, unakuta kuna biashara ambayo inasaidia watu wengi kama vile ilivyo kuwa mkorosho ulivyo enda, sukari, ilivyoenda, kuna vitu kama maziwa pia watu huku wana-complain ni kwa sababu biashara zakutoka juu zimekuja zinachukuwa zimefanya competition yao, biashara yao yakuwasaidia hivi, imeuawa. Sasa kitu kama kile ingelikuwa katiba inasema kabisa ikiwa watu wa pwani wanategemea maziwa, na maziwa inayotoka kwa watu wanayotumika wa pwani ni asilimia hamsini, jawabu la wale watu wa bara kama wataleta imports zao huku, ziwe ni kuongezewa kile kiasi ambayo hawezi wakatoa. Lakini sio kuja waje wararie biashara za watu, wasiu watu hao hawana kitu cha kufanya. (clapping) Nafikiri ni hayo . Mengine sina!

**Com. Abida Aroni**: Agnes Kahindi? Yuko? Makori Chengi Karisa

**Makori Chengi Karisa**: - Mimi naomba machache na ndiyo haya. Muundo ama aina ya serikali tunayo penda, ama nayopenda mimi binafsi ni ile aina ya serikali iliyopewa mawazo na kiongozi wetu aliyokuwa anaona mbele marehemu Ronald Ngala; Federal Republic. Kwa sababu gani tunapenda hiyo? Ama ninapenda hiyo? Serikali ya umoja haijafaulu kutekeleza na kutenda na kutimiza yale ambayo yalikuwa inatusumbua kutoka enzi za wakoloni. Tulipopata uhuru, walituahidi yakwamba katika serikali hii, tutahakikisha ya kwamba katika serikali hii, tutahakikisha ya kwamba ujinga umeondoka yaani kusoma na kuandika, magonjwa yote, kutakuwa hakuna wasiwasi, pamoja na umaskini. Lakini kufikia sasa, kutoka mwaka 63 hadi wa leo, umaskini umeendelea kuwa wimbo katika kila mdomo wa mtu. Kwa hivo, ikiwa pengine kutakuwa na mabadiliko mengine kidogo ya serikali, tumeendelea kupika chakula kimoja, mahali pamoja mpishi mmoja lakini mji umekuwa mkubwa huu.Tugawanyane chungu (clapping).

Judiciary: Kwa kuwa yaonyesha yakwamba ndugu zetu wanakoti ya kazi; kama ya kidini, wakristu nao pia wawe na kitengo chao cha mahakama, ili nao watekeleze kazi za ku-fungamana na kidini – kama kuoza, kama kuridhisha, na mambo mengine yanayo fanana na hayo. Ikiwa itakuwa hivyo basi, tuwatie pia hawa ndugu zetu ambayo hawana dini customary courts.

Haya mambo ya Kigiriama ki – giriama miundo miundo ya wale ambao ni wagiriama wanajuwa kigiriama mambo vile inapo endelea. Hao nao wanajuwa kuridhisha, hao nao wanajua kufanya nini? Kuozesha. Kwa nini basi kusiwe na kitengo cha koti kidogo? (clapping) Basi ikiwa haitawezekana, kwa nin koti isiwe moja? Ikiwa vyote vitashinda basi na koti na iwe moja. Na yawe mamlaka ma moja.

Land and property rights:- Haki za ardhi na mali. Masikiano na mapatano yaliyo kuwepo kabla ya uhuru, miongoni mwa majamii kama vile wamazrui na kadhalika na ukanda wa pwani. Jambo la kwanza ninataka niseme ya kwamba jambo kama hili ndilo ambalo limeleta masquota – shida ya masquota. Hivyo katika kitengo hiki cha mazrui land, tunaomba yakwamba kiweze kuondolewa na ardhi iwe ni ya wakenya na ya watu wote, kwa sababu hiki ni kipawa ama zawadi tuliyo pewa na Mungu, Nafikiria tumepatana hapa. Sababu gani iwe hivyo? Imeleta masquota wengi, ardi hii ni kipawa ni zawadi kutoka kwa mungu. Kwa nini kiende na mtu? Kwa nini kiende na mtu mmoja ili hali tunajuwa ni zawadi tuliyopewa na mwenyezi mungu kuwa hapa, halafu mtu mwingine anasema ni kipande chake- Sufferers.

Kuna jambo jingine – hili la pension mafanyaji kazi wa serikali anahesabiwa miaka vizuri sana. Na kabla haja ritaya anapewa barua ya kwamba kufikia wakati huu ama tarehe fulani mwaka fulani, utakuwa sasa hatutaki tena huduma zako, umemalizana na serikali. Sasa baada ukiwachishwa kazi, mara nyingi shida ya matatizo, shinda ya mshahara haiji tena. Tungependa kuomba basi, pension office or officer ahakikishe kabisa, yakwamba, kama itakuwa hivyo, basi baada ya miezi mitatu ameritaya Januari huyu mtu, tunapenda pengine mwezi wa nne tarehe moja mshahara wake pesa yake nda! Ziwe zinaingia. (Clapping)

Haya jambo jingine ambalo ni la mwisho. Wapendwa tunarekebisha katiba. Hii katiba itakuwa nzuri. Ikiwa maoni yetu yatachukuliwa vile yalivyo. Tumeelewana? (Giriama dialect) Hii itakuwa nzuri. Hivi natake kusema hivi, ikiwa tutaikubali, tuwe na sisi tayari kijirekebisha – kama tunavyojirekebisha hiyo nini? Katiba. Mwizi asiibe tena, mfisadi asifisadi tena ili tufuate hii katiba ambayo itakuwa nzuri na tutafika, hakika tutaona matunda mema. Asante ni sana.

**Com. Abida Aroni**: Sara Kalu? Yuko? Basi kazana Kidogo.

**Sara Kalu**:- Hamjambo wananchi wenzangu? Maoni yangu, nina maoni matano.

La kwanza, katika katiba ijayo, natake tupate haki zetu za mashamba huku kwetu pwani. Kama vile ambavyo wengine wamesha zungumza. La pili, kukitangazwa uchaguzi wa kazi, kwa mfano kama vile ma-askari kuwe na mtu atokaye katika sehemu ya mkoa wetu. Nita fafanua kidogo hapa. Yaani utakuta mara nyingine kutasemekana kuwa kunatakikana polisi,

vijana wa polisi. Watachukuliwa huku, watatangaziwa ama kwa magazeti, ama kwa vyombo vya habari. Watoto wataenda. Wakifika kule, watakuja kuchukuliwa pengine mmoja tu katika hii constituency nzima na hali wameambiwa wote waende. Wanapata tu mtoto mmoja. Na pengine wengine wanafikisha zile qualifications ambao huwa wanatake lakini utakuta kuna ufisadi fulani ambao unaendelea hapo. Utakuta watoto hawachukuliwi. Na kama ingekuwa pengine imefanywa kwamba kutoke mtu wa pwani huko , maanake katika majeshi ya serikali yetu, naona wako wengi sana na watu ambao ni wa sehemu hii. Kama kungekuwako kuna wezekana, katika serikali hiyo, kukichaguliwa ma-askari kupatikane mtu ambaye atakuwa anatoka sehemu hii aje achaguwe watu wa sehemu ya huko. Pili hilo.

, Tatu tunataka kina mama wajawazito na watoto wa kuanzia mwaka mmoja hadi miaka mitano, kusiwe na malipo. Maanake katika muda huo mtoto wa mwaka mmoja mpaka miaka mitano na magonjwa mengi sana na pia mama akiwa mja mzito an magonjwa mengi sana. Leo atatoka hospitali, akatoezwe pesa, hiyo dose hata haijamalizika, ameanza tena kuuguwa tena, hivyo hivyo. Sasa wengine hali zao ni -- si sawa na wengine. Hawana nafasi kubwa sana. Hasa atakuwa hiyo hospitali inamsumbua, mara anashindwa, mama anakufa, ama mtoto anakufa kwa hivo, naomba katika katiba ijayo kusiwe na malipo katika mama mja mzito tu, na watoto wale wa mwaka moja na miaka mitano. Lakini ikiwa ni – kama hivi mimi sina mimba sina mtoto, nikachajiwe na wagonjwa wengine, lakini wale wa mimba na yule mtoto wa mwaka mmoja mpaka mitano tafadhali tunaomba. Maoni yangu lakini.

Namba nne. Hivi vyu vikuu ziweze kujengwa kila mkoa, ili kupunguza hata garama ya usafiri. Huku kwetu kwa mfano kama huku pwani, tuwe na si tunaweza kupata chuo kikuu chetu huku. Watoto wamepita huku wawe wanaweza kwenda kama kwa mfano kutakuwa ni Mombasa, kuwe tunajua kwamba hapa pana chuo kikuu. Watoto wetu wakipita, huku maskuli huko kwao wawe wanaweza kusoma hapa. Badala ya kwamba pengine vyuo vikuu huko. Na pia hizi karo za huko. Angalao ziwe zinapunguzwa kidogo maanake saa ingine watoto wetu wanapata lakin wanashindwa. Eee - inakuwa sijui nyingi mpaka mtu anashindwa. Kwanza mtoto akirudi huku, elimu ana ya juu. Halafu huku hawezi fanya kazi yoyote. Basi tu anaranda randa hakuna kazi ambao inamulenga alipata kule lakini hakuweza kwenda. Kwa hivo viwe karibu katika mkoa halafu zipunguzwe kidogo hivi, gharama zake, ama karo zake.

Mwisho tano, narudia tena huko kulalama. Maanake katika karo hizi, za sekondari utanisamehe kwa sababy ya kudai kupunguzwa punguzwa , lakini hizi karo za ziku hizi, shule ya sekondari pia zi juu mno. Zipate kupunguzwa kidoto sisana. Hatuwezi kusema zitapunguzwa ngapi maanake hiyo siwezi kujua mpangiliyo lakini angalao kidogo ziwe zina nafuu.

Wamama wengine huwa wako peke yao yaani kwa mfano mtu mwingine alifanikiwa, ama ni mama tu ambaye yuko peke yake. Ana mtoto wake apenda asome. Amemsomesha lakini anafika sekondari mwisho. Pengine ana kalika masomo mtoto akiwa form 3 ameshindwa kabisa mama maana hana msaada wowote. Kama ingekuwa kuna pengine kidogo zikawe ile fees zinaopunguzwa kidogo, mama angependa ku-angweza na yeye mtoto wake akasome. Kwa hayo machache asanteni. (clapping).

**Com. Abida Aroni:** Asante mama. William Kadenge Ngumbao? Yuko? William Ngumbao?

**Wilson Ngumbao**:- Mimi kwa majina naitwa Wilson Ngumbao ninatoka sehemu ya Sangalaweni, katika Ganze location. Ganze Division.

Mimi nilikuwa nimepanga kuongea machache kuhusu mambo hii ya pension na gratuity, yaani kwa watu wafanya kazi wa serikali. Wale ambao wanastaafu. Lakini nafikiria kwamba sitaendelea zaidi kwa sababu, kuna wenzangu wemetangulia hapa, kuongea jambo hilo, na ninaonelea kwamba nikiendelea zaidi, na wenzangu mambo hayo wameyazungumza tayari, ni kama kwamba nitakuwa nina chukua wakati wa mwingine ambaye angekuja hapa. Lakini tu kwa kuunga mkono wale wenzangu ambao wametangulia kuongea jambo hilo, pia mimi ningezidi tu kuunga mkono kwamba ikiwa kunawezekana kwa hii katiba ambayo tunataka ifanywe, yaani katiba mpya, ningeunga mkono wale wenzangu ambao wemetangulia kuongea kwamba wenye kustaafu, wafanyi kazi wa serikali ambao huwa wanastaafu, hawa watu, huwa wanaenda kila mwaka, kila baada ya mwaka, kuna watu wanastaafu. Maombi ni kwamba, serikali ifikirie jambo hili kwamba, ile wenzangu wametangulia kuongea malipo haya, yajaribu kuletwa kwa kila mkoa. Kila mkoa uwe unapata pesa hizi kulipa watu wale ambao wamestaafu na kulipa pension yao ya kila mwezi, kupitia kwa district zao kama vile hiyo mambo inaendelea. Lakini malipo ya miaka ile ya mfanyi kazi amefanya ile miaka na amestaafu, pesa zile ziwe zikilipwa kupitia kwa Province ya yule mtu, yule ametoka. Kwa hayo machache, nani kwa vile wenzangu walikuwa wametangulia kuongea jambo hili singependa kuchukuwa muuda mrefu. Kwani ni kama nitakuwa ninarudia hiyo maneno, na tayari yamezungumzwa. Sasa, kwa hayo, Asanteni.

**Com. Abida Aroni:-** Asante. Joseph Toya Mbaya.

Joseph T Mbaya:- Asante mwenye kiti na wenzangu wote wako hapo. Kwa jina ni Joseph Teya Mbaya. Mimi kitu ambacho nimejisikia nizungumze na ni maoni yangu. Maoni yangu mimi, si ungi mkono kwamba ati Standard 8 haiwezi kuendesha kitu chochote. Hicho siungi mkono kabisa. Kwa sababu Standard 8 yaani haswa hiki kiti cha udiwani. Kiti cha udiwani ikiwa itawapasa, Form 4 awe ndiye anaweza kuchukuwa kiti hicho, hapo ndiyo makosa kabisa kwa sababu hii ni kazi ambayo ni ya ku-elewana na raia. Kwa hivyo, hii ni kazi ambayo mtu anachaguliwa akiwa na tabia ya kutosheleza. Si lazima awe form IV kwa hivyo, mimi siungi mkono kabisa na la pili, hapa tumenyakuwa uhuru kutoka mwaka wa 63. Sasa maoni yaungu ya katiba hii mpya ambayo iwe sasa nikwamba wakati huo wote pale ilikuwa ikitwangalia University hakuna, chuo cha utalii college, kiko Nairobi na bahari iko hapa Pwani. Hilo ni jambo la kusikiiiza. Watoto wetu, wakimaliza mashule, wengine hawana nafasi ya kuendelesha watoto wao. Unapata watoto wanaranda randa huku wakirudi huko. Kenya Utalii college ingewapi angalau wachukuliwe hawa Std. 8. hakuna. Eh ! Hii ni jambo ambalo kama katiba hiyo mpya ingeunga mkono haya maneno, ingekuwa mzuri zaidi.

Pili, watu wanaumia sana, kuwa mambo hayako sawa sawa hapa Kenya. Unapata mtu mmoja anachukuwa mia – elfu

thelathini – 300,000/= mshahara wa mtu mmoja. Je Wale walio chini wafanye nin jameni? Ukikala huu. (Giriam dialect)

**Com. Abdirizak A Nunow**: Utaongea kiswahili au ki Giriama?

**Joseph T Mbaya:** - eh eh Kiswahili: Ikiwa serikali hii na tunaomba kitu kizuri ndicho ambacho ni kizuri cha kuchukuliwa mfano ili kwamba hata ukifika hapo, kwetu kiwe ni kizuri. Mnaruka na ndege kwenda mbali sana. Na mufikapo huko watoto wetu wale tumewachaguwa, munaona mambo tofauti tofauti. Kwanza manatwambia Amerika kama mtu hafanyi kazi, anapata tu mshahara. Si mchukuwe huo mfano mtuletee na sisi (Clapping) kwa nini sisi hatuwezi kupata huo mfano? Eh ! Nasisi tunataka. Sio kuomba ni lengo letu tusipofanya kazi. Na pili mafunzo ya kilimo Yafunzwe sawasawa hapa, inchini pwani. Yafunzwe ili kila mtu kwamba aelewe.

Tatu, hata sijui ni ngapi, sifurahii mimi ikiwa munazi ukaenda ukipuziwa na matunda yake yako. Ikiwa munazi hamtaki na ile nazi ina maji yake, kwa nini huu utafiti hauchukui yale maji ya nazi basi? Sisi tunakaa kwa barabarani ili maji yaleya nazi ikawa inachukuliwa vile maziwa inachukuliwa? Eh! Kama sio pombe, maziwa – maji ya nazi yachukuliwe! Ukafanye utafiti. Maji yake nazi yachukuliwe! Ukafanywe utafiti!

Nimesikia ya kwamba – hiyo ni maoni ambayo nimeyapewa tu. Iko tofauti tofauti na wenzangu – hawa akina mama wakikosa kuelewa vizuri kule kusema watoto wagawanywe wakitoka hapa watasema " hata Katana Ngala alikuwako akasema watoto wagawanywe bila sababu ya kueleweka. Kweli, urongo! Eh. Nikisema hivyo si kwamba ati sitaki mpate uridhi au nini. Kwa uridhi ni sawa nishayaunga mkono. Lakini kama kugawanya watoto kwa sababu ambayo ni kinaga naga, sio – kwa sababu nimeambiwa watoto tugawanye – ah – no way. (clapping) Asanteni sana.

**Com: Abida Aroni:** - asante. Chengo Kamtu? Chego Kamutu?

Chengo Kamutu: - Basi mwenye kiti, wakenya Wenzangu, hamjambo? Basi siku hii ya leo ni siku ambao na chukuwa nafasi kushukuru kwa sababu ni siku ya kurekebisha katiba. Tunajuwa ya kwamba katiba ambayo hutengenezwa na mwanadamu ni lazima kuwa kuna marekebisho. Majina ni chengo Kamtu. Na kinacho tengeneza wa Mungu hakina marekebisho. Kwa hivo tumekuja hapa kutengeneza katiba ama kurekebisha katiba kwa maana ilitengenezwa na mwanadamu na ni lazima iwe iko na makosa. Kwa hivo wakati huu, mambo ambao ningependa kuchangiya ama kuongea ili kwamba yangeweza kurekebishwa ni chache sio mengi kwa sababu ya wakati. Kwanza ningesema yakwamba kuhusu Rais. Sitaki Rais ambaye ni vuguvugu aniongoze. Nataka Rais ambaye amepewa mamlaka yote, amepewa nguvu zote. Sitaki Rais ambaye kesho amepelekwa mahakamani.. Kesho kutwa amepelekwa mahakamani basi. Mimi mwananchi wa Kenya hii. Rais huyu ataweza kunihudumia lini? Kwa hivo nataka Rais ambaye atapewa na atakuwa na mamlaka yote.

Jambo la pili ni kwamba kumekuwa na huu mvumo wa kitaifa – ama maongozi ya umoja, kwa hivo wakati huu ningeomba ya

kwamba tuweze kuwa eh na federal government ama serikali ya majimbo kwa sababu ukijaribu chakula utie nazi usikie kwamba haikwenda sawa sawa si utajaribu mafuta mengine? Kwa hivo kwa sababu huu umoja tumeujaribu kutoka mwaka huu wa tisini kwenda mpaka sasa, tumeona kwamba hakuna utamu. Afadhali sasa tuwe na majimbo, hata mzee wetu Ngala alisema, let us have majimbo – kwa hivo wakati huu ningeomba yakwamba majimbo, - eh – yaweze kuwa ndiyo yatakayo eh tuongoza.

Mambao ya waziri mkuu, mimi sina aja na waziri mkuu. Katika hii katiba ambayo eh tunaendelea kuwa nayo, maana tunataka jogoo moja awe ndiye anawika. Kama wakati huu tuko na Rais wetu, Rais Moi, akiwika pale juu, sisi zote tunasema yakwamba mzee anafanya nini? Amewika. Kwa hivyo ninataka y kwamba tuwe na huyo ambaye ni Rais moja lakini hii mambo ya waziri mkuu ambao watakuwa wachichanganya na Rais wetu, upande wangu naona ya kwamba si sawa sawa. Kwa hivyo ninaomba ya kwamba katiba hii katiba ambayo inakuja iwe na Rais lakini waziri mkuu asiwepo.

Katika elimu. Sehemu ya elimu: Tangu mwaka wa sitini ndio yakwamba ni kupigna na umaskini na hali ya kutojuwa kusoma na kuandika. Na wakati huu kuna hii elimu tunayoita ngumbaru. Hii ngumbaru naona yakwamba hili jina ndiyo inafanya hata wamama wengine na wazee wengine wetu wakose kuendelea nayo kwa sababu ngumbaru, hili jina wanaona kama wanatukanwa. Kwa hivo ningeonelea ya kwamba katika Katiba hii, tubadilishe hii jina gumbaru, iwe inaitwa elimu ya watu wazima. Elimu ya watu wazima.

Jambo lile lingine ni kuhusu kuabudu ibada. Katika Katiba ya kwanza, ambayo hata sasa tunaendelea nayo, Kila mmoja yuko huru kuabudu. It doesn’t matter whether you’re worshipping the devil. No matter you are worshiping tree. Hata kama anaabudu mtu ni sawa sawa maanake katiba nasema ya kwamba ni haki mtu kuabudu. Lakini nikiangalia katika Katiba ya Mungu, Mungu anasema, mimi ni mwenye wivu na sitakubali kwamba kuchanganywa na mwingine. Anasema niabuduni mimi peke yangu. Na sasa hii mambo ya devil worshipping ime ingia katika nchi hii kwa sababu hatukuwekewa kiwango fulani katika Katiba ya Kwanza. Kwa hivyo wakati huu ninaomba ya kwamba – e – kukipatikana mtu ambae anaabudu shetani eh devil worshipper – awe ana – a – kunayo hukumu ambayo atakayo ipata baada ya kupatikana, asiachiliwe hivi hivi, ili kwamba tuweze kupambana na hii maovu ambayo yamekabili nchi hii. Wakati mwingine tunasikia yakwamba Kyanguli watu wamechomeka. Tumesikia sehemu zingine moto unawaka, lakini tunapo ulizia sana tunaambiwa ‘ is because there are somewho are worshipping the devil’ katika sehemu hizo sasa wakati huu katika Katiba hii, ningeomba ya kwamba, mtu akipatikana ana abudu shetani – devil worshipping achukuliwe hatua katika hii Katiba, ambayo tunayoiunda kwanzia siku hii ya leo.

Jambo lile lingine ninaorudia ni upande huu wa alimu pia. Haiwezekani tuwe maskini na tajiri wote nawekwa a kwenye mlolongo moja. Sisi zote ni wakenya. Na kuna matajiri na kuna maskini, na maskini ni achukuliwe kwamba ya kwamba yeye ni maskini, na tajiri achukuliwe yeye ni tajiri. Kama ni mtoto, na kuna fees ambayo inatakikana, maskini ama mtu ambao hajiwezi, awekewe kiwango chake, na yule mtu ambaye anayojiweza awekewe kiwango chake maanake sisi zote hatuko

sawa hali ya kifedha. Hilo jambo iliwa halitawezekana, elimu iwe ni ya bure kwa mtu ambaye anayojiweza na asiyo jiweza. Zote tuwe kitu kimoja. Kwa hivo mimi ni Chengo wa Kamutu hayo ndiyo mambo ambayo nimekuja kuchangia, lakini katika kuandika msiandike Chengo wa Kamtu mwandike FrancisGathii Mwangi .

**Interjection- (Laughter and Clapping)**

**Com. Abida Aroni:** Ningependa kuwaomba, kwa hisani yenu mukijiandikisha jiandikisheni majina ambayo ni ya haki na halali kwa sababu, mambo haya inaenda katika record ya kitaifa. Bwana Kariuki na wenzako tafadhali hatuna ubagusi, ikiwa ni Kariuki, Otieno, mtu yeyote tutamsikiza kwa hivyo hakuna haja ya kubadilisha majina yenu. Fridah Karisa? Yuko?

**Fridah Karisa**:- Kwa majina naitwa Frida Karisa kutoka shule ya msingi ya Ganze. Niko na maoni matatu lakini nitazungumzia moja na ile mengine nitapeleka pale mbele. Jambo la kwanza ni elimu ya wasichana. Wazazi wengine husema ya kwamba usomesaji ya wasichana ni kama kupoteza pesa zao kwa sababu baada ya masomo, msichana ataolewa na ataenda kuhudumia jamii ile ya akina bwana. Mimi ningependa kukataa kabisa hapa kwa sababu msichana hata akiwa baada ya masomo ataolewa anastahili pia kusomeshwa kama ule mvulana. Maanake anaweza kuolewa akaenda kule halafu baada ya muuda atakosana na yule bwana na akiwa je kama hakusomeshwa, halafu akirudi pale kwao atafanya nini? Atajitegemea jena akiwa hana kazi? Hakusomeshwa hana kazi na yuko na watoto. Sasa ataweza kujitegemea kivipi? Yale mengine ambayo nimeyaandika hapa yatasomwa pale mbele. (clapping)

**Com: Abida Aroni**: Peleka pale. Nyevu Chengo?

**Nyevu Chengo**:- Asante sana (Giriama Dialect) Translator. Jina langu naitwa nyevu chengo. Natoka Petanguo. Maoni yangu ni kwamba watoto wasome shuleni kwa lazima. Kina mama waliyofiliwa na bwana zao wasiridhiwe. Sina mengi na memorandum ambayo nitaitoa.

**Com. Abida Aroni**: - Asante mama kwa maoni yako. Jamwa Kitao? Jumwa Kitao.

**Jumwa Kitau**:- (Giriama Dialect) – Translator – Jina langu naitwa Jumwa Kitau. Maoni yangu ni kwamba watoto wa shule waendelee kusoma. Mimi mwenyewe si kusoma lakini nasikia uchungu sana. Watoto wasome na wapite mtitihani yao.
Maoni yangu ni kwamba wakati mwingine, mzazi wa kiume akiondoka duniani ama akifariki, uridhi wake ama mali yake inachukuliwa na mtoto mvulana. Mimi nimeishi sana kwa babanu. Hata nikanunua shamba. Naketi hapo. Baada ya baba kufariki yule mdogo wangu anataka kuninyang'anya shamba lile. Mimi nilimwoza yule bibi mdogo wangu. Saa hii anataka kunipiga maanake ataninyang'anye lile shamba langu. Mtoto wangu je atapata nini? Yote ni mpatie huyo. Yangu ni hayo tu. (Clapping).

(Interjection: Ululations and clapping.

**Com. Abida Aroni**: Mohamed Shariff?

**Mohammed Shariff Omar:** - Kwa jina naitwa Mohammed Shariff Omar. Mimi ni mkaazi wa bahari mzaliwa wa Takaungu. Katika maoni yangu, nilikuwa nataka kuchangisha kuhusu uharibivu wa taifa. Tabia za watoto wa kiume na wa kike. Miaka ya sasa tuliyo nayo nafikiri tunasumbuliwa sana na ugonjwa iliyo ingia wa ukimwi. Ugonjwa huu, unaendelea kuenezwa kwa sababu ya tabia mbovu. Kwa hivyo mimi napenda Katiba izuie washerati - prostitution – iweze kuchukuliwa hatua.

Pili: Mavazi ya kike hasa katika miji mikubwa. Miji kama vile Nairobi, Mombasa vijiji kama Mtwapa, utakuta mwanamke anavaa skati ambayo iko juu ya magoti, anatembea uchi. Kwa hivo wanawake kama hao, wasiruhusiwe, waweze kuchukuliwa hatua , kwa sababu wanachangia katika usinifu.

**Interjection: Clapping.**

Pili, nataka kuchangia kuhusu tofauti za kikabila. Nafikiri, tukiangalia nchi jirani kama Tanzania kiongozi wao wa kwanza Mwalimu Julius Nyerere, aliweza kufaulu katika siasa ya ujamaa. Mtanzania yoyote ule anamwita mwenzake ndugu na kuna makabila mengi kama vile hapa Kenya. Kwa hivo nilikuwa napenda katiba iweze kutilia maanani kuweza kuleta umoja wa mkenya – iwe tukizungumza kitu tunazungumza kama mkenya sio kikabila. Halafu iwe tukakuwa tukichukuliwa hatua ya mtu ambaye aweza kumuhujumu mwenzake, kumtukana kikabila.

Iwe tukizungumza kitu tunazungumza kama Mkenya sio kikabila. Halafu iwe kutachukuliwa hatuwa ya mtu ambaye anaweza kumhukumu mwenzake ? ? ? aweze kuchukuliwa hatua, kwa sababu analete tofauti.

Ni kija habari ya maswali ya majimbo, sisi tu watoto wadogo sana lakini katika historia tuliosikia wakati wa uhuru kiongozi wetu walikwenda Lancaster House na ikapitishwa utawala wa majimbo. Wakati huo, Mzee Ronald Ngala ndio alikuwa katika chama chake cha KADU alipewa utawala wa majimbo na Mzee Kenyatta. Akaitikia utawala majimbo kwa shingo upande. Sasa mimi kwa maoni yangu kulingana na utawala ulioletwa na makubaliano baina ya Mzee Kenyatta na Mzee Ronald Ngala, tumeona hatari ambazo sisi watu wa pwani tumezipata. Sisi watu wa pwani, tumezipata. Watu wa pwani tumepaguliwa, kikazi, kimasomo. Utakuta nafasi nyingi za kikazi zime chukuliwa na watu wa bara. Ukiuliza ni kwanini unambiwa kuwa pwani hawakusoma na ile hali wako waseme. Lakini nafasi tumenyimwa.

Pili, kuhusu nafasi pia za kusoma utakuta bara ndiyo kuna Universities nyingi sana. Kwetu hakuna Universities. Wanafunzi wetu wanamaliza sekondari, nafasi za university nyingi zinachukuliwa na watu wa kule wenyewe. Watu wa pwani unakuta ni kidogo sana huko. Na waliopesa ni wengi hapa pwani. Unakuta nafasi, hakuna. Miyome iko pale Mombasa Polytechnic ni kupendekezwa ifanywe Univeristy, lakini sababu wanasema pwani kuna joto nyingi kule. Hakufai University?

Interjection: (Clapping)

Hii yote ni upagusi. Utakuta pia kuna ubagusi watu wa hapa wanapaguliwa mpaka kwa michezo. Utakuta katika football Harambee Stars utakuta wanachaguliwa hakuna wa pwani ni wabara. Ni sababu wa pwani hawana nguvu. Watu wanapenda usherehe, ustarehe. Mimi nakumbuka upagusi katika michezo. Nilikuwa swimming mimi, nilifanywa swimming sportsman. Mombasa sisi ni watu ambao tumezaliwa baharini. Na unajua bahari iko na waneo, na ikiwa unawezakufanya mazoezi katika bahari na unaweza kwenda masafari marefu kimazoezi, kibahari, vipi utashindwa na maji yaliotulia katika Swimming Pool? Siku hizo tukafanyiwa mchujo, wale waogaji waakilishe nchi ya nje wakachaguliwa watu wa bara. Sisi watu wa pwani tukaachwa. Hiyo ni maonevu. Kwa hivyo mimi napenda majimbo iweko. Kila jimbo lipate nafasi, watu wao wapate nafasi za kushugulika na mambo, makazi na nafasi za kimichezo.

Pili, kuhusu lugha ya taifa, nashukuru sana sijui ule mwanzo diye unda kiswahili simjui ni nani. Lakini kiwahili kimeweza kutusaidia sana. Utakuta makabila tofauti wanakaa pamoja wanzungumza wanaelewana. Lakini watu wakikaa wakabila fulani wakikaa wakizungumza kikwao, unakuta hawaelewani kilugha. Hujui anaongea nini. Lakini Mungu alitujalia akatuletea lugha ya kiswahili ili kuunganisha watu wote wapate kuelewana. Kwa hivo naomba lugha ya taifa iendelee kuwa kiswahili.

Interjection: (Clapping)

Maonevu ya wanawake katika ndoa: Nimeona katika practice za watu wengine kuhusu sisi waislamu sheria ya mwanamke imewekwa wazi, na napenda iingishwe katika katiba. Sis tukioa mwanamke, tunatoa mali. Mali ile anafaa mwanamke. Mwanamke ananunua vyombo vyake vya nyumbani na kama anafanya biashara mimi kile chombo ambacho amejinunulia ni chake kwa ndoa, kimekuwa ni chake, na wakati nikikosana na yule mwanamke, mimi sidai kitu chochote pale; atachukuwa vilivyo vyake vyote hata kama ni kusafisha nyumba aniachiya watoto wangu basi.

Interjection: (Clapping)

**Kuhuzu mnasi**: Mnazi ni mmea ambao uko na faida nyingi sana. Kando na pombe, mnazi uko na faida. Kutoka madhifu kuja mpaka tunda lenyewe mpaka mti wenyewe, mapaka mizizi. Mizizi ni dawa. Mizizi ya mnazi ni moja katika kichanganyio cha dawa cha nguvu cha ume. Kwa hivo mnazi una faida sana (Clapping). Kwa hivo ningependa serikali iweze kutilia manani hii ya pwani na kuweza kutafuta njia vipi tutaimarisha ukulima wa mnazi na faida ya watu wa pwani waipate pitia hiyo mnazi. Hapa

kidogo ningependea kujijulisha mimi kama nilivyo mwambia ni mkaazi wa Jakaongu, kule waliko Mazrui. Tukija katika maswala ya ardhi, mazrui hawa ni watu waliokuja zamani sana na nafikiri 600 years ago. Mazrui hawa waliokuja, walikuwa ni soldiers. Walikuwa ni waume peke yao. Walipokuja hapa, baadaye wakaasi amri ya mfalme wao wakaamua wasirudi tena kule, kwa sababu wakirudi kule watauliwa wakakaa hapa, waka intermarry hapa na miji kenda pamoja na wanyasa wazee wa kimazrui wale waliokuja kwanza waliofariki pia watoto vizazi na vizazi miaka ikaenda. Kula hivo, isipatikane kuwa siasa ambao inaenezwa kuhusu akiambiwa mtu ati mazrui akiniona hawaoni mtu kama mimi ni mwarabu wanasema ati huyu ndiye mazrui. Mazrui ni mwafrica kama wengine. Nafikiri Mzee Ngala anatupea mfano mzuri kwa sababu alikuwa very close to my father Shariff Arwi. Nafikiria walikuwa wakifanya kazi pamoja miaka mingi. Infact Shariff Awri yeye ndiye alishababisha mazrui wapokonywe ardhi igawiwe watu. Hiyo ilikuja kwa sababu ya kujenga sekondari school Takaungu. Wakati alikuwa ni councillor babangu mimi anataka ardhi kujenga sekondari school. Mazrui akapata site moja ambayo iko katika ardhi ya mazrui. Mazrui wakakataa. Akawaambia, sasa nyinyi munakataa, mimi ninjenga sekondari school ambayo itakawa faidisha mpaka watoto wenu. Nyinyi hamtaki maendeleo. Na mimi nitakwenda mpaka huko juu kwa sababu muko na pande kubwa jinsi kutupwe hamtumii hili ardhi mumepata vile vile. Akaenda juu, huko, akasema ndiyo serikali ikaamua ichukuliwe ile ardhi kwa sababu ni crown land. Na crown land zote ningependelea katika katiba zichukuliwe na serikali, zigawanyiwe raia ambaye ni jamii za hapo. Ama mtu ambaye ameweza kukaa hapo zaidi ya miaka 15 apatiwe. (Clapping). Halafu nakumbuka wakati huo, minister alikuwako wa Lands alikuwa ni Minister Darius Mbela alikuja kutangaza kule ardhi zigawanyiwe, watu wapate vichochoro wagawanyiwe. Hata mazrui wenyewe, hawakunyimwa. Waliambiwa wachukuwe wakakataa.

Isipokuwa mbali ya hizo ardhi zinacho chukuliwa, lakini bado wako na mashamba vile vile. Kwa hivyo ardhi napenda katiba, ardhi zote ambazo ni za crown land, ziweze kuchukuliwa na serikali, na zipatiwe wenyeji wanao kaa pale. Nyingine serikali anaweza kufanya mambo yake kupitia hizo ardhi.

**Com. Abida Aroni:** **Time**

Ah nafikiri sina la zaidi kasi.

**Com. Abida Aroni**: Asante. Chengo Kenga? Yuko? Yuko wapi? Chengo Kenga?

**Chengo Kenga**: Mimi ni Chengo Kenga wa Mumba. Naishi Petanguo, (Giriama Dialect) Translator. Naunga mkono yale yote yaliyo semwa na wenzangu, na sina zaidi. Nataka yale yote yaliyosemwa yatengenezwe ili kila mtu afaidike. Basi.

**Com:** **Abeda Aroni**: Kifuso James? Duweka Gabriel? Dieka Gabriel? Esther Johana, Joseph Charo. This is the 37th tafadhali kazana kidogo.

**James Charo**: Mimi kwa majina naitwa Joseph Charo kutoka Petanguo. Maoni yangu kuhusu marekebisho ya katiba ni

haya. Upande wa sera za mitaa, kuhusu madiwani, nilikuwa naona wakichaguliwa kwa muda wa miaka miwili. Wawe wana elimu ya kidato kama cha Form 4 na pia kuna upande wa machifu, ma-DO na manaibu wao. Wawe wakipigiwa kura na wananchi pia, maanake kuna watu wengine ambao kama vile tumeunga mkono hii sehemu ya majimbo ni bora zaidi.

Kama vijana ambao wamemaliza masomo wako na ujuzi wangechaguliwa na wananchi wenyewe waongoze sehemu zao. Kuna machifu, maDO na manaibu wao, na ma subchifu hivi. Wachaguliwe na wananchi wenyewe. Kama vile kuna upunguvu wa nafasi za kazi hapa, kuna vijana ambao wamesoma, na kazi hizo wangezifanya wao wenyewe. Hasa wangechaguliwa na kutawala sehemu zao kwa vile wanajulikana tabia zao na mienendo yao pale mtaani.

Kwa upande wa miundo ya muundo wa utaratibu wa uchaguzi mapendekezo yangu ni kwamba, wakati ule wa uchaguzi, wale wanaopiga kura wafike siku hiyo halafu zile kura zihesabiwe pale pale kituoni tayari badala ya kupeleka maboxi mpaka kwa ile eneo watu wanajazana pale nakungojea wajue matokeo. Ingekuwa bora zaidi kama wange hesabu pale pale tayari kwa kituo halafu wakajuako wapo peleka wamehesabu kiasi gani. Badala ya kupeleka mnachukuwa boxi halafu kuna kuwa na ufisadi ule sijui kadi zinaibiwa sijui zina fanyiwa nini. Hiyo ingekuwa wazi kama hiyo kazi ingeweza kufanyiwa pale pale kituo tayari.

Kuhusu upande wa haki ya makundi, mimi ningependekeza kuwe kuna haya makundi ya kamati za maendeleo ya kijijini. Wapewe nafasi ya kupangiwa pesa za miradi yao ili waisimamie wenyewe kwa vile wanajua matatizo yao na wanajua kuitekeleza. Wangepangiwa nafasi hiyo ya pesa kwa serikali halafu wakafikiriwa. Na pia hawa wazee wa vijiji pia, wangepewa nafasi kuwa kama ni malipo kidogo hivi wapatiwe, maanake wanaacha kazi zao na kuzunguka. Wanatumwa na hawapati kitu. Wangelipwa kitu kidogo hivi ili wakawa na moyo wa kuleta maendeleo kwa sehemu yao. Yangu ni hayo hayo tu. Nashukuru.

**Com: Abeda Aroni**: Asante Amini Ngawa?

**Translator**: Amini Ngawa (Giriama dialect) Mimi naitwa Amini Ngawa na sina mengi, nataka chama cha kanu kiendelee kwa moyo mkujufu. Ni hayo tu.

**Com: Abeda Aroni**: Thomas Jeffa?

**Thomas Jeffa**: Basi kama ninavyo chukuwa nafasi hii, ningependa kusema yafuatayo kama mchango yangu kwa katiba inayo kuja. Majina yangu ni Thomas Joseph Jeffa. Kipengele changu cha kwanza ama mchango wangu wa kwanza ningetaka kusema kwamba upande wa vyama vya kisiasa, kuwe na idadi ya vyama vya kisiasa kulingana na uwezo wa nchi. Ninasema hivi kwa sababu utakuta ya kwamba kwa kuwa wakenya sasa wamekuwa ni watu wenye njaa kila mtu anataka awe kiongozi, kila mmoja naunda chama chake, hata kingine nafikiria itaitwa Thomas jeffa hivi karibuni. Kwa kuwa kila mtu awe atakuwa kingozi. Na hata ni Kenya, ama nchi yetu ya kenya, ni vile ndogo ambao tunalijuwa zoteni ni hatia vyongozi wetu wanajua

hivyo. Hii ruhusa ya kupatia kila mtu mwenye kujisikia kwamba anaweza kuongea mbele ya watu na kuunda chama, hali hii pia imeleta ukorofi katika uongozi wa serikali yetu.

Kipengele changu cha pili, ningezungumzia juu ya wabunge na malupu lupu yao. Malupu lupu haya ya wabunge ni kwamba, mtu yeyote ambaye anayo fanya kazi ni lazima apate kitu kidogo kama kiinua mgongo ili kazi ile akaifanya katika hali iliyo – sawa na hata kawakilishe wale watu ambao waliyo mchaguwa katika uathifu huo. Hivyo basi, ni hali ya kuwapatia mshahara tena hali hii ifanywe kulingana na ni kitu gani serikali inapata katika kuokota okota zile pesa serikali iko jumla. Isiwe ni ile hali ya kuwa kwa vile wewe uko pale ile jumbe ambalo ni nzuri pale, anavumikisha pesa nyingi kwa kuwa yeye pale anawakilisha watu. Jambo hili unaumiza watu wanafanya kazi katika tabaka mbali mbali.

Hoja yangu nyingine ya kuchangiya hali hiyo ya katiba mpya Ninge zungumizia juu ya mahakama na mamlaka yake. Imejulikana wazi kwamba katika mahakama, wengi wamefanya makosa, vyongozi wa sasa wamepoteza pesa nyingi kwa serikali na wanao laumiwa ni mkenya ambaye ni mwananchi ambaye hajui hizi pesa ambazo sa????? Zilitoka wapi na zilikuwa ngapi? Tunaambiwa tu yakwamba pesa zilikuweko na eti hakuna pesa. Kwa hivyo hali hiyo ya mahakama kama mtu amejulikana kwamba hiyo alihusikana na hiyo mahakama ikajaribu kuwa kidogo kufuata ile sheria – neno – baada ya neno, ili yule mtu ambaye amefanya vile akapata kutupiwa kilicho sawa na kosa lake. Hali hii ya kusema huyu ndiyo ukoo wangu, huyu ni mchumba, huyu ni dada yangu amefanya makosa mume wacha namna hiyo, ndiyo imefanya mpaka sasa migomo ya wafanyi kazi imekuwa mingi sana. Kwa hivyo mahakama katika katiba mpya ikapatiwe uhuru ya kufanya kazi yake bila kusumbuliwa na wale viongozi ambao wenzangu wamekuja kusema kwamba hawa wakisonga mbele wanaambiwa ati wawe na mamlaka makubwa zaidi kushinda mwanchi yeyote. Kwani Siyeye – mimi – navuta hewa huku chini yeye navuta carbon dioxide? Sisi zote ni wakenya. Kwa hivyo kama ni sheria kusimamia mwanakenya, isimamie kila mwanakenya.

Mchango wangu wa nne ambao huo watatu ulikuwa ni wa mahakama, wa nne ni kuhusu haki za ki-msingi. Katika mahakama hizo hizo, kuna hii hukumu ya kusema kwamba mtu fulani amehukumiwa kifo. Kwa kuwa kosa alilofanya,halingetaka kurudiwa tena na mtu huyu ni apotezwe. Nataka niulize swali ama pengine ni jaribu kuongea kulingana na hali hiyo. Huu mtu ndiyo yule alichaguwa mbunge jana, juzi, akambpatia madaraka yale. Leo amefanya kosa hapa, amehukumiwa, anakufa. Je huyu mbunge akitaka kura kesho atapigiwa na nani? Wazi kwamba hata?????? Yangu waangalie hapa. Kuna kirefu, kifupi, kizito, hali namna hiyo, lakini jee katika hali ya ujiwa, kama kiko, tumezungumza tume elewana, lakini wewe unasifa ambayo kunipatia kwa nini na zungumza hivi? Ni swali la walimu.

Walimu walikubaliwa na serikali wakazungumza, wakaelewana, yakakubaliwa yote na wazee ambao ni viongozi wetu, wakajua sasa, kuna huu muvutano. Nipe ulimahidi. Siwezi kupatia sasa, lakini nitakupatia muda fulani na haya mpaka muda fulani nitakupatia ulicho taka lakini hali hiyo haijakuwa. Ukiangalia hao ambao walisema wapatieni hawa walimu wako tayari tupatiwe lakini vyongozi fulani walichukuwa hizi pesa, wakazitumia kwa njia yao, ambayo wenyewe walikuwa wakijua hivi sasa walimu walikubaliwa tu wapate kitu kidogo. Hiyo pesa walizitumia, pesa hakuna. Tunalaumu viongozi wetu kama Rais Moi kwamba

naye anafuata mambo za watu ambao hawafai. Na kama hawafai kwa nini mahakama haichukuwi sheria yake? Kwa hivyo, nataka hapo kama itawezekana katiba mpya iangalie sehemu hiyo.

Kuna hali ya uongozi na watumishi wa mali asili na hata na misaada mbali mbali ambayo inakuja katika serikali hii. Swala hili la kuwa mali asili ilikuwa namna gani ni kwamba na hii hali ya shida ya nafasi za kazi. Tuna watoto ambao kama walivyo tajwa, wengine wamemaliza darasa la nane, wengine kidato cha nne, hawa watu hawana kazi. Kama serikali ingekuja na mpango fulani katika katiba mpya ya kueleza kwamba hii mali asili kuwe na watu hivi kama vijijini ambao watapelekwa katika course fulani fulani waweze kulindap kile kinachopatikana pale eneo lao ili zikaweze – ku – kama saa zingine serikali ili unaweza kuzitumia ama kuzichukuwa iwe katika hali ya mpango na wale wanao kaa katika ile eneo wapate manufaa ya kila kitu kinapatikana wapate manufaa ya kila kitu ambacho kinapatikana katika eneno hile.

Lakini kama vile ilivyo sasa kwamba nikijulikana kwamba hata leo kwangu kuna, mafuta, mimi kwamba nafuatwa na ma-askari natolewa na mahali inachukuliwa. Hali ni nzuri, lakini tutazidi kuumizana.

Katika hali hiyo ya uongozi tena kila moja wetu hapa ni kiongozi. Wewe ni kiongozi, mimi ni kiongozi, lakini je, katika uongozi wako unaongoza namna gani? Unajiangusha katika hali iliyo sawa. Yale yote nayo unayaongea mbele ya watu, ndiyo hayo unayozingatia mpaka unapata uongozi.

Katiba mpya, kama viongozi walio katika mamlaka sasa, hawa hawakuwa wanapata taratibu za uongozi na kufanya yale yalipo kwa wale wananchi wana wachagua. Ina haja gani tuwachaguwe hawa katika uongozi? Tunajuwa hali zetu za kiafrica. Tunajua kwamba hali zetu – kisomo ndiyo – kuna wengine wamesoma zaidi ya wale wengine bado. Lakini katika hali lile ukiwa wewe ni kiongozi uje hawa wana uongozi katika eneo lake, wana shida gani hasa? Mimi kama kiongozi, natakikana niitatuwe mwanzo, halafu niangaliye zingine. Kama utapatiana uongozi, na hutua iangalie hali zetu tutakuwa tunaongea mambo ya katiba kubadilisha kitu, moja ni tofauti na kile ambacho tunataka.

Mbali na kuangalia katiba, ile tunataka ibadilishwe hapa, hata viongozi wetu pia nao wabadilike. Kuna kule kubadilika kwa kuambiwa ubadilike na kubadikila kwa humo humo. Mimi mwenyewe na amua nibadilike kwa sababu hali ni mbaya sasa.

Haya, kuna hii swala la misaada kutoka nchi za ulaya na hali kadhalika kwa marafiki, matajiri vitu kama hivyo. Misaada hii ilikuwa ikija katika hali ya uzuri. Wakati chama cha KANU ilicho kuwa peke yake, misaada hiyo ilikuwa ikija, hivi Kenya ilipata vyama vingi, inaonelea vizuri, lakini maajabu ni kwamba kilicho fanya hii misaada isimamishwe na hawa wafadhili, ni kitu gani? Kwa nini alaumiwe mtoto wa darasa la nursery ama aliye nursery alaumiwe kwamba wewe uchumi ni mbaya, aambiwe uchumi mbaya yeye tulia na yeye hajui kilicho tendeka?

Uhusiano wetu wa kimataifa utakuwa mzuri tu tukikaa chini katika meza kama vile ndio tuongee kama wanadamu na tuelewane

je kipande fulani nikifanya mimi. Isiwe ile ume niambia nipatie mia moja, nikupatie mia moja, badala ya kununua unga akapelekee watoto, unachukuwa hiyo mia moja, unazunguka ule mti pale, unapata chupa mbili unaenda nyumbani umelewa, watu wanalala njaa. Nafikiria kama unashida hata ya kama mia moja, nitakupatia? Hali hiyo ndiye imefanya Kenya imekosa hii misaada mpaka sasa tuna ile hali ya kuvutana. Je ninani wa kulaumu? Ni yule ameongea katika microphone sasa ama ni nani? Utalaumu mimi, ama ujilaumu wewe? Je ni wewe ulinishika? Kwa hivyo katiba yetu mpya, utakuwa una anglia, ile katiba kifungo cha kwanza, cha pili hii ni hali tu! Yakurekebisha hali fulani lakini ilivyo ni kwamba hawa viongozi tunawachaguwa hawa, wawe na ule utu wa uongozi katika tabaka mbali mbali. Nimesema kila mmoja ni kiongozi kwa hivyo tupate hizi taratibu za kiongozi ili angalao pale ambao panaponeka, popote kunyoshwa ile hali iwe nzuri. Hata hivyo, wenzangu wamesahau kwamba ile serikali ambao tunayo sasa wakawa wanaitisha – a – serikali ya majimbo, ha – si mbaya maanake kuna unajuwa serikali ya majimbo iweko tutakaa pamoja na wewe, katika nyumba yangu tupange, halafu unapo kwenda kwa nyumba yako, utajua je katika nguzo hizo tumezungumza nini? Kwa hivyo hebu tuulize ile tuliyo yazungumza katika ule mkutano, nitajua ni lipi linalofaa katika nyumba yangu ili mambo yawe mazuri. Kwa hayo machache, nasema asanteni lakini viongoz tafadhali turekebishe hiyo sehemu. Asante.

**Com: Abeda Aroni**: Mwanje Daa? Yuko? Kazungu Mwaringa? Japhet Kahindi?

**Japhet Kahindi**: Habari zenu? Mimi naitwa Japhet Kahindi kutoka Dungisha. Mengi yasha zeungumzwa tayari, lakini kitu moja ambacho ninataka kuzungumza ni la pension kwa watumishi wa serikali. Ningetaka serikali ile itaundwa hivi karibuni, iangaliye kulingana na malipo ya pension ya watu wanao acha kazi serikalini. Mambo mengi yashaa zungumzwa tayari, kwa hivyo, ni hayo tu!

**Com: Abeda Aroni**: Asante. John Mwarua? Ismael Kaka Nzaro? Wote? Watatu? Christine Ngala,

Christine Ngala: Kina baba na kina mama, hamjambo? Kwa jina mimi naitwa Christine Ngala kutoka kauma, mkaaji wa Gariz.

Uongozi: yaani nataka rais awe mmoja. Raise awe mmoja lakini sitaki kuwe na ma-rais wengi.

Pili: Natka majimbo. Majimbo nayataka kwa sababu sisi watu wa pwani tume nyanyashwa sana, na watu wa bala. Watu wa bala wametunyanyasha kwa sababu, mambo ya elimu, mambo ya mashamba, hata mambo ya afya. Kwa sababu mtu anatoka, huko juu na tittled deed yake na hajui shamba iko wapi na nakuja kupokonya baba ama mama pwani. Na kule kwao, sisi hatukujui, hatukuendi. Kwa sababu yeye ameandikwa pwani anataka mali ya pwani iwe yake yeye. Kwa sababu yeye ni mkubwa. Ananyanyasha wananchi pwani. Kwa hivyo tunataka majimbo, na tukitaka majimbo, kila mmoja atakwenda akiwa mkoani kwao. Kila moja atajitekeleza mwenyewe.

Mambo ya elimu: Kusema kweli elimu katika huu mkoa wetu we pwani kwa jumla. Watoto wetu wasichana wengi wamekaa nyumbani hawaendi shule. Mtu anafundisha mvulana tu, lakini msichana anamwacha. Hajui kama akifundisha msichana amefundisha jamii nzima ya ndani ya nyumba yake. Mischana anaelimishwa nyumbani kwao hat kwa wensake. Msichana hata kama akiolewa amemfundisha, amepaka kazi, lakini hawezi kusahau nyumba ambayo amezaliwa. Hawezi kusahau ndugu zake, jamii yake ile iko ndani ya nyumba. Nasisifiza sana katika hii katiba wasichana wasome kwa lazima. Mtu ambaye yoyote hataki msichana aende shule, achukuliwe hatua yeyote, juu chini, ahakikishe kuwa anapeleka mtoto shule, msichana.

Mambo ya hospitali: Mambo ya afya sisi kina mama tunapata shida sana hasa mahospitali. Unabeba mtoto, unabeba miimba, tunaenda hospitali. Na ukifika pale hospitali, hakuna mtu wakukuhudumia haraka iwezekanavyo. Hakuna mtu ambaye anaweza kukuhudumia wewe, hata kama wewe mtoto ni mgonjwa sana unaweza kufa naye juu ya mikoni yako. Nakufika siku hizi, vile ambavyo mambo yako utakuta hizi hospitali za serikali hazina madawa. Wengi siku hizi wanakimbiliya private, na private siku hizi inacharge watu kali sana. Kwa sababu wanajuwa kwa Government haina dawa. Na katika private ile ukienda mambo mengine tu hawafanyi vizuri kule private. Lakini utakimbiliwa kwa sababu kule wanakuchukuwa kwa haraka. Kwa hivyo naomba mambo ya afya. Afya kwa jamii izingatiwe zaidi katika hii katiba yetu ambayo tuko nayo. Tunaishi kwa wakati huu.

Ukabila: Ukabila katika Kenya hii umezidi, kwa sababu hii. Tunafundisha kweli watoto. Ijapo kuwa ni sisi tunawekwa nyuma, hatujui kusoma, lakini twajua. Kwa vile sisi hatuna kiongozi ambaye ana uwezo wa kutuongoza katika huko juu, naweza kutusemea, tunaweza kukuta kama hata mtoto amesoma lakini hapati kazi. Ukienda huko una ambiwa ulipishwe 6,000 ndiyo mtoto wako aandikwe. Eh alipishwe shillingi 20,000/= wewe huna shillingi 20,000/= za kulipisha ule mtu mpaka aandikwe kule mtoto wako anarudi, na amesoma. Kwa hivyo utakuta hawa watu ambao wanakuja kuchukuwa hawa watu ambao wataend kazini ni watu ambao wataenda kazini ni watu wa bala. Kwa hivyo kwa wakati huu, katiba inataka kama ikiwezekana, hii katiba, mtu yoyote ambaye ataletwa sehemu za pwani aandikishwe kazi, huja wale ambao wanamshika. Kama ni mgiriama, aje huko giriamani, kama ni mjaluo, enda ujaluoni, kama ni mkamba aende kwenye wakamba (Clapping) kwa sababu ukabila umezidi.

Mali ya aridhi: Sisi kina mama tunaonewa sana mambo ya urithi. Mambo ya uridhi, bwanako wewe akifa kama uko na kadimali pale ndani ya nyumba utandanganywa wewe. Nataka kukuoa, nataka kukuoa. Akisha kuposa basi. Asha pata njia ya kuchukuwa ile mali. Atasahau pia watoto wako, hata kama ni watoto wa ndugu yake atawasahau kwa sababu yeye alikuwa anaomba tu apate ile mali. Kwa hivyo naomba wale kina mama ambao wako hapa, wakatae uridhi. Kuolewa ufa. Kuolewa ufa siku hizi hauna maana. Manake mtu atakuwa anakudanganya nakudanganya, akishaa pata hiyo mali, ni basi. Humuoni tena yuwaenda.

Mambo ya ardhi: Mambo ya ardhi: Wenzetu wamekula mavuno mengi sana ya ardhi zao ambao wako nazo. Lakini sisi huku

kwetu hatujapata title deed zetu za kuendesha mashamba zetu. Kwa hivyo utakuta watu wanagongana kabisa. Kila moja anataka haki yake. Lakini kwetu bado. Tunaomba ikiwezekana katiba hii ya sasa iangalie wananchi. Mambo ya ardhi na kuwapatia title deed zao kwa haraka. (Clapping).

Mambo ya kustaafu: Yamezungumzwa lakini mimi nazidi kuongeza kwa sababu ili jambo lilinipata mimi. Na siwezi kulisahau. Ikiwa hii katiba ya siku hizi inarekebisha hii katiba, nataka hii mambo ya kustaafu tuletewe karibu na sisi wenyewe. Kwa sababu wewe utachukua tikiti hapa ya kwenda Nairobi pengine utakopa, utafanya nini nende na ukifika kule, hutashughulikiwa na mtu yoyote kabisa. Ukizidi sand mtu anaenda kujiweka kwa choo. Sasa hii ni tabia gani. Hii ni tabia gani? Kwa hivo mimi naomba ikiwezekana hii mambo ya ardhi kama mambo ya kustaafu ikiwezekana, ili mtu akiwa na ritaya, afunganiwe mizigo yake. Kabisa kabisa asafirishwe aende kwao. Badala ya kuwekwa hapa na hapa. Kwa nini wanajua miaka lakini hawajui kutengenezea mtu vyake and kumuruhusu kwenda kwake. Kwa hivyo ningependa hii mambo ya kustaafu, wengi wanaanch mali zao za kustaafu, pengine ana watoto, nyumbani ana bibi, zile pesa zinabaki kule mpaka anafariki, hiyo register pia inapotea, sasa imekuwa maneno chungu nzima, kwa huko ndani. Kwa hivyo, ikiwezekana, serikali ichukuwe hatua hiyo katika hiyo katiba hii; mtu wa kustaafu, aende na mizigo yake. Afunganiwe kabisa. Akiwa anaenda, aendee kabisa na mizigo yake. Mimi nimeongezea hapo. Nafikiri wenzangu wame izungumza sana hiyo.

Mambo ya mnazi: Mnazi pia umezungumzwa hapa. Mnazi ni mmea mzuri sana huku pwan. Hata huko bala pia wanafurahia sio pwan peke yao. Lakini utakuta mnazi huku kwetu hauna maana kwa sababu haushugulikiwi na kitu chochote. Wenzetu kule wanavuna kahawa, wanavuna majani yanaenda ngambo yanafanya hivi watoto wao wanadiminka and zile pesa ambazo wakonazo. Lakini kuja pwani, utakuta mnazi umezoroteka konasho umezoroteka. Mtambo wa miwa pai ukanawa. Sasa mumetukata mikono na miguu sisi huku watu wa pwani. Nataka katiba ya safari hii, iweze kushughulika na mambo ya mnazi, makorosho na miwa. Nataka mtambo irudi. Mitambo nataka irudi (clapping) Mtambo wa miwa, mtambo wa mkorosho, hata tulikuwa tunatumaini na maziwapia maziwa siku hizi, maziwa yanaozwa. Tuko na ngombe lakini maziwa sasa yanoza. Tunategemea mapi sisi? Kwa hivyo tunaomba hayo machache ambayo nimezungumza, na palilizwe ananteni.

Com: Abeda Aroni: Clapping. Asante mama. Tutamwita bwana Daniel Baya wa kikundi cha 3 cs Trustee Committee.

Bwana Daniel Baya: Haya ni mapendekezp ya kikundu ya CC cha upande huu na bungeni sehemy ya ganze, na wanakamati ni kama wafyatai,

Mheshimiwa Noah Katana Ngala.
Councillor Susan Biria Mesha
Kahindi Karis Masha
James Gitau Philip
Ruth Muramba

Martha Salama

Joseph Chengo Mwaro

William Rora Muumba

Na Co-ordinator wetu Daniel Mwaringa. Wengine hawako maana wako vitengeni wakati huu, na kwanza mapendekezo yao kwenye haya marekebisho wanaanzia na mvumo wa serikali, wanataka serikali ya kiungo cha kati ambayo kutakuwa na rais, na rais atamchegua makamu wake, halafu pia wanapendekeza kuwa na waziri mkuu, na waziri mkuu huyu awe na wanachini wake au wasaidizi wake wawili ambao watachaguliwa na wananchi. Hii baraza la mawasiri ichaguliwe na rais kama ilivyoko sasa.

Kipengole cha pili walichosika wanasema haya mabaraza local authorities hizi zipewe nguvu zaidi, meya wa local authorities, haya mabaraza ya miji awe na kiwango cha elimu angawa cha form 4, hata kama macouncilor watakuwa darasa la nane, lakini yule anasimamia chairman wao, elimu yakeiwe inafika for 4 na wakati wao wa kukaa offisini uwe miaka 5.

Kipengele cha tatu ni viama via kisiasa. Wanapendekeza kuwa na vyama vingi kama ilivyoko sasa; kuna vyama vingine ambavyo malengo yake si mazuri, ni kama ya kikabila. Yani nia ya kurusha ghasia. Viama kama vile wansema viondolewe mbali kwenye hii katiba mpya visipate kabisa nafasi, kwa sababu vinaweza kuleta ghasia katika nchi.

Kipengele cha nne ni tume ya uchaguzi. Electrol Commission. Wanasema ile hali ilivyo sasa iendelee kuwa hivyo itumishwe, isipokuwa ile siku ya uchaguzi kama ni siku mbili, uchaguzi utachukuwa siku mbili au ni siku moja iwe declared public holiday ili hata wafanyi kazi waweze kupata nafasi ya kupiga kura zao. Halafu pia wakati wa uchaguzi, usalama uweko sana. Tena tight security kwa sababu tunaona kama uchaguzi nyingine watu wanapoteza maisha yao wakati wa uchaguzi.

Sehemu ya tano waliogusia ni kuhusu ardhi, wanasema ardhi yote iwe chini ya uongozi wa madarasa. Na title deeds, vile vyeti vya kumiliki ardhi, viwe vinatolewa na mabaraza hawa yanayohusika na wanapendekeza mtu kama amekaa mahali kwa muda wa miaka mitatu au zaidi ile ardhi apewe kitambulisho chake na haki ya kuimiliki kama yake, kama mumilkaji.

Sehemu ya sita, ni kuhusu elimu. Elimu ya msingi iwe ya lazima na ya bure. Kusiwe na fees ndogo ndogo, kusiwe na levies ndogo ndogo. Iwe ya lazima watoto wetu walazimishwe kwenda shule hasa za msingi. Kwa sababu tunataka kuendelea na hatuwezi kuongoza taifa halijui chochote.

Sehemu ya saba ni wajiri: Katika kila sehemu, katika kila mkoa wale wakuu wa idara mbali mbali za serikali na makampuni ya binafsi wawe ni watu kutoka eneo lile.

Halafu wanaongezea kusema haya mashirika ya serikali, idara za serikali, na makampuni ya binafsi iajili asilimia themanini na tano ya watu wakutoka sehemu ile.

Interjection: (Clapping).

Sehemu ya nane ni kuhusu ndini na mila. Kuna ndini nyingine ambazo zinahitilafiana na maisha ya watu kama vile utasikia ndini zingine zinasema Yesu Kristo anakuja mwaka ujao kwa hivyo watu wasiende shule, wasisome.

Sehemu ya tisa ni kuhusu afya. Mipango yote ya afya katika sehemu zote iwe chini ya mabaraza. Kama ni mabaraza ya miji, kama ni baraza ya sehemu ile iwe chini ya mabaraza na mabaraza yawe na jukumu la kuhakikisha angalao karibu baada ya kilomita tano, sita, kuna dispensary nzuri, kuna zaanapi nzuri, na maternity with a full maternity wings ambayo iko in operation for 24 hours kwa sababu wamama wetu wanakufa kabla wapate msaada wa hospitali. Kama vile tunaona, eneo letu ni kubwa na mtu kutoka pengine Dungisha, kitambo afike Kilifi, atakufa hapa barabarani. Wakina mama wengi wamepoteza maisha yao kwa njia kama hiyo. Kwa hivo, wanapendekeza kwenye katiba ijayo, kuwe na mikakati, maternity, angalao baada ya kilometre fulani, kuna hospitali pale, na maternity ya akina mama kujisaidia wakiwa na matatizo.

Sehemu ya kumi, sehemu hiyo kipengele cha pili ni kwamba, watu wote wanaofanya kazi katika hospitali za uma; wasiruhusiwe kuwa na kliniki zao. Wakati ule wanaendesha shuguli kule halafu huku wanaendesha shuguli zao, kwa sababu kumekuwa na hizi kesi za kuiba madawa katika hospitali kuu za uma, wafanyiye kazi katika kiliniki zao. Sisi tukifika kule, tuna ambiwa hakuna madawa, hakuna madawa. Na serikali inatoa madawa lakini wanachukuwa wanapeleka katika kiliniki zao. Watu kama wanataka kufanya kazi in private practice, they resign. Waache kule kazi, waje huku wafunguwe kiliniki zao.

Sehemu ya kumi ni kuhusu maji. Haya mabaraza ambayo yamepewa uwezo kulingana na haya mapendekezo yetu tunao yatoa hapa, yahakikishe kila mwananchi angalao baada ya kilometre 5 kuna mfereji wa maji, si maji ya mabenezi. Maji ya mabenez watu watatumia pengine kwa kuoga na kufuliya. Lakini wahakikishe maji masafi yanasambazwa kwa watu wote ili magonjwa kama typhoid tunaweza tukaiepuka. Ni haya tu, asanteni (Clapping).

**Com: Abeda Arono**: Asante Daniel, tutamwita mwenzake ambaye atakamilisha maono yao, Susan Biria?

**Susan Biria**: Asante Bi Mweney kiti. Mimi niko hapa kuwakilisha kina mama wa sehemu hii ya Ganze. Nitawataja majina baadhi yao. Mimi Susan Biria kama Mwenye Kiti, Grace Tinga, Secretary, Salakalu, Mary Kenga, Hadija Mohammed, Nyevu Chengo, Mary Mwarua, Kaka Kingi, Juma Kisao, Elena Kasike, Alice Siaa, Margaret Kalolo, Rama Charo, Peninah Joya, Rama Gona, Kabibi Katana, Bahati Charo, Kazo Kilonzo, Mary Kahindi, na Sarah Karisa.

Ya kwanza ni kunajisiwa kwa akina mama. Hii tulisema mama katika katiba hii mpya kuwe na sheria kali kwa wale ambao watawanajisi kina mama ama wasichana.

Uridhi: Wale kina mama ambao wameachwa na mabwana zao na walikaa na bwana zao kwa muuda pengine wa miaka 10

ama 20, kwa sababu kuna wengine hukaa muuda mrefu halafu mwishowe wakaachwa na kina bwana zao, wale ambao wamekaa muuda mrefu, na wametafuta mali pamoja, na wamezaa, wapewe asilimia hamsini ya malezi ile ambazo walitafuta na waume zao. Wale kina mama ambao wameachwa na waume zao. Kwa sababu kuna wengine, mtu amepata bibi mdogo, yule bibi wa mwanzo, amemfukuza.

Elimu ya msichana: Tulisema kwamba elimu ya msichana itiliwe mkazo na pia iwe ya lazima. Pia wakisha zaa, kwa sababu kuna bahati mbaya pia, pengine hudanganyika wakafanya miimba si kwamba ati ameanza mambo ya usherati, lakini saa ingine huwa ya kibahati mbaya. Akipata miimba, akishaa zaa, asikae nyumbani, lakini arudi shuleni.

Maternity leave: Kina mama tulisema wapewe angalao miaka minne ya kukaa nyumbani kwangalia watoto, badala ya ile miezi ambayo wako nayo sasa.

Kina mama wajawazito: Wale wapate huduma za afya bure, wale wenye mimba na ambao wananyonyesha.

Kifo: Pengine baba amekufa, mama ameachwa peke yake. Huyo, kuna ile eda. Eda huwa ianakaa miezi nne na siku kumi. Badala ya hiyo angalao kina mama ambao wako kwenye eda waongezewe hiyo leave yao kama miezi mitano pia walipwe. Wawe wakilipwa. Na wale ndungu zetu waislamu.

Kifungo: Kina mama wale wenye kunyonyesha na ambao pia ni wajawazito, na pengine wamefanya makosa wasifungwe lakini wa – wafungwe kifungo cha nje. Asifungwe jela.

Kuridhi kina mama: Hiyo tulikataa tukasema kuwe na kifungo ambacho kitakataza kina mama wasi chukuliwe ufa. Kuna watoto wa mama peke yake mbila baba. Wale mara nyingi huwa wanaitwa halali, haramu, tunaomba wale watoto witwe watoto wa halali. Kwa sababu kila mtoto ni mtoto. Hakuna haramu na wa halali – hata kama huyo mama hajaolewa.

Kuna baba wale wenye kutia watoto wa shule mimba. Hawa tulisema wachukuliwe hatua kali, hasa na pia na waangalie ule mtoto mpaka afikishe miaka kumi na minane.

Mali ya akina baba. Tulisema kina mama ama wasichana pia wawe na uwezo wa kuridhi mali ya baba zao, hata ikiwa wameolewa. Tuko na mfano hapa akina mama walikuwa wakisema, wao wamekaa kwa baba zao miaka mingi lakini wananyanganywa mali zao hata nyingine mali nunua wenyewe, sio mali ya baba zao, lakini wananyanganywa kwa sababu ni wanawake. Kwa hiyo hapa tulisema, kwamba kuwe na sheria ya kuwalinda akina mama nao wapate uridhi wa baba zao.

Kuna wale kina baba ambo hurudi tena wakaenda kuwanajisi watoto wao. Tulisema hao, wafungwe maisha. Wakifungwa maisha, ndiyo hawata waona hawa watoto wao, na hawata waona hawa bibi zao.

Interjection: (Clapping).

Kiti ya jamii: Kezi hizi ndogo ndogo za kwamba mke amekosana na mume, ama kezi hizi za kinyumbani ziwe na koti tofauti. Kuwe na koti ya jamii. Kwa sababu utakuta kwamba kina mama saa ingine wanapelekwa makotini huko na hawawezi kujieleza mbele ya watu – ama watu wengine ambao hua hawajui. Kwa hivo utaona kina mama mara nyingi huwa wanadhulumiwa. Utakuta pengine saa ingine wanaambiwa kwamba wamefanya vitendo viofu, pengine wamefanya usherati na mtu mwingine. Hii nayo saa zingine si kweli. Lakini akiona wale watu huwa anaogopa; anakubali kosa ambalo sihoi ameambiwa atolewe mali. Tukasema hiyo mali pia nayo kama itachukuliwa, ichukuliwe pande zote ituyo bibi apewe naye, ndiyo bwana akimpatia yule mwingine huyu mwingine naye apate. Kama sivyo, yaondolewe

Interjection: (Clapping)

Armed Froces & Police: Hii iwe na usawa. Kama wavulana wanachukuliwa kama ni majeshi, wasichana paia nao wachukuliwe sawa sawa na hawa wavulana. Kama ni polisi wanachukuliwa, wasichana na wavulana iwe nambari sawe sawa. Si wasichana 10 na wavulana 50. Iwe nambari ni ya sawa sawa. Kwa sababu wote wamesoma mashule moja, wote wamepita sawa sawa, kwa hivo kusiwe na ubaguzi wa kazi. Kazi zote ziwe ni sawa sawa. Hata wakipigiana simu.

Maternity ya waume: Maternity leave ya waume tulisema kwamba waume pia, bibi zao wakiwa wamezaa na wako leave, hawa waume pia wapewe leave ile wasaidie akina mama shuguli zile ambazo zinahitajika pale nyumbani. (clapping) Nyingine nitaziwacha basi naona mnafanya kelele. Nyingine ya mwisho nitaachiya hapo. Hiyo ya mwisho ni kwamba huku wamijikenda wana tabia ya kuoza watoto wadogo. Katoto kama haka kako hapa chini kanaozwa kwa mzee wa miaka 70. Hiyo kina mama wa sehemu hii ya Ganze tulisema hatutaki. Na atakaye fanya hivyo, achukuliwe hatua kali. Tena kali sana. Huyo mwenye kuoa na huyo mwenye kuoza. Kwa hayo, nasema asanteni.

**Com: Abeda Aroni**: Asante sana. Sasa nitamwita Kazungu Kenga. Ndiyo wewe? Una maoni?

**Kazungu Mramba**: Mimi maoni yangu si mengi. Jina yangu nitwa Kazungu Mramba. Kwetu kwenyewe ni hapa Ganze Mwaeba. Sasa maoni yangu jamii zote zilizo hapa na viongozi wote waliyo kuja wataisikia kati ya choir yangu ikifika. Nitatoa maoni, na muskie. Hata huko kwenye karatasi, nimeandika zaidi kwa hivo asanteni.

**Com: Abeda Aroni:** Ile timu ya mzee ijitayarishe. Wana nyimbo za maoni yao. Ziko katika nyimbo. Kwa hivyo wajitayarishe baadaye tutawaita, hiyo team ya mzee.

**Com: Abeda Aroni**: Robert Mae?

**Robertt Mae**: Jina langu naitwa Robert Mae. Shuguli hii ya leo, nikubadilisha mambo ya katiba. Katiba inastahili kweli kubdilishwa.

Kwanza nikianzia, nitaanza na upande wa mishahara. Mishahara ya chini inastahili kuwa kama elfu kumi. Ninasema hivo kwa sababu, hapa kuna wazee ambao wanafanya kazi. Na utapata mshahara wake ni elfu tatu, kama vile umetangazwa juzi na Waziri wa Labour. Mshahara huu wa elfu tatu, mzee huyu akiwa na watoto wako sekondari, ataweza kufundisha vipi? Na watakula vipi? Utapatawatu wengine wanapata zaidi ya millioni moja, kama yule Chief Justice. Na wengine wanapata elfu tatu. Na wote ni wazazi, na wana watoto wanataka kuelimisha. Mshahara wa elfu tatu utaweza kuelimisha mpaka wapi?

Pili, ni upande wa labour: Upande wa labour inastahili wale maofisa wa Labour kama wanafanya hizo kazi zao, pia wabunge wa sehemu kama hii ya Ganze, wawe pia wanapatiwa nafasi ya kusaidia upande huo pia. Sababu yake ni kwamba Maofisa wa labour, wanahongwa sana na matajiri. Unapata mfanyi kazi, pita pita kila siku, anadai haki yake lakini haipati. Atakopa mpaka mwisho atawacha ile kazi na hiyo ni haki yake. Kwa hivo inastahili awe kuna mtu anaweza kuwa nyuma yake na kuangalia kama ukweli unafanyika. Sababu hiyo ni kwamba mbunge atakuwa ana lazimishwa afanye hivo kwa sababu akiwa hawezi tekeleza mambo kama hiyo, wakati mwingine hawezi pigiwa kura.

Interjection: (Clapping)

Tatu ni majimbo: Majimbo iweko sababu yake nikwamba mfano mzuri sana hapa tayari kuna vijana wame enda college kama ya walimu. Na hivi sasa, hawana kazi. Unapata wakimaliza, course kule juu, watu wa bara pia wanaletwa hapa, wanachikuwa hizo kazi, na vijana wahapa pwani wanakosa kazi (Clapping). Kwa hivo majimbo lazima iweko. Hata kama watu wa bara watakuwako, tuseme kama Kilindini asilimia 75% wawe watu wa hapa pwani. Ile 25% ndiyo iwe ya watu wa huko juu.
Interjection: (Clapping).

Mengi yashaa semwa na wenzangu, lakini kitu moja ingine ile ya mwisho ni kwamba – ni kuhusu sheti za kumiliki mashamba watu wa bara wengi wana cheti hizi za kumiliki mashamba. Wanaweza kwenda kwa mabenki wanachukuwa mikopo, wanajiendeleza. Na shangaa sana hapa Ganze. Ganze nzima constituency yote hakuna mtu mwenye title deed hata mmoja. Mikopo hiyo sisi tutaiweza kuilipata aje? Naona mengi ishaa semwa lakini mimi yangu ni hayo machache, Mungu ambariki.

**Kazungu Kenga**: Hivi nataka kuendelea na choir yangu ya KANU "Tetemeko Mwaemba".

"Mimi Kazungu Kenga, nina maoni na kushangilia katiba na itatoka kuhuzu na choir. Harambee – Jogoo, Haraambee – Jogoo. Nini Umoja x 2 Umoja Nini? Jogoo x 2. Haraambee Jogoo?" (Giriama Dialect)

**Com. Abida Aroni**: Asante sana mzee Kenga na timu yako. Ningeomba tuwapigie makofi. Tuwa shukuru kwa ku-clap.

Asante sana mzee. Kwa wakati huu tungetaka kumpa nafasi waziri apate kutuzungumzia kwa dakika chache. Ana shuguli zingine za mambo kama haya sehemu zingine ya Ganze. Karibu Mheshimiwa.

Interjection: (Claps of welcome).

Mheshimiwa: Asante. Shukurani kwanza nataka nichukue nafasi hii niwakaribishe hawa wageni wetu, watume, ambayo mumesikia kwa muda mrefu. Kuna mama Abeda Aroni, ambaye yuko hapa, anaye anaendesha mpango huu, kuita majina, kuna Dr. Abdirizak A. Nunow ambaye ameketi karibu na mama Abeda, na yeye pia ni mmoja wa wale wanatume, halafu kuna hawa kina dada ambao ni waandishi, na bwana hapa ambaye anaitwa John Watubini na Gladys Osiego, Hilda miranga, and Rose Samba, hawa wote wamekuja hapa katika kuja kutimiza wajibu wao, na yule mwingine ambaye ni Jeff Wakingi ambaye yuko hapa, ambaye ni msimamizi wa mambo haya ya jumla kule Malindi. Lakini amekuja hapa kusaidiana na wale watu ambaye ni Daniel Mwaringa, ambaye yuko Vitengeni dakika hii.

Mimi nimechukuwa nafasi kidogo ni wasalimu kwa sababu ninataka niende vitengeni, vitengeni nako kuna shughuli kama hii ambayo anaendelea. Tume ilitupa siku moja pahali pawili, ambapo ni hapa halafu kuna Vitengeni pia, mambo yameanza wakati mmoja. Sasa nataka nipate nafasi pia nikimbie kule nikaweze kuona vile vinavyo endelea kule, ili niweze pia kujua kumekuwa na mpango gani. Kwa hivyo, nataka niwashukuru hapa, kwa kufika hapa, nataka niwashukuru nyinyi nyote kama raia ambao mumekuja hapa ili kuja kutoa maoni yenu, ili yaweze kuchukuliwa na hawa waliyotumwa katika mpango huu ambao unendelea katika nchi yetu ya Kenya, ya kurekebisha katiba ya Kenya, ambayo imetuchukuwa kwa miaka arubaini. Na sasa inaonekana ni vizuri katiba hii ijaribu kugeuzwa ili kushikana na wakati wa sasa. Kwa hivyo ni katiba ambayo imefanya kazi miaka arubaini, lakini sasa inaonekana kuna haja ya kupinduwa zipengeleo fulani, na kuweza kuwa na mpango mpya ambao utashikamana na mambo ya kisasa. Na haya maoni ndiyo haya, ambayo munaya toa kila mmoja anavyotoa anavyo ona, in sawa. Ningetaka tu kuwasii kwamba mwendelee kutoa maoni yenu, musiwe na hofu yoyote, musiwe na woga yoyote, mimi sina watu ambao nimewaleta hapa waje wazungumze kwa niaba yenu, nyinyi mutazungumza wenyewe munavyotaka na munavyo ona ni sawa sawa. Kwa hivyo nataka kila mmoja achukuwe nafasi hii kabisa, ili aweze kufanya lile ambalo analiona ni sawa na ni uhuru ambao tumepewa na nchi yetu.

Tunashukuru serikali pamoja natume kwamba iliona ni vizuri ije mpaka Mashinani huku kuleta karibu mambo haya, ili watu wasiwe na hatua ndefu ndefu za kusafiri. Waweze kukamatwa wakiwa karibu na sehemu zao, wanazoishi.

Yale ambayo yamezungumzwa katika hali ya kuzungumza juu ya mambo ya katiba, mimi nasema tu yakwamba, katiba ni kitu muhimu sana katika nchi yoyote. Na ni katiba ambayo inatakikana iwe na kuweza kuwakilisha watu, na Raia wake, kwa mambo ambayo yatakuwa ni yakuwasaidia maishani mwao. Kwa hivyo katiba ni kutu muhimu, nikiungo muhimu katika utawala. Katika utawala wowote, lazima kuwe kuna katiba ili iweze kuweka mambo sawa. Tuweze kujua rais ni yupi, na wale wengine katika mambo ya kikabala. Kwa hivyo ikiwa ni mwili wa mtu, ni ile mshipo wa katikati, ambao ndiyo wenye kufanya

mtu kufanya yale anayoweza kuyafanya.

Kuweza kutembea, kuweza kusimama kuweza kufuga macho, kuweza kucheka. Lazima kuna kitu ambacho kina simamia mambo yale yote. Kwa hivo katiba ni kitu muhimu ambacho tungetaka tuweze kuizungumzia.

Maoni ambayo yametolewa na mimi ijapokuwa tutakuwa na nafasi zetu kama wajumbe kuweza kutoa maoni. Tumependa sana miundo ambayo ni katiba ambayo inatoa mamlaka ya watu wa chini zaidi. Watu ambao wanaweza kuwa na nguvu katika Mashinani. Na ndiyo tumesema kwamba katiba tunaiona inaweza kufaa sasa zaidi, ni katiba ambao inaweza kutoa uwezo mwingi mikoani, uwezo mwingi katika serikali za mitaa. Hiyo inaweza kuwa ni katiba ambayo inaweza kutusaidia katika nchi yetu. Tungependa watu waweze kuwa na mamlaka yao, waweze pia kusimama, kusimamia rasilmali zao. Maana rasilmali ndizo ambazo mara nyingi zinaleta utetanishi.

Namna ya kusimamia urasilmali. Sasa ikiwa tutakuwa tumepewa uwezo kusimamia rasilmali zetu, na tunaweza kuziendesha wenyewe, tunaweza kupata nguvu, pengine anaweza kuwa na katiba, ambaye inaweza kufaa wewe. Kwa hivyo maoni haya ambayo mtatoa nina hakika yatakuwa yanaweza kusaidia katika mambo ambayo ni ya kuweza kusaidia kwa siku ambazo ni siku hujazo. Kwa hivyo ni siku muhimu siku ya leo. Ni siku ambayo inatakikana useme. Mukutano huu wa leo uko tofauti na mikutano yale mingine.

Mikutano mingine huja viongozi wakiwaambia nyinyi maneno. Leo ni nyinyi mumepewa nafasi katika mazingara haya. Muweze kusema, muweze kueleza, ambavyo munaona katiba inaweza kumfaa. Kwa hivyo hatutaki katiba hii, wakati ikiwa serikali mpya inatumia katiba hii, tuwe katiba hiyo hatutakuwa na chochote ambayo tumeichangiya. Sitaki uchangiwe na watu wengine. Ni sisi pia nasi tuweze kuhusika katika kule kusema. Kwa hivyo wakati hawa wamekuja hapa kwa siku nzima, wasikize maono yetu. Na wasikize ambavyo tunataka kusema. Kwa hivyo ningewasihi kila mmoja wetu ambaye yuko hapa, mke, kwa mume, kijana, na viongozi wote ambao wako hapa. Chukuweni nafasi hii za kutumia ili kurekebisha hii katiba. Bila shaka kuna makosa ambayo ameyaona kama raia. Ambayo unafikiria yakizungumzwa katika pahali kama hapa na yakikamatwa na hawa, yanaweza kusaidia mambo mengi ambayo pengine tunayaona hayako sawa.

Mumetaka habari ya mashamba, hayo yote ni mambo ambayo yanahakika. Yanatazamiwa kwamba yatasemwa na mpwani. Ikiwa hakutakuwa na kitu ambacho kimesemwa cha shamba katika mtu pwani, pengine kutakuwa na kasoro. Kwa hivo wengine waanze kutaja, endeleeni kutaja vile ambavyo munavyoona ni vipengeleo muhimu, ili mwangalie vile ambavyo mutaweza kufanya yale mambo yenu ya kisiku zijazo. Kwa hivyo tunazo taka katika katiba itakayo kuja ni kwamba ule utumishi, uwe karibu na watu labda. Wengi wamesema hivyo kwamba kuwe na hali za utumishi uwe karibu na wao, katika hali hiyo. Kwa hivo mambo haya ni mambo muhimu ambayo mumepewa nafasi, kuweza ku yazungumzia na musiwe na wasi wasi. Hakuna atakaye sema kwamba mumelaumu mtu yoyote. Umetukana mtu yoyote, tofauti tu ya leo, nikwamba tunatoa maoni. Hatutoi malalamishi. Kwa sababu kuna tofauti ya maoni na malalamishi. Kwa hivo, ikiwa tutazingatia zaidi kutoa maoni,

tutakuwa tumelenga ile agenda ya leo.

Yale malalamishi unaweza kuwa na wakati wake, ambapo anaweza kuyatoa. Lakini sasa kitu cha leo ni maoni yako, ungetaka Rais wako awe vipi? Atawale kwa miaka mingapi? Mjumbe achaguliwe kwa muda gani? Nazo mambo mengine ambayo yatakikana. Lakini la hakika, ni wakati mzuri huu ambao serikali imeona, watu wetu wapewe nafasi hii, na kwa hivyo na wasihi sana kila mmoja sikize mwenzake maoni yake, kama ni dakika moja, dakika tano, tuweze kuyasikiza. Na vile ambavyo mumekuja kwa wingi namna hii, itambidi ya kwamba muna musisimuko kuchangiya mambo haya. Ingekuwa hungeyaona ya faida, hamungekuja.

Kwa hivyo na wasihi sana kila mmoja asikilize mwenzake, maoni yake kama ni dakika moja, dakika tano, tuweze kuyasikiliza na vile ambavyo mmekuja kwa wingi, namna hii ni dalili ya kwamba mnamusisimuko mnataka kuchangiya mambo haya. Maana kama hamgeyaona yana faida hamgekuja na wengine bado wakili kuja kwa sababu ni kitu chako ni kitu ambacho ni cha serikali utakayo ipenda kesho katiba ya kesho, twapanga mambo ya kesho. Yale ya jana na juzi yanaenda kuishi lakini ile ya kesho tumepewa nafasi tuweze kichangiya kwa hivyo sisi wote tukiwa hapa wakati huu wa leo nawasihi sana, muweze kusema maneno yenu . Itakuwa ni heshima kubwa ambayo mutakuwa mumeifanyia Katiba ya Kenya, kuisemea na kuichangia kitu fulani, ili tuweze kuona mambo bora yakiweza kugeuzwa kwa hivyo ikiwa tunataka mambo haya ya mageuzo hapa na pale, wakati ni huu hatuwezi kujua kama itakuwa tena nafasi nyingine lini, ikiwa tutaenda kwa muundo ambao imeanziswa kwamba ni baada ya miaka arubaine ndio Katiba nyingine izungumzwe, basi miaka mingine arubaine wewe na mimi tutakuwa wapi? Pengine tutakuwa hatuko lakini, chukuwa nafasi ya sasa. Ya hivi uko hai na umepewa nafasi na una akili, una bongo, ya kuweza kuwasa kitu uweze kusema vile unavyoiona ni sawa. Katika hali ya maisha yako, ya siku zijazo. Kwa hivyo mimi ilikuwa nichukuwe nafasi hii niwashukuru waliyo kuja, niwashukuru nyinyi kama raia muliyowacha shughuli muhimu zingine lakini hili ni jambo la kitaifa. Yale muhimu labda, ni kulima ni chakula ni muhimu, lakini hili ni jambo la taifa nzima. Na jambo lolote la taifa lina umuhimu. Kama ni chajo niza kitaifa, kama ni kitu kingine, ni cha kitaifa, magonjwa, kwa hivyo katiba nayo ni ya kitaifa. Kwa hivyo lazima mambo mengine yawekwe kando, watu waje wazungumze jambo la kitaifa. Kama siku ya kitaifa ya Madaraka, ya Jamhuri, ni siku ya kitaifa. Kwa hivyo ni kitu kizito, hiki ambacho twa kizingatia hivi leo, kwa hivyo nikiwa naondoka hapa mutaendelea kwamba nataka nifike Vitengeni ili niwe kuona kule pia upande ule kama vilivyo desturi basi, kama unasehemu mbili na umzazi basi (Giriama Dialect) sehemu mbili. Kwa hivyo haya ndiyo ambayo nilikuwa nataka niwaeleze niwashukuru sana, muendeleeni kutoa maoni yenu yatapokelewa bila shaka na sisi tutaweza kuwa tayari na tutashukuru tutapata kwamba mmefika hapa hivi mumevyo fika na mumesema maneno yenu kwa uhuru ambao munaoma ni vizuri. Kwa hivyo kuweni nasiku jema hapa. Semeni munavyo weza kusema wale nao nataka nikawasikize kule Vitengene nijue kidogo nao wamekuja kama mlivyo kuja upande ule, halafu tutachanganya yale mengine. Juzi tulikuwa Bamba tarehe tatu naikawa pia nao wanasema mambo yao. Kwa hivyo ninataka nishukuru tume nzima hii imetushika division zetu tatu zote, katika hali ya kutoa maoni, kwa hivyo hakuna tarafa ambayo itasema ya kwanba imeaachwa nje. Zote zimekamatwa nani muhimu kila maoni ya pembe zote yaweze kushikwa. Kwa hivyo na washukuru, mukae salama tutaonana tena, lakini endeleeni na

maoni yenu, yanapendeza yanavutia sana ukiwa pale, unasikia vile watu ambavyo wana maono yao, katika maisha yao ya siku zijazo. Kwa hivyo asanteni, kaeni kwa usalama.

**Interjection:** (clapping)

**Com. Abida Aroni :** Asante sana Mheshimiwa kwa mawaidha yako na maneno yako ambayo yana zidi kutupa moyo. Ningependa kuwa ambia kwamba watu wasehemu hii muna bahati sana kwa sababu, kwa wiki mbili unusu hivi, tumekwenda katika constituency zaidi ya kumi. Tano huku pwani, tano mkoa wa wakati, hatukupata kuona kiongozi yeyote wawakarishi bungeni katika constituency yake. Kwa hivyo nadhania muna kiongozi halisi, mheshimiwa tunakushuru sana kwa kutupa moyo.

**Interjection:** (clapping)

**Com. Abida Aroni**: Nadhaniya basi tutaendelea kwa vile listi yetu bado ina watu wengi zaidi. Naningewao omba musipitishe dakika kumi kwa watu ambao wamazungumza na ambao wananakula msipitishe zaidi ya dakika tano tuweze kupitia listi nzima, kabla ya kufunga mkutano, ikiwa bado hakujakuwa na giza. Na jina ambalo tunalo kwa wakati huu ni Tabu Jogolo? Samahani ikiwa sikuweza kutamka jina lako sawa sawa.

**Tabu Jogulo:** Asante sana. Langu mimi ni kushukuru hii siku ya leo, siku ya kubadirisha katiba. Sina mengi lakini ni kwenda pale mahali pamchanganyiko wa makabila kukaa pamoja. Hilo linaingia hata nyumbani, boma likiwa kubwa lazima vita viweko. Halafu watu wanachana kukula pamoja na kuchenga maboma tofauti tofauti halafu wanaanza kuwasiliana kimawazo. Hapa sasa mimi ninataka tukiendelea kukaa pamoja tumegunduwa kwamba wengine wananyanyaza wenzao. Ile sahani tunakula lakini wengine wanakula riziki za wenzao. Ni sawa kila mtu kukula pande zake. Iiiwa ni hatari sana mwingine akiwa ana lala na jaa hapa akiangalia mwenzake anakula pale. Si vizuri.

Lingine, tunapata hizo ofisi za serikali zinafanya nyingine hiki kirauni badala ya kuheshimika kinaogopewa. Ofisi ya DO ni ofisi ya hapa. Ni sawa iwe kila mtu yuko free na ile ofisi. Tunataka pale pawe mijikenda kama DO. Kwanzia ofisi ya sub chief, chief, DO wale wawe ni watu wa kule kule.

**Interjections:** (people clapping)

**Taabu Jogubo :** utakuta wengine hawajui kiswahili wakiingia pale wakiona yule askari pamoja na DO wake, anarudi nyuma, halafu haki yake inapotea. Utakuta wengine hapa wanasoma wakipata nafasi akienda Kilifi kule, akipata sub chief akivaa akienda kule juu akirudi hapa akionekana ana kubiwa. Kiraoni inakimbiwa ambao ni kitu kizuri, watu wanakikimbia. Yote yanaletwa na yule mchanganyiko maalum. Usiweze kutu changanya, ukiwa unaona kuna hatari baadaye ambao itakuja. Leo ni siku ya kubadilisha Kati tubadilishe. Kila mtu akikaa kule kwao sio kwamba hatuwezi kuwasiliana lakini sasa ni sisi tupate riziki zetu kama ilivyo pangika.

Hawa subchief, chief, na DO wale wanatakikana wawe ni watu ambao wanapitiswa kupitia kura. Utapigia kura mtu ya bara? Haiwezekani. Kwa hivyo tunataka hizi ofisi ziwe na watu wa kule kule na sisi zile nafasi zote ambazo zinastahili kuendelezwa, ziendelezwe na watu wa hapa. Kama vile ma file zote sitoke zote huko bara zije hapa, Mombasa. Hapa ni karibu hata namguu unaweza ukafika hapa. (clapping)

Utakuta kosa la kitambulisho ana ambiwa toa elfu mbili ama ubebe mtu hapa akipeleke kule ku sababu huko juu. Kama ingekuwa hapa mambo yangu ingekuwa rahisi. Utakuta tunalemaa chini kumbe saa ingine ni zile garama ni kubwa. File zote zitoke zije hapa. Mambo zetu zote ziwe sina tengeneaewa hapa hapa na sisi tungenegenezwa hapa hapa, na sisi tuweze kuoja ule uhuru. Lakini la sivyo wengine tutafanya kusikia uhuru na hatutaoja uhuru hata milele na milele. Asante.

**Com. Abida Aroni:** Sidi Kazungu? Yuko?

**Sidi Kazungu:** (Giriama Dialect**)** **Translator.** Mimi naitwa Sidi Kazungu. Maoni yangu yote nimeandika katika karatasi. Basi.

**Com. Abida Aroni:** Karisa Mume Ngua? Ama ndiye huyu mzee, Foleni Kadenge? Rogers H Gala?

**Rogers H. Gala:** Asante sana Bi Mwenye kiti na watu wote ambao tumefika hapa. Mimi nataka kusema kwamba serikali yetu na katiba ambayo tunahitaji kwa wakati huu ningependa kwamba iwe ya majimbo ambayo kwa hakika majimbo itakuwa kila mkoa unajutegemea na unaweza kufanya mambo yako ambayo yanaweza kutoshereza wenyeji na wakaaji wa sehemu hiyo.

Pili, nataka kusema kwamba, Rais awe na mamlaka ambayo itamuwezesha kuendesha Kenya hii kama vile ambavyo anaweza kuongoza vile ambavyo wananchi wanapenda. Na kwa hakika Rais akiwa anaweza ndiyo ataweza kuendesha na kufanya yote ambayo anapendekeza wananchi wake waweze kuendelea.

Tatu nataka niulize katiba hii ya sasa ambao tunataka kuiunda elemu ya msingi iwe ua lazima ya kila mzaliwa na akifika miaka ya kwenda shule mke kwa mume awe ni lazima na iwe ya bure. (clapping).

Kipengele ambacho nataka kusisitisha ijapo wenzangu wamesema nataka kusema kwamba, serikali, na kipengele cha Katiba kihuzishe wale wastaafu wote wa serikali waliostaafu kusahauliwa wakipewa ile haki yake basi. Wanawasahau kabisa ambao waamefanya kazi nzuri, na wamefanya kazi na wanashkrani wakipewa, basi wanasahauliwa hawa kumbukwi tena. Naomba katiba hii iweke kipengele cha kwamba akiwa amestaafu baada ya miaka mitano wafikiriwe ingawa increment ya miaka mitano

mitano aweze kupata kwa sababu wamefanya kazi nzuri na wanapaswa kufikiriwa mara kwa mara kwa hivyo miaka mitano waweze kufikiriwa na kupewa angal chochote na kuongezwa aweze kwa sababu cost of living inapanda kila wakati na akipewa mwananchi ambaye amefanya kazi nzuri afikirewe miaka mitano na awe kila mara anaongezwa kwa sababu maisha ni magumu. (People clapping)

Kwa hayo machache, nataka kusema kwamba ardhi yote ambayo ni Government land ambayo ni Crown land tunaita hapa pwani ichukuliwe na serikali na ipewe wale ambao wanaishi pale wapate nafasi ya kwanza. Tunataka kila mmoja akipata basi ile imebaki yule ambaye atikuwa yuko karibu anaishi na wao apewe lakini first priority iwe wale wakaaji wa hapo kwanza. Kwa hayo machache nataka kusema hayo mengine yako karatasine imesemwa na wengi. Asante sana.

**Com. Abida Aroni**: Mary Kanze Mwarua? The women have started going.

**Mary Kanze Mwarua**: Mimi kwa jina naitwa Mary Kanze Mwalua. Sitazungumza. Mengi yako humu kweny karatasi.

**Com. Abida Aroni:** Helena Katite? Ana memorandum? Yuko?

**Helena Katite**: Kwa majina naitwa Helena Katite. Yote nimeandika hapa.

**Com. Abida Aroni**: Monica Mwalata? Monica Mwalata? Kwa jina naitwa Monica Mwalata kama mulivyo sikia. Maoni yangu mimi, la kwanza:

Madiwani: Ikiwa umechaguliwa kama diwani ama kiongozi, kwa hiyo miaka mitano na kama uongozi wako haukuridhisha wananchi, kabla ya ile miaka mitano kama inawezekana, kuwe na uchaguzi mwingine ambao utapatikana mtu mwingine badala ya wewe ambao utakuwa umechaguliwa.

La pili, elimu ya wasichana: Wasichana na wavulana, wazazi wahakikishe wanapeleka watoto wao shule, wasichana kwa wavulana iwezekanavyo.

La tatu ni kuhusu hao hao wasichana. Mzazi ambaye atachukuwa mahari kwa msichana yeyote wa shule achukuliwe hatua.

Nne, hii ni kuhusu nursery school. Watoto wote katika wale wazazi, watoto wote kuanzia miaka mitatu hadi miaka sita, uhakikishe mtoto wako unampeleka nursery, ama sivyo mzazi achukuliwe hatua.

La tano, elimu ya watu wazima. Wakina baba na wakina mama, serikali itie mkazo wa kina mama na akina baba wahudhulie masomo ya watu wazima. Asanteni.

**Com. Abida Aroni:** Hassan Kalishu?

**Hassan Kalishu:** Ma commissioner wote mlioko hapa, viongozi nyote mlioko hapa siku ya leo akina baba akina mama hamjambo?

**Interjection:** Hatujambo.

**Hassan Kalishu:** Hamjambo tena.

**Interjection:** Hatujambo.

Hassan Kalishu: Kwanza ninasitikika, nimefahamishwa kwamba majina yameaandikwa mengi sana lakini nimesikia kwa bali kwamba wengine hawataki kuja kusema maoni uao. Mimi kama kiongozi, mimi ni Hassan Kalishu. Hare, mimi ni diwani wa Dungisha. Natoka tarafa ya Ganze. Nina masikitiko makuu kama kuna wengine wenu, nilivyo sikia kupitia na habari fulani nilivyo pewa na viongozi hapa. Mmeandikisha majina yenu, sasa humutaki kuongea. Munasema mimi sina moani. Mimi sina maoni mimi nina sikitika kwa sababu hawa ndugu zetu wako hapa na wanataka maoni yetu wengine wenu munafikiria kwamba mukirudia rudia ni vibaya lakini ni vizuri kwa sababu kule wakifika wanaangalia ile nambari iliyo sema hivi ni ngapi ili tujulikane tunataka nini na hatutiki nini. Pengine leo nitalalumika na Commission hii si siku ya kuelimisha lakini hapo ningetaka mtaje. Kwa hivyo, kama ni mmoja wao aaliyesema kwamba mimi sitaongea, ningetaka ubadilishe mwoyo wako useme unataka kuongea. Mimi maoni yangu ni serikali. Serikali iwe ya majimbo. Kwanza hata tumechelewa kupata majimbo, kwa sababu mmoja alikuwa hapa kitambo kidogo akasema kwamba Lancaster House watu walienda wakatengeneza

Kati iba na wakaafikiria ya kwamba baada ya miaka fulani, Kenya hii itakuwa na utawala wa majimbo. MarehemuNgala ndiyo alikuwa amesimamia lakini haijatokeya kwa sababu karibu na kuwe majimbo yafike, Gala akawa marehemu kwa bahati mbaya. Kwa hivyo, tunataka serikali ya majimbo. Kuna majimbo ya kila mtu kwao na majimbo ya kila mtu abaki pale alipo lakini sisi twataka kila mtu abaki pale alipo isipokuwa tu wakati wa kugawanywa kama ni rasilmali, mtu wa

Pwani, mimi ninasemea pwani saa hii, na mwingine yeyote yule apatiwe nafasi ya kwanza na nafasi kubwa. Wale waliokuwa wanasema asilimia hamsini, mimi naongezea ikuwe asilimia tisaini. Halafu wale wengine kumi wakibakia, haya wagawanyiwe. Mfano mkubwa mzuri ni hali mashauri ya bandari ya Mombasa, Kilindini. Asante kwa kunisaidia. Kilindini ni mahali ambapo kuna utajiri wa pwani nzima. Meli zote za Kenya zinapitia Kililndini. Leo ukifika pale katiba ina andika watu. Tunataka safari hii katiba iseme mtu wa pwani na Swale Mohammed peke yake, kwa sababu anatoka Mombasa, ni Hassan Karisa Hale kutoka Ganze na mtoto wake na mjukuu wake nao wakaandikwe kule kazi. Asilimia tisaini ya watu wa pwani tumesikia hiyo arimashauri ya bandari vile vile imeuzwa. Inauziwa watu kwa nini? Sisi hatujapata nafasi ya kuhuzishwa katika ku-privatize. Privatization inaendelea katika hali machauri ya bandari ikiwa katiba hii ikiwa leo Katiba hii itagueka, wacha mtu wa pwani naaye apewe nafasi ya kwanza awe ni mtu wakwanza kwa wingi kununua share katika hali ya hali mashauru ya bandari.

**Interjection: (**People clapping)

**Hassan Kalishu:** Mashamba. Wengi wameongea kuhusu mashamba na mimi ninaunga mkono maaoni yao. Nataka tu kuongezea kwamba, leasing kukondisha kuishe. Watu wamekondisha mashamba miaka tisaini mtu anakondisha shamba mpaka anakufa amaenda waarabuni, anaenda uraya, huko bado anasema Kenya kuna sehemu yangu kama wale wamazrui, pole mazrui kama uko karibu, lakini huko sehemu hiyo ndiyo munafanya hiyo kazi halafu mimi ninabaki squatter hata na mwingine anabaki squatter mahali. Leasing iishe. Watu wagawanyiwe mashamba yao waishi wakipewa title deed zao, Katiba hii kama itageuka, ningeomba upande wa mashamba, vile vile pwani iwe ya kwnza kugawanywa, watu wagawanyiwe mashamba yao, na wapewe haki za kumiliki ardhi. Kwote kuwachwe lakini pwani waanzie pwani, kwa sababu walichelewa kufanya hivo ndio maana sisi tunasema ni maskini, ni maskini kweli, lakini hatujapata nafasi kama wale wenzetu. Mwenzangu amesema hivyo nimekumbuka. Wenzetu kule wamefaidhika kwa sababu serikali ilikuwa karibu nawao labda.

Uongozi. Tumesema habari ya uchaguzi sawa Rais awe mmoja, wa Kenya, achaguwe awe na uwezo mkubwa wakuchguwa mawaziri ni sawa. Katika vipindi vya miaka mitano. Na unga mkono hapo, nimesikia mwenzangu mwingine akisema diwani achaguliwe, akimaliza miaka miwili atoke, mwingine amesema diwani akimaliza miaka miwili hajafanya kitu atolewe. Mimi ninaomba mwendelee kuchaguwa diwani kwa kipindi cha miaka mitano. Miaka mitano hiyo anauwezo wakasoma vitu vingine dani na nje kusiwe na kikwazo cha kumuondoa hapa katikati. Hatakuwa amepata wakati wa kujifunza mambo mengi ili awaletee uwakilishi mzuri sehemu yake ya kata anayo akirisha. Kwa hivyo miaka mitano ya diwani, katiba hiyo iendelee hivo hivo.

Mabaraza. Ni vizuri mabaraza wapate meya ama Mwenye kiti wa baraza akiwa Form 4 kama iliyotanguliwa kusemwa na wenzangu na pia ningependa katiba hii iseme kwamba achaguliwe na watu. Asichaguliwe kule barazani na madiwani peke yake. Achaguliwe na watu wote katika sehemu anayotoka. Kama anatoka taraka ya Ganze, apigiwe kura kama vile mbunge anavyo pigiwa kura na akae kwa miaka mitano.

Diwani. Nimesikia diwani anatakikana awe diwani tu, mtu yeyote ambaye hakwenda shule bora tu awe anasikizana na watu. Ni sawa mimi maoni yenu nimeyapenda sana, lakini sisi tulioko hapa zote, ni watoto wa Stone Age. Na mimi nilipozaliwa nilikuwa sijui kusoma wakati huo nikiambiwa niende shule nimepata mabandiliko mengi sana. Sasa kama mpaka leo tunasema diwani asiende mpaka form 4, tunarudi kwa stone age? Tunatoka bali? Tunazidi kurudi bali? Kwa hivyo mimi naona katiba hii irekebishe kipengele hicho. Diwani awe Form 4 kama hana elimu ya kutosha kabisa, ya chini awe form 4. Hapo tutakuwa tana saidiana kimawazo. Tutakuwa tunasaidiana ki maoni na tutaendelea na uongozi mzuri.

Wale wenzangu waliokuwa wanasema mabaraza yapewe uwezo, ni sawa. Utaona kwamba mshahara wa diwani ni bunge ndio inasema diwani apate kitu gani, na diwani yuko mashindani. Anatakikana aende mazishini. Kuna matumizi mengi mpaka bunge akija. Diwani ashaumia kwa hivo, naomba katiba hii ibadilishe baraza lenyewe lipangilie mipango ya malupu lupu ya diwani kuliko bunge wapitishe. Utaona kwamba hata wabunge pia mishahara yao wakisikia madiwani wamepeleka mswada bungeni,

kwamba walipwe kiasi fulani cha malupulupu, wabunge wanakanyanga. Sasa wao wapange yao kule, sisi maluplupu yetu ama maaalupu lupu ya madiwani watapanga wenyewe kutoka kwa mabaraza. Asanteni kwa kunisikiza. Asante sana. (clapping)

**Com Abida Arono**: Kamutu Karisa?

**Kamutu Karisa**: Asante sana kwa kunisikiliza. Mimi naitwa Kamutu Karisa kutoka Petanguo. Nimefurahia sana mpango huu wa Kati, na tangu pale tuliposikia basi tunaona unachelewa
maana tuna nyannyaswa basi lakini hatuna la kufanya. Maana tunaambiwa tulinyakuwa uhuru kutoka sitini na tatu. Lakini tukiangaliya hivi tunaona hatujapata uhuru. Kwa vile tunavyo teseka siku zote ni watoto wetu wanaenda shule. Kuna wengine wanajiweza na wengine hawajiwezi. Mtoto anaenda anamaliza shule na babake hana kitu. Wengine wamechelewa lakini kuna ambiwa kuna bursery. Itawasaidia watoto. Bursary yenyewe upande mwingine inatoka, upende mwingine haitoki. Basi watoto wamebaki manyumbani na vile baba zao hawajiwezi. Unalazimishwa ati upeleke mtoto sasa hata wewe mwenyewe unalala jaa atapeleka mtoto na nini? Basi ndio umaskini umezidi hapa pwani. Tena umezidi sana. Wengine wanafundishwa wanaenda huko wanaabiwa leo kuna andikwa watu kazi basi watu wakifika huko basi watu wa bara ndio watachukuliwa. Lakini watu wa pwani hawawezi kuchukuliwa maana ni maskini.

**Interjection**: People clapping)

**Kamutu Karisa :** Saa zote tuna aharaiwa, Siku zote tuna dharaiwa. Basi tunasikitika sana ikiwa skuli watoto wataenda wakisoma bure, hata wale maskini wata tajirika. (clapping) maana ni wengi maskini imejaa kweli kweli. Maani hakuna tajiri upenda huu wa Ganza maana kila mtu ni maskini kwa vile tunanyanyaswa.

Ninapenda sana hata kama ile elimu ya watu wazima tulikuwa tunaendelea sijui kama vimekwenda aje, ninakuja ninauliza walimu wale wakufundisha watu wazima wataambiwa watakuja watakuja, akija siku moja siku tatu wanafunzi wanaenda pale wazee wamewacha kazi zao, wanasimama hapo hakutakuja mwalimu yeyote. Ukiangalia hivi basi tunaambiwa ni vile ambavyo hatu kusoma kweli si kusoma lakini nasikitika. Huko kusoma hata sasa nilikuwa naendelea na mambo ya gumbalu sasa naambiwa isitajiwe tena, lakini nitaitaja maana tulikuwa tukienda huko tunaambiwa tunaenda gumbaru wengine wanasema ni nyambaro.

**Interjections:** people laughing.

**Kamutu Karisa:** Basi tunaenda hivyo nyambaroni. Tunaenda tunasoma kidogo tunaelewa hata kama tumekuwa wazee macho yanakufa lakini tukipata miwani tutaona zile herufi. Tunataka sana hiyo elimu ya gumbaru iweko.

Tena kitu kingine ambacho kinatuchoma roho, yale kama sub-chief na madiwani basi na machief. Watanye kuchaguliwa na wananchi. Maana kuna wengine wanaumiza ma roho. Huna lakufanya ukiwa unapoenda usipende ni huyu hapo.

**Interjection:** People laughing and clapping.

**Kamutu Karisa:** Ni huyo huyo atakuwa anakuumiza ni huyo huyo. Maana hakuna la kufanya maana yeye ana kirauni. Basi tunaumia sana sisi. Uutakuwa tunaenda tu kama vile umechelewa basi ukaambiwa ni babako wa usa huyo babako mwenyewe amekuja utafanya nini? Ni lazima unakaa hivyo basi tunaumia. Sisi tunataka kama kattiba itageuzwa basi igeuzwe akiwa chief atichaguliwa diwani mtuele pia achaguliwe.

**Interjection:** People clapping.

**Kamutu Karisa:** Achaguliwe na raia yule ambaye anatambia nzuri ndiye atachaguliwa Hata ukiwa umechaguliwa na unamaliza miaka miwili hufai utatolewa.

**Interjection:** People clapping.

**Kamutu Karisa:** Maana utakuwa unaumiza watu. Kuna mipango mingine mimi ni mwanachama wa kikundi. Tumefanya mpango tukaweka zingine kukundi chetu tukaweka mfereji wa maji, maji yenyewe haitoki hata kila siku inatoka kidogo. Lakini bill ikija, basi utapelekewa elfu thelathini hata mia mbili zenyewe hukupata.

**Interjection:** People clapping.

**Kamulu Karisa:** Basi elfu thelathini sikikuja ile ni bill ya maji, na hata hukupata hata elfu moja hiyo wiki nzima. Mwezi ukimalizika waweza kupata kama elfu mbili na mia tano unaletewa bill ya shilingi elfu thelathini utazipata wapi? Basi tunaona hakuna maendeleo. Maendeleo ni kama hayo tunafanya tunajikaza lakini hatupati kitu, tuko hivi hivi. Ukiwaangalia watu wa pwani hawanamaendeleo hawajui maendeleo, tunayajua lakini hatuna la kufanya maana akiwa ni babako hata akiwa mbaya ni huyo huyo tundiye babako.

**Interjection:** People clapping.

**Kamutu Karisa:** Basi ikiwa kweli itawezekana hiyo katiba ikabadilishwa, basi kila kitu kinadirishwe. Kile kibaya kiachwe, kibaki kile kizuri. Ndio tutakuwa tumepata uhuru. Lakini uhuru wa kunyanyazwa hatutaki. Hata akiwa ni huyo kiongozi naye

akichaguliwa, awe ni kiongozi wa kufaa. Lakini akiwa hafai, basi tutakuwa na manunguniko saa yote. Na manunguniko basi inavunja imani kama watu wa Kristu tunavunjika imani kwa manunguniko. Hata ukiomba huyo Mungu na unanungunika huwezi kupata kitu.

**Interjection:** People laughing and clapping.

**Kamutu Karisa:** Basi hayo yote yaangaliwe kama katiba itabadilishwa basi ibadilishwe kila kitu. Wawe watu wa kupendana tena kuna wengine kama hizi dini wanadharauriana. Ukiwauna dini yako, una dini yako. Usidharau dina ya mwenzio. Kuna wengine wanadharau dini ya mwenzake. Anasema hiyo dini haina kazi. Lakini huwezi kulazimisha maana ruho yake imepanga hivyo hivyo. Ikiwa u mwisilamu una dini yako.

Ukiwa u mukristo, una dini yako. Huwezi kudharau dini ya mwenzako. Maana ukimdharau basi itakuwa hakuna uhusiano mzuri na Mungu anasema tuwe tunapendana. Na kupendana ni kuwa mumepatana, munazungumza mpango mzuri ndio mnapendana. Kwa hivyo mimi nina furaha kwa kuletewa katiba siku ya leo nilikuwa ninasema lakini takuna? Kumbe itakuja kweli. Nimekuja nikasema hata sikuwa na mtarajio wa kuwa hapa lakini Mungu amenibariki. Nikaja nikaambiwa basi ukiwa utasema basi utaandikwa nikasema basi ninani anaweza kukubali kibaya. Kila mtu anataka kizuri kile ambacho nakitaka nitasema. Kwa hivyo nimesema. Ninasema asante. Jina langu naitwa Kamutu. Asante.

**Com: Abida Aroni:** Kahaso Katana? Yuko? Beatrice Bahati?

**Beatrice Bahati:** Pia mimi nashukuru siku ya leo. Hata nilikuwa naona leo haitafika lakini – Kwa majina naitwa Beatrice Bahati Tembe: Majimbo nataka iweko na kwa upande wa Rais nataka watu wa pwani tuwe na Rais wetu kwa maanake sisi wakina mama tukaingalia hivi tunanyanyaswa sana kwanza hasa hapa Ganze hata Mwaeba.
Kwabudu shetani. Sote tunajua kuwa shetani hata hana uzuri kwa mwanadamu. Kwa nini tumwabudu basi? isiweko. Asanteni.

**Com. Abida Aroni:** Joo huku tafadhali. Immanuel Charo?

**Immanuel Charo:** Ninawapongeza nyinyi ambao munahuzika na mambo hii ya Katiba Lakini jambo la kuhuzunisha ni kwamba mulituelimisha mambo ya Kati kuchelewa, ili hali mukihitaji kupewa maoni kwa uharaka.

**Com. Abida Aroni:** "Bwana charo tafadhali tupe maoni kwa vile hatuna namna ya kukusaidia kwa hayo unayosema".

**Immanuel Charo:** Kuhusu Rais, mamlaka yake yapunguzwe. Isiwe kama Idi Amin analala anaota, asubuhi nikuamrisha. Twataka Rais awe atashirikiana na mbunge na kamati kuu, kushughurikia masilahi ya nji.

Kuhusu kutumia kiasi kikubwa cha fedha za taifa kwa shughuli ama safari za kama pengine Rais, anaenda mahali fulani,

unakuta gari mia moja, zote zinatumia mafuta na hiyo ni hasara. Ikiwa watu Mashinani wanateseka, pesa zinatumiwa vibaya.

Kuhusu wabunge, pia nao waache kujitetea wenyewe wakiwa mbunge. Mishahara yao ni mikubwa tena bado wanataka kuongezwa. Wanataka hata mabunduki watembee naya. Wamesahau wananchi waliyo wachaghuwa. Wabunge wakienda mbunge twataka washughulikie wale waliyowachaghua. Serikali twataka ya majimbo kwa sababu Miji Kena amevumilia siku nyingi sana. Nani bahati kupata Fulsa hii ili tuweze kutoa maoni yetu.

Majimbo yaweko ili huduma tuweze kuzipata. Hivi leo miaka mingi kutoka tupate uhuru, barabara zetu ni hizo munazo ziona. Sipitali zetu ni zile munavo ziona, nduni, twataka majimbo.

Kuhuzu wazee wa vijiji, Wanakazi ngumu sana. Kuzungukia wananji kila siku. Nje, ataenda zunguka namna gani ikiwa nyumbani ameacha kuna njaa? Jamii yake wanalia. Hawa ni viungo muhimu katika hii serekali. Kati iwahuzishe wazee wa vijiji wawe na bahasha yao.

Machifu pia wanakazi ngumu. Hawa wanafaa mishahara yao iangaliwe na pia hali ya usafiri; wapewe hali ya usafiri. Twataka serekali ijayo iwapatie machief hali ya usafiri. Kama ni magari, kama ni piki-piki. Lakini twataka wawe wakifanya kazi kwa hali ambayo itakuwa inafaa. Na pia wapate usaidizi ambao ni askari. Wakati mwingine kuna manjanga yanatokea, chief anafanya nini? Lakini chief apate usaidizi wa askari.

Nitaongea kuhuzu uongo ambao nimeusikia kuhuzu maili kumi yakwamba sijui ni ya mazrui, sijui ni ya mazurungi, huu ni uongo mtupu. Walipokuja hapa mukoani, miji kenda alikuwa hapa. Na hakuna mahali abapo panaonyesha yakwamba kulikuwa na makubaliano yakwamba mazurui alinunua sehemu hiyo, na kama alinunua, sehemu hiyo na kama alinunua, alinunua kwa nani? Kwa hivyo, swala hilo naona ni uongo mutupu. Sehemu hii ni ya mkazi wa hapa pwani, anahaki ya kuimiliki na kunufaika.

Nataka Kati ikomeshe ujire wa watoto. Habari za watoto wadogo kwajiriwa kuuza sabusa, kuuza vitu vidogo vidogo. Kati ikataze, na mtu yeyote akipatikana ameajili mtoto mdogo, achukuliwe hatua.

Pia nahimiza usawa wa akina mama na akina baba, ili waweze kushauliana. Na zaidi ya hapo ningetaka kuwe na utaratibu wa hivi viwango vya mahari Mvulana mwezio anataka msichana, amekuja kwako unamwambia elfu mia moja. Kuwe na utaratibu, ambao hata Katib itairuhusu kuwe na kiwango kamili. Zamani ilikuwani elfu tatu hata wende wapi ni elfu tatu ulikuwa unatoa. Kwa hivo kuwe na kiwango kama ni elfu sita, iwe ni elfu sita. Maana wao pia wanaenda kuaza maisha wanahitaji pesa wakitoa elfu mia moja halafu wakateseke faida ni nini?

Kuhusu haki wa kuabudu. Ningesema ya kwamba haki ya kuabudu iendelee. Lakini kuwe na njia furani ambayo itazuia hali hiyo isije hali hiyo ama uhuru huo ukatumika vibaya. Kwa hivyo uhuru wa kuabudu uweko, lakini kuwe na utaratibu ambao unazuia uhuru huo kuharibiwa.

Naona ninagongagongewa lakini hata hivyo, namoba yale yote ambayo wananchi wameyatoa tume ikaweze kuyatia maanani maana jimbo hili sisi tunataka majimbo. Asanteni.

**Com. Abida Aroni:** Asante. Hassan Kalume?

**Hassan Kalume:** Basi asante sana tume ambayo imeweza kutembelea hapa kwetu Ganze, sehemu ambayo imewakirishwa na mbunge wetu mheshimiwa Waziri Noah Katana Ngala. Kwa jina ninaitwa councillor Hassan Kalume, kutoka wodi ya Kauma.

Nimejisikia mimi pia nitoe changizo zangu ijambo nimechelewa lakini nashukuru vile mulivyo nipatia hii nafasi, najua mengi yamezungumuzwa, lakini katika uchangizo yangu, mimi ninawaunga mikono wasemaji wezangu, waliokuwako hapa ambao wameongea kuhuzu utawala.

Hasa ni kisema utawala ni machief. Ninataka Katiba hii ambayo hivi sasa tuna itengeneza hapa itilie maanani utaratibu wa machief wetu. Machief wachaguliwe kupitia na kura. Hiyo ni sawa kabisa, maana hapo kwetu pwani tumeona machief wengine wamechanguliwa, kwa mlango ya nyuma, ati kwa sababu ni mwalimu. Hiyo ninaomba Kati iondolee mbali kwamba lazima mtu awe ni mwalimu ndiyo achaguliwe kuwa chief. Pana msemaji mwezangu ambae amekuwa hapa. Ameongea ya kwamba wapigiwe kura. Na ni sawa kabisa. Na machief hao wapewe vipindi viwili tu vya kuhudumu kama chief.

Kusudi ya kusema vipindi hivyo ni kwamba kuna machief wengine ni waizi na ni wa nyanyasaji katika sehemu wanazo tawala. Kwa mfano utaona mtu ni kiongozi wa location anafanya maovu na maovu yale yeye katika utawala anashirikiani na kiongozi wake ambaye ni D.O. Uchafu umeaza kwa machief hadi kwa ma D.O. Chief akila, D.O. naye anamlisha DO, naye anamlisha DC, DC naye anaenda mpaka juu huko. Anaingia mhadi katika ofisi ya Director.

Halafu sasa, akishajulikana, wewe kama kiongozi ambaye umechaguliwa na wananchi, na wameona ule uovu una unafanya na chief, ukianza kuupeleka utaandika barua uisukume kwa D.O. itakanyangiwa. Utaandika mbarua useme mbona sipati majibu, ndio inaenda barua, itaenda barua, itaenda mpaka mwisho itaingia kwa state council.

Ikishaingia kwa state council, hapo nayo state council nayo inachukuwa utaratibu wa kwamba ati inajibu kwamba hao ni zuruhisho. Naomba katibu, state council isiwe zuluhisho kwa adminstrators. Ikiwa administrator amekosa, ahukumiwe, kulingana
na mwananchi yule ambaye akikosa anahukumiwa.

Nanikiongea hivi, ni kwamba wanamsemo kwamba, “tusaidiane wenyewe kwa wenyewe”. Njee, mimi kama diwani namsaidia mwanachi na wewe kama utawala, hutaki na sauti yangu haiingi katika ofisi zetu za wakuu, mini nifanye nini! Zuruhisho ni kotini.

Ukiwa ni chief, judge atahukumu na kama nikufungwa wewe ukipatikana na hatia, ufungwe kama mwananchi wa kawaida. Ni jambo la kuhuzunisha, mini naiomba Katib hii nyinyi ambao ni timu hii ambayo mumebalikiwa, maana yoyote amechaguliwa kaa team hii, na imefika hapa Ganze, mmefika nyumbani na yako mawazo ambayo ni ya kusikitisha kabisa. Ile habari ya kuwa sisi kwa sisi tusaidiane, hasa utawala, chief, DO, DC, PC, maofficers wa CID from the district upto the provincial. Hadi hao madirectors huko, hadi katika mapermanent in the office of the president. Ni lazima kama wamepata kilio kutoka chini, wakizingatie kwa makini. Wasiseme hati state council imekaa imeamua.

Therefore that case or that file, it has been closed from the police. Why? Imefungwa vipi hiyo file huko namimi sikutosheka? Tafadhali mimi ninaomba na nikisema hivi, ninaongea mambo ambayo ni ya haki na ukweli. I am a transparent man. Kwa hivyo nimeiomba state council wakati wowote wanapopata barua ambayo inakilio cha mwananchi si diwani. Mimi ninasukumwa na mwananchi kwamba sisi tunasikitika. Administration inatuibia. Na nikiingia kila ofisi hakuna majimbu. Haki yangu mimi ninasema this is not the only office. Hii siyo serikali pekee. Najua serikali iko. Mimi ni tagonga mlango mlango mlango mlango. Sasa nikishafika huko mbele naambiwa kwanini hii jambo la location limeingia kwa kwa kwa state. Hiyo state siingelikuwa kwa sababu imeanza kwa mwananchi wa kawaida hapa Ganze! Kwa hivyo, mimi kwangu nikuomba state council ni watu wa maana, na watu ambao wakikaa, jambo lao limekomaa. Lakini wanjue ya kwamba machief wakati wengine wanawapigia twist twist twist. Kuwapima hakili zao kama ni watu wa state kweli. Na ikiwa mtu wa state atachezewa, si inaoneka ni serikali tu inachezewa hata adui anaweza kuingia. Ikiwa President matumaini yake anatumaini yakwamba kuna watu ambao serikali wameshika kuanzia Maashinani ambao ni wazee wa vijiji, madiwani, machief, hadi huko mbele, leohao wanasema tusaidiane sisi kwa sisi, anamuua mwananchi wa kawainda. Hilo ni jambo ambalo nimejisikia niliseme, na lisikike Kenya nzima, kwamba the state council isijiamulie kukata kukata kwamba sis tumekata jambo hilo kwa sababu sisi ni state. Hiyo taratibu hiyo ikome kabisa.

Na ninaongea kama diwani wa wodi ya Kauma.

Secondly, yangu ni mawili tu. Moja nitaongezea ni kuhuzu wambunge. Wabunge wetu ni wabunge wetu ambao wanajilidikizia mapesa Kenya yote. All MPs wote, ministers wetu wote katika Kenya nzima. Nikisema katika Kenya nzima naaminisha Kenya. Nanikisema Kenya, ni kuanzia msururu. From the President to the last person. Na wananchi mimi ninawaomba, usijiskie mwoga kumtaja mkubwa furani kama anakosea. Leo ni siku yetu yakutoa maoni yetu.

Wabunge wetu katika serikali yetu ya Kenya, ninaomba Katiba hii iibadilishe kabisa uwezo wao wakukaa katika mbunge letu tukufu, nakuoaua yale watakayo hao. Maanake haya wambunge wakiamua kuna msemo wa wengi wapi? Njee Rais yeye atakataa? Nahao wabunge wote wameamisha ni hivi. Lazima raisi atakubali. Rais hana makosa. Makosa yana wabunge. Kwa sababu wengi wapee ndiyo Sasa sisi twasema wachache wapawe. Sababu ya kusema wachache ni kwamba, wapunguziwe malibikizi yao ya mishahala yao ya mishahara yao, na wawe na vipindi vya vipindi viwili viwili.

Hata kama wewe ni mpunge mzuri, unafanya mambo gani mazuri katika, katika division yako? Lakini vikipita vipindi viwili, wewe usema ya kwamba na mpisha mwezangu. Mazuri ilitekeleza na mini narudi shamba, nikaangalie mambo ya shamba, mwezangu ingia hapa.

Lakini wewe ni mbunge. Wewe unataka upige vipindi kumi wewe peke yako. Unajitajirisha wewe peke yako. Diwani yeye

yuko chini. Diwani kijishahara chake ni viji shiringi elfu saba, ni pengine huko aliko anaingia sehemu ambazo zimefiliwa, kuna misiba. Kuna matanga. Mwananchi akimuona yule councillor wake anamufurahikia. Diwani mimi nimefiliwa nasina utaratibu wa matanga. Hebu niangalie. diwani hana kitu. Mbunge anacho, na haone kani. Yuko huko katika mbunge lake. Na akitoka huko, hajui ni nani aliyekufa wapi wala wapi. Yeye anachukulia tu jogoo jogoo. Jogoo ni letu tunataka jogoo liwike hata mashambani kwa wananchi wa kawaida, ambao wanatupa kura zao na uwezo katika utawala wetu.
Basi nimesema nitasema maneno mawili. Na maneno maliwi nimemaliza. Kumaliza ni kwamba ninataka muzingatie nilio sema. Na yawe yatafatilizika. Nimezungumza kuhusu utawala machief, ma DO, ma DC, ma PC na hadi nimeingia katika ofisi ya President. Pili, ni upande huu niliongea kuhusu wabunge wetu. That's enough. Thank you very much. May God bless you. Thanks (clapping).

**Com. Abida Aroni:** Ronald Zilo Zivya? Hayuko? Vitzo Joshua, its ok, amelala huyu.

**Ronald Nzilo Zivya:** Kwa majina naitwa Ronald Nzilo kutoka Petanguo. Maoni yetu ni kama yafuatavyo. Ninawakilisha kikundi cha VDC ya Petanguo. Majina yaliyonituma nifanye kazi hii ni Ronald Zirya Zilo mwenyewe, Kazungu, Mwaringa, Elizabeth, Toya, Karisa Kalume, Kazungu Mbao, Ubao Nzae, Kazo Changawa, Kaidi Kiti, Changawa Ndidadiyo, Njevu Chengo.

Serikali: Tunataka majimbo. Rais moja. Mashamba yetu, mashamba tumesema ikiwa kutakuwa na wageni basi asilimia, themanini na tano wagawanyewe wenyeji wa pale. Halafu kama kutakuwa na wageni, asilimia kumi, na tano peke yake; Rasilmali zetu tuzimamie wenyewe. Hatuwezi kuruhusu mtu mwingine aje huku.

Kazi : Kwa mfano kama vile tumesema kampuni zetu zilioko hapa pwani, kuna kampuni kama - Oil Refineries, KPA, Bamburi Portland na hata zile hotels pia, wale viongozi watakao endesha makampuni yale, watoke katika sehemu hii. Kwa ajili wale wafanyi kazi sasa. Asilimia tisaini wawe ni watoto wetu wa kutopa hapa pwani. Halafu asilimia kumi, kama kutakuwa na wengine wapate.

Elimu: Tumesema elimu ya msingi, iwe ya bure, elimu ya sekondali, njamani malipo yamekuwa hali ya juu kwamba wale wadogo ambao hata wengine hawana vibarua. Watajisikia kama labda wao pia sio wa kenya ama si watu wa ambao wanaishi katika dunia hii. Kwa hivio yale malipo ya shule za upili, kidogo yapunguzwe kiwango cha kwamba, hata wale ambao wana viwango vya chini pia wataweza kujimundumu kusomesha watoto wao.

Vyuo vikuu: Inasikitisha sana kwamba nafasi zinazovotoka za chuo kikuu, labda ikizindi watoto wanaotaka katika sehemu ya Pwani ni wakuhesabu tu. Lakini ni wengi ambao wako, wale ambao wanapata nafasi zile ni wale ambao wako karibu nazo pale pale. Kwa hivo, Kati hii, tunauliza kama ikiwa itawezekana, na si kwamba kama itawezekana, iwezakane kwamba vyuo vikuu vijengwe pia hapa pwani.

Chuo cha utalii, nafikiri hapa tulipo labda tukiangalia asilimia ya watalii, wanaoingia Kenya 90% wanakunja hapa pwani. Kwa hivo chuo kikuu chafaa pia chuo cha utalii kinafaa pia kijengwe hapa pwani. Hali ya kupunguza ngarama ya zile vyuo vikuu ni kwamba zile garama zinazindi wakati unasafirisha mtoto wako kumtoa hapa kumpeleka huko. Labda pengine ni kwenda kuuliza njee, nafasi itapatika ama vipi? Pengine akizidiwa na matatizo kwamba mzazi wake hawezi jua, na huku hata akijuwa labda kwenda haraka kumsaidia itakuwa vingumu kwa sababu ya ubali na garama ya hali ya juu. Naunga mkono wezangu walifo sema kwamba DO, chiefs, Assistant chiefs, wachaguliwe kwa kura.

Tena basi, mtu yeyote atakaye staafu either kwa kampuni ama kwa serekali, asiruhusiwe kugombea kiti chochote. Maanake itakuwa kama kuwanyima wale wengine ambao vibarua hawana. Yeye amefanya kazi miaka yake yakutosha. Amejipangia za kutosha. Amelimisha familia yake za kutosha. Halafu apewe uwezo tena yeye, nafasi zile. Njee huyo mwingine ambaye yuko hapa nyuma amesoma akamaliza na hana kazi aende wapi? Kwa hivo hapo naomba hiyo Katiba iparekebishe. Atakaye staafu asiruhusiwe kugombea kiti.

Ushuru: Ushuru wote ule wa makambuni yetu yaliyoko hapa pwani, ubaki hapa hapa. Watu wa pwani wenyewe wanajua shda zilizoko hapa. Kuna mambo hata ya mabarabara. Kuna shida zingine ambazo zinahitajika kufanyika hapa. Imekuwa kwamba ushuru ule unapotoka hapa, kwenda ukanjenga zaidi huko juu. Na hapa sisi wenyewe tunabaki tukifagia. Kama vile abavyo unaona mbuzi imekunya hapo unafagia mavi lakini mwenye kula nyama ni mwingine.

Majeshi. Tunaomba ikiwezekana katika Katib hii, wale ambao wanakuja kufanya recruitment. Kwa sababu wale hawawajui watoto wetu, hawajui mtoto wa Charo alimaliza mwaka gani. Na wakienda pale wanaulizwa unasimamiwa na nani. Hajulikani yeye. Kwa hivyo tunaomba recruitment ianzie kwenye division level ambapo yule atakaye simamia recruitment awe ni mtu labda kutoka kule, ni mtu wetu wa pwani hapa hapa.

Mahakama. Kuwe na usawa. Kuna mambo mengine ambayo hutendeka kwamba, pengine nimeonewa nimeenda kustaki. Lakini sasa basi, mimi ni myonge sina chochote. Yule aliyemshika labda hata ana magari. Bado mimi nangojea pale niende kotini najua atapelekwa kesho. Nikianda pale naabiw huyo mtu alitoka tangu juzi. Nitajisikia kweli na haki mimi? Nimeibiwa labda. Mwizi yule aliyeniimbia ameenda pale akahonga labda akatoa shillingi mia mbili ama mia tano. Pale sasa mimi nikienda kwa vile niko mikono mitupu sisikizwi mimi. Naambiwa mzee tulikutuma ukachukuwe pesa uje ufanye hivi na vile, wewe ukasema huma chochote. Siku hizi bwana mambo ni hizi. Hayo pia tunaomba yangaliwe.

Mwisho. Askari pia naomba ikiwezekana waheshimu wananchi Maanake wao wameajiliwa na wananchi. Wananchi ndio wamewafanya mpaka wamepata kazi ile ile. Yeye yuko pale kumlinda mwananchi sio kumnyanyasa. Hapo mwisho. Kwa hayo machache, asanteni sana. (clapping)

**Com. Abida Aroni:** Dakika tano kuanza sasa ili tuweze kupata maoni ya kila mtu ambaye yuko hapa.

**Vizo Joshua Mukala:** Kwa majina mimi naitwa Vizo Joshua Mukale. Katika taratibu hizi za urekebishaji wa Katib, mimi

nitaanzia upande wa mamlaka, upande wa Rais.

Rais kama sheria vile inavosema ya Kati wakati huu raisi yuko, Rais yuko - is above the law - I mean sasa, ile sheria hiyo ningependa iwe itaondolewa na awe chini ya sheria kama mwananchi wa kawaida.

Pili, Rais ameondoka asipate kinga zidi ya mastaka. Na upande wa mawaziri, waziri asiwe mwana siasa na asiwe mbunge. Kwa mfano, kama waziri, pengine waziri wa elimu, awe ni educationist. Mtu ambaye alisomea ile taaluma Kama ni waziri wa afya, namna hiyo. Halafu, upande wa kuanzia PC, DC, DO, assistant chiefs na chiefs, wawe wakichaguliwa na raia.

Upande wa rasilmali, nitaongelea juu ya mnazi. Mnazi kama zamani, kama mfano mgema. Mgema ilikuwa inamlazimu anakata licence. Na yule mchuruzi, ambaye ni yule atakuwa yuko na club chake, pia alikuwa akikata kodi kwa serikari. Kwa hivyo, ikiwezekana, hiyo iwe itatiliwa maanani. Kusudi tukisema pombe ya mnazi ni halamu, hata beer pia ni pombe na yote ukinywa utalewa, isipokuwa labda watu wale ambao wako na mabar, ni vile huwa wanakata licence. Kwa hivyo watu wa mnazi pia nao wawe watapangiwa mpango wao pia wewe wakikata licence ile waendeleza maanake ile ni biasha watu wanajisaidia nayo.

Halafu, kuna upande wa usalama. Utakuta upande wa polisi, raia huwa wanadhulumika sana. Umestakiwa, polisi amekunja amekufuata. Hujapekelwa mbele ya mahakama ukapatikana pengine uko na hatia. Utakuta utapigwa kabla hata hujahukumiwa. Na hiyo hiyo inaingilia mpaka upande wa maskara wa utawala, ambao wako na ma DO. Unapelekwa pale, uwende usikize pengine malalamshi bibi yako kwa mtu fulani. Ukifika pale, hujapelekwa kotini. Unapewa ringa, unafyeka kama ni miti unan'goa. Sasa ile ni njia moja hapo yakudhulumiana.

Na upande wa elimu, elimu ya msingi iwe ya mbure, na ya lazima kwa kila mtoto. Na halafu, upande wa polisi, askari jela ama GSU. Utakuta pengine mtu amefanya kazi miaka kama ni kumi na mitatu halafu anapatikana na hatia ndogo. Sasa pale mtu kama yule, utakuta anafutwa kazi. Na hatapewa chochote pengine zile pesa za zile miaka aliyofanya. Sasa watu kama hawa huwa wanadhulumika halafu wakirudi kuwa raiya, wao ndiyo watakuwa majangili numbari moja. Asanteni.

**Com. Abida Aroni :** Daniel Gona; Yuko? John Mbaa, dakika tano tafadhali.

**John Mbaya:** Basi kwa majina, naitwa John Mbaya, Pala Kumi location, Ganze division. Mimi nina maoni matatu.

Na oni la kwanza. Oni langu la kwaza ni la upande wa uchaguzi wa Rais. Uchaguzi wa Rais na mmbunge na diwani. Oni langu ni mchanguwe Rais kwa miaka mitano na mbunge kwa miaka miaka mitano, na diwani kwa miaka mitano. Tena nikichagua Rais, akiwa kwenye mamlaka, awe na nguvu za kufanya kazi yake ya aah yaki yakikenya. Na mbungu vile vile, nikimchagua, awe na nguvu za kufanya kazi yake za wodi yake aliyochaguliwa. Vile vile, diwani pia akichaguliwa katika wodi yake awe na nguvu za kufanya kazi yake kama diwani.

Maoni yangu ya pili ni ya upande wa machiefs. Upande wa machiefs, Isabu chief, na chief na DO, na DC hawa ndio wenye viti wa maendeleo. Isabu chief ni mwenye kiti wa maendeleo wa sub location ile, na chief ni mwenye kiti wa maendeleo ya location ile, na DO ni mwenye kiti wa maendeleo ya division ile. Lakini kuna tatizo moja la kuhusu wachagulia na waajiliwa wandikwa. Kwa sababu isabu chief na chief dio waliyoshika usukani wa maendeleo ya location ama ya sub location, kuna matatizo ya wachaguliwa na machiefs walioandikwa na mwenye kiti huyu, hana siku ya kuchaguliwa tena. Akiajiliwa ni mpaka kustafu. Anaendelea kazi yake na uchief vizuri, ni mpaka astaafu akiwa hataendelea vizuri uchairman huu ameshikilia mpaka astaafu.

Kwa hivyo wenye kiti wa maendeleo kwanzia sub location na location, na division na wilaya, tuachiwe wananchi wenyewe, tuchague mwenye kiti wa maendeleo kutoka sub location, location na division na wilaya. Iwe nafasi hii, ikichukuliwa na wananchi wenyewe.

Na oni langu la tatu ni kuhusu hawa akina mama. Wakina mama, mimi kama baba, nitaoa msichana na nitakaa naye tutafute vitakavyo tusaidia hatimaye nimuache akiwa bado akelihai mimi niondeke. Oni langu ni kwamba, uridhi nitakau wacha niwachie bibi na watoto. Hayo ndiyo maoni yangu. Asanteni sana.

**Com. Abida Aroni:** Japeth Munga Chai. Japheth yuko? Kingi William? Joseph Kingi?

**Joseph Kingi Kahindi:** Asanteni sana macommissioner ambao muko hapa pamoja nasi leo. Kwa majina naitwa Joseph Kingi Kahidi na mimi ni katibu wa chama cha walimu wilayani kilifi. Kwa niaba ya walimu wetu ambao wako wilayani kilifi, tuna maoni ambayo tuko nayo hapa. Nitapitia tu kwa halaka kisha nitaweza kuwapatia maandishi ambayo tumefanya.

Kwanza tungetaka kusema yakwamba, tunayo imani yakwamba tume abayo inatengeneza inatayalisha Katiba yetu itafanya kazi nzuri. Ikishamaliza kufanya kazi hiyo kazi nzuri, ni jambo lingine kutekeleza mambo ambayo yameandikwa kwenye Katiba. Kwa hivyo, tunataka Katika katiba yetu kuwe na vipengele ambavyo vitalinda Kati hiyo, ili iwapo mtu anatakakukosa kuiheshimu Kati hiyo, aandhimbiwe vilivyo.

Tunataka kutoa maoni kuhusu urais. Mambo mengi yamezungumziwa, na tunataka kuongezea ya kwamba yeyote ambaye anataka kugombea uraisi katika jamhuri yetu ya Kenya, awe na umri kati ya miaka thelathini na mitano. Hiyo ndiyo minimum, na maximum, iwe miaka sabini.

Akiwa nje ya miaka sabini asiweze ku qualify. Akiwa chini ya miaka thelathini na tano asiweze ku qualify. Vipindi twakubaliana na viwili natunasema kwamba Rais katika Jamhuri ya Kenya aendeleekuwa head of State na pia aendelee kuwa head of the Government na aendelee kuwa Commander in Chief of the Armed Forces. Tunaamini yakwamba Kati ikimulinda vilivyo ataweza kufanya kazi yake. Mbila matatizo.

Tunakataa mvumo ambapo tutakuwa na Prime Minister kwa sababu tuwe na President na ma-vice wake, na prime minister na ma-vice wake, na uchumi wa nchi hii tunasema bado ni mchanga unazoroteka, nafikiri tukiaza kuandika watu wengi, itakuwa si sawa. Lakini hata hivyo twa sema kwamba rais huyu aondolewe mamlaka fulani ambayo anayo. Kwa mfano asiwe

na uwezo wa kuchagua wale senior civil servants, Kazi hiyo iwachiwe kamati fulani ambayo itaundwa kikatiba.

Asiwe chancellor wa univervisty zote. Na wakati wa kumchagua president uwe tofauti na wakati wa kuchagua wabunge wengine. Tufanye kura za wabunge kwanza tumalize kisha halafu ndio turundie kura za President. Hawa ambao wanataka kugobania kiti cha president, wawe na running mates. Wawe na marafiki zao. Kila mtu na mmoja. Sasa atakayeshida president yule mwezake abaye ni running mate, awe automatically atachaguliwa kuwa Vice President. Twasema katika ofisi ya rais, commissions muhimu kama zile za AIDS, poverty eradication, environment, na zile za disabled ziondolewe na ziwe kwakatika wizara abazo zinaambatana nazo. Kwa mfano, kama ni commission ya AIDS, iweze kwenda kwa ofisi ya wizara ya Afya. Upande wa ministries, tunasema kwamba wizara zipunguzwe kutoka idadi iloyoko sasa hadi zibakie kuma na tano na tumeandika zile abazo tunazo proposals hapa tutawachia. Tunakubalia na maoni ya kwamba mawaziri wasiwe wabunge wanao wakilisha sehemu fulani katika jamhuri. Wajua kuwa mbunge kisha halafu uwe waziri, kunafanya uwe na double standards. Maana unaweza kupewa rasilmali uweze kutumia kwa wizara yako kama ni ya afya. Badala ya kutumia kwa taifa nzima, unawe zakutumia rasilmali hiyo kwa constituency yako peke yake.

Kwa upande wa elimu, tunaungana mkono na wale wezetu waliyosema kuwe na free and compulsory education kutoka nursery school mpaka dalasa la nane. Lakini kuwa na elimu hiyo na kusema ile lazima ni jambo moja.

Tunataka kusema kwamba ni lazima Katiba ihakikisha ya kwamba kutakuwa na mwalimu kwa kila darasa. Kwa mfano sasa katika eneo hili, tunayo shule hapa juu inaitwa Mnangoni – Midoina. Inayo madarasa manane. Lakini kwa wakati huu kuna waalimu wanne. Sasa sisi tunasema walimu watoto waende shule nani lazima waende. Wakifika kwenye mashule, hakuna walimu. Itakuwa kama ambayo hatufanyi lolote. Na madarasa yetu yapunguzwe. Badala ya kuwa na watoto hamsini, tuwe darasa moja na watoto thelathini.

Mambo mengine kuhusu elimu ambayo tunataka kuyazungumzia hapa, wakati huu tunamatatizo mengi ya nidhamu katiaka shuleni. Kwa hivyo tunasema katiiba ya sasa iweze ku-introduce measures abazo zitaweza kuchukuliwa ili hali ya nithamu iweze kurekebishwa. Wanafunzi wengi katika taifa hili, wanatumia madawa ya kulevya, wanavuta bangi, wanavuta sigala, hata wengine wanakunywa pombe wakiwa shuleni. Lakini uwezo wa kuadhimbu watoto huu walimu wameondolewa. Hatuwezi peana ile inaitwa corporal punishment tena. Sasa ikiwa shule imeondolewa uwezo ule, uwezo huu upewe mahakama, ili mtoto akipatikana anavuta bangi au ni mrevi achukuliwe apelekwe kwa mahakama aende akastakiwe na afungwe kama mkenya yeyote yule. Mtu anayevuta bangi, mimi naona si mtoto tena. Huyo amekomaa, na anaweza kufungwa.

Aa, upande wa registrator, twasema, aa wambunge tumawazungumzia kwa muuda mrefu hapa. Naongezea tu ya kwamba, wabunge ni watu ambao tumewachagua tunawaheshimu. Lakini mara kwa mara tunasikia kwamba katika bunge letu hakuna quorum. Wambunge waliyoko hawatoshi. Na hali hawa watu wanafanya kazi siku tatu kwa wiki, jumna, jumatano na alahamisi. Zile siku zingine wamewachiwa wafanye kazi za nje. Kwa hivyo tunapendekeza katika katiba tuseme ikiwa mbunge amekosa viakao vitatu mfululizo basi mbunge huyo apoteze kiti chake mara moja. Iwapo wananchi hawatoshelezi na kazi yao ya mbunge waweze kuandikia barua speaker na speaker aende katika constituency hiyo wafanye mkutano kama hivi tulivyonavyo hivi leo,

na tuzungumzie kwa speaker kwamba mtu huyo mbunge wetu hatuna haja naye, ajitetee. Ikiwa tunaridhika, tumpe nafasi aendelee. Kama hatutaridhika, akose kazi yake, na tuchague mtu mwingine mara moja.

Tumezungumzia habari ya akina mana, na twapendekeza kwamba ile cabinet wale mawaziri ambao sisi pia tumependekeza wasio wambunge wafanye kuchaguliwa at least 20% of them wawe kina mama, ili nao tuweze kuwapatia nafasi.

Mara kwa mara tunaskia wabunge wana-defect katikati ya term. Amechaguriwa halafu anaendelea baada ya miaka miwili end of term iko mbele yeye ana de-fect.

Matatizo mengi ya ardhi yanasababishwa nakule kupeana ruhusa uusaji wa ardhi. Twasema kwamba sisi zote niwazaliwa wa hapa Kenya. Inchi ya Kenya tumeikuta hapa na tutaiwacha hapa. Ingekuwa sawa kila mjoja wetu awe na haki sawa kwa ardhi hii. Ikiwa mtu mjoja atapewa eka kuma auze, na apate milioni sita na labda aende akanjenge kwao mahali pengine, huyu mtu anauza ardhi yako wewe na yangu mimi. Maana hii ardhi ni yetu zote. Si ya mtu mmoja. Kwa hivyo hiyo hali ya kuuza ardhi iondolewe na kila mkenya apate haki sawa. Tunapendekeza eka kumi na mbili za tosha kwa matumizi ya kawaidi. Ikiwa ni matumizi ya corporate, kama pengine mashule, au watu pengine wanataka kufanya ranching, hiyo iangaliwe kilingana na mahitaji.

Tuingilie upande wa employment, ambao sis tunahuzika zaidi. Tunasema kwamba uanjiliwa huwe haki ya kila mkenya na mtu yeyote ambayo amefika umri wa kuanjiriwa, na amesoma na amepata elimu, amefunya kazi pengine ametrain, basi aweze kuanjili Ikiwa serikali haiwezi kumuajiri, basi iendendelee kumpatia subsistence allowance wakati inatitayarisha kumtafutia kibarua. Na mara kwa mara tunapata kuna mizozo katika wafanya kazi na waanjiliwa. Mizozo hii tuhakikishe kwamba tumeimaliza kwa kuiingiza vipengele katika katiba ambavyo vitafanya labour movement iwe na nguvu za wizara. Wa-waziri wa labour awe atapewa mamlaka ya kuchukua hatua zidi ya mtu ambaye anakosa kufuata makubaliano ambayo yako katika mikataba. Mfano mzuri ni yule wa waalimu na serikali ambapo makumbaliano yapo, lakini serikali haitaki kufuata makumbaliano. Wizara ya labour ipo na kama ambayo imekimbia badala yakufanya jukumu lake la ku-arbitrate wao wanachukua sides, halafu mambo inakuwa magumu. Aaa twasema pia kuwe na automatic insurance na health cover kwa wafanyi kazi. Ikiwa watu wameajiliwa, labda ni serikali au ni kiwanda fulani, wawe na automatic insurance na health cover. Kuna waanjili wengi ambao wana wana ujaja fulani. Wanaandika wananchi wetu hapa baada ya miezi sita wanawafuta. Kwa sababu wanaona labda wakiwacha zaidi ya miezi sita watakuwa permanent and pensionable. Tungetaka kuwa na policy ya employment. Kama ni kiwanda cha kutengeneza mananazi, kama ni kiwanja cha kutengeneza sandles watu waandikwe on permanent and pensionable terms, ile tuhakikishe ya kwamba kutakuwa na mambo au kutakuwa na pesa zao wakati wakistaafu.

Mara kwa mara tunaona kwamba kuna wezetu kama hao askari, askari jeshi. Hawa ni wakenya wenzetu na wanafanya kazi nzuri. Lakini sasa askari anaweza kwenda kwa training. Akamariza akaenda kwa kambi. Na akakaa katika hiyo kambi huko anapanda madaraka na hakuna vita na hakuna kazi anafanya. Na huku twasema hakuna waalimu hakuna madaktari. Twapendekeza kazi kama zile mtu enda akafanya training yake ya jeshi. Kisha akimaliza apitie kama ni training ya skuli au kama ni training ya nursing. Halafu apelekwe hospitali afanye kazi. Au apelekwe shule aende afundishe. Wakati wa vita, watoke

mashule, waende wachukuwe bunduni, waweze kwenda kupigania taifa lao. Lakini wasikae tu kwenye kambi mpaka mtu anafikia umri wa kustaafu. Wasikia mtu ni major general anamapete sijui karibu mia hapa na hatujamwona ujasili wake mahali popote.

Mara kwa mara aa walimu au hata wafanyi kazi wa serikali hutaka kupigania viti vya mbunge au vya ukancouncillor.
Kuna sheria kwamba ni lazima wa resign. Utaona hii sio sawa. Wepewe tu leave. Kama ni ya mieze mitatu au minne waende wakapiganie viti. Wakipata, waache hizi kazi walikuwa nazo waendelea na zile mpya. Wakikosa warudi kazini, waendelee kama wenzau. Aa na hata mala nyingine tunambiwa tusifanye campaign ya kutafuta candidate ya kusaidia. Hasa mimi nataka Rais aniongoze. Wee pia unataka Rais aniongoze hutaki mimi nitoke nje niende nikamwambie mwenzangu nataka huyu, lakini wewe ujipatie nafasi ya kwenda kuongea. Hati mimi ni kifanya hivyo ni makosa na ninastakiwa. Kila mtu awe na uhuru hata ikiwezekana hizo wiki tatu za campaign, tuseme kila mtu aende leave. Tutafuta njia tu lakini kila mtu awe na uhuru aende akafanye campaign yake mpaka tupate Rais tupate mawizi na wambunge, halafu twende kazini.

Na mwisho, kwa upande wa maoni twataka kusema yakwamba aa kuna kuna vitambulisho hizi national identity cards ambazo zinapeanwa katika umri wa miaka kumi na minane. Elimu ya darasa la nane inamalizikia labda katika umri ya miaka kumi na miine, na tumekubaliania kwamba hii elimu hii mtoto akimaliza darasa la nane kuna uwezekano akapata kuanjiliwa mahali kwa sababu amejifunza kuchora vizuri au kuchonga viti. Sasa atakwenda kuanjiliwa lakini hawezi kuwa na kitambulisho kwa sababu mpaka afike miaka kumi na minane. Mapendekezo yetu twasema, mtoto anapomaliza darasa la nane, akiwa yuwatoka apewe leaving certificate yake yakutoka shule pamoja na kitambulisho aende nje akajiaombee Mwenyezi Mungu Mwenyewe.
Twakumbaliana na wenzetu waliyo zungumuza kuhusu mamba ya afya. Ukahaba umezidi. Ukahaba ni hatari kwa taifa hili aa una zambeza ukimwi, na tunashangaa vile serikali yetu au Katiba inaweza kuacha night clubs ambao kila mtu anajua kabisa hapa kakuna mambo inaendelea isipokuwa ni ya ukahaba na yataleta ukimwi, na twangalia huku twatamka kila mahali this is a national distater na hatuna tufanyalo.
Aaa ingekuwa pia ni vizuri wakati huu wa nji hatari kabla mtu hajaoa na kabla mtu hajaolewa, maanake mimi nawezakuwa na mtoto wangu mvulana au msichana nikamfuga vipaya. Akaingilia mamba ya ukahaba mapema. Wewe una msichana wako na mvulana wako ukamtuza. Wakati msichana wako akiwa tayari anataka kuolewa akaja akapatana na mototo wangu ambayo alikuwa na ukahaba, mtoto wangu akamuoa mtoto wako, badala ya kumpatia familia, akampatia ukimwi na aka muua. Kwa hivyo tunasema kuwe na test. Watu wafanyiwe testing ndio waweze kuruhusiwa kuoana. Hawa watu ambao wanatia mimba wasichana, hao wanatupatia shinda. Msichana yuko darasa la sita ana dungwa mimba. Msichana yuko form 3 anadungwa mimba, hakuna lolote anafanywa. Pengine akiwa mwalimu atakuwa interdicted, halafu afutwe kazi nani basi. Kisha aendelea hata anaweza kutafuta kazi nyingine kesho akapata. Twasema mtu akijihuzisha na mambo ya mapenzi na msichana wa shule au hata ni mana ajihuzishe na mapezi na mvulana wa shule, na ajukilane, mtu kama huyo afungwe gerezani kwa muda usiyopungua miaka mitano. Iwapo mapenzi hayo, iwapo mapezi hayo yamesababisha mimba, maanake mapezi yanaweza kusababisha mimba. Sasa una kuta msichana anazaa mtoto na huyu bwana aliyemdunga mimba hataki kumuoa na antembea akiwa huru kama yeye hakufanya makosa yeyote. Twapedekeza either alazimishwe na Kati amuoe na kama hatakubali kumuoa aende

kifungoni kwa miaka kumi na minane. Hiyo miaka kumi na minane ikiisha, huyu mtoto aliyezaliwa atakuwa amekuwa sasa ni barubaru. Anaweza kujisimamia sawasawa. Watoke wote sasa ulimwenguni waende wakafanye kazi pamoja.

Tuna mambo mengi lakini kwa sababu ya wakati yale yaliosalia. Bado sijapigiwa kengele.

**Com. Abida Aroni:** Aah sasa zimekishwa tafadhali. Kuna wengine hapo, wengi.

**Joseph Kingi Kahindi:** Nitasoma – okey – nitasoma. Hii mambo ya retired officers. Mtu akiritaaya asirudi kwa public office.

Retirement. Siku hizi zile payslip zinaandikwa umri wako ni huu umri wako ni huu. Hata ile ya mwisho inaandikwa kazi yako sasa imeisha umestaafu. Lakini retirement benefits zinakuja baada ya mwaka moja kama ile computer husahau tu bado ikifikisha kwa retirement kazi yako imeisha. Twataka mtu akiritaya leo 31st January, 28th February aende akachuuwe retirement benefits zake. Asanteni na nitawachia hii karatasi, yale mengine mweze kusoma wenyewe. Thank you so much.

**Com. Abida Aroni:** James Hale? Joseph Kingi Kahindi? Tuko pamoja. Simon Toyo? Mathias Fondo? Dakika tano.

**Mathias Fodo:** Asante sana bi mwenye kiti, mabibi na mabwana. Mimi kwanza kwa maoni yangu nitaaunga mkono hili jambo la kusoma kwa wavulana na wasichana. Liwe la lazima kwa ile serekali ijayo, na kusiwe na malimbo yoyote, ili wezangu wamegusia juu ya mnazi. Mimi pia naunga mkono kwamba mnazi uhalalishwe isipokuwa tuunywe kwa masaa, ili tupate wakati wa kwenda mashamba. Na upande wa kuchaguliwa kwa machief na manaimbu wao, mimi pia naunga mkono kwamba wawe wakichanguliwa kama madiwani.
Upande wa Rais, kulingana na Katiba ijayo, nataka Rais ambaye atakuwa na nguvu za kuweza kusimamia mamlaka yake ya urais. Na upande wa lugha ya kitaifa, maoni yangu ningependa lugha ya kitaifa iwe moja ile ya kiswahili. Kwa hayo machache nasema asanteni.

**Com. Abida Aroni:** Nathaniel Mweli Mbaya? Alex Kisau? Morris Mungela? Kahindi Kiti?

**Kahindi Kiti:** Kwa majina, naitwa Kahindi Kiti, kutoka hapa Ganze, Sub Location yangu ni Petanguo. Mimi katika maoni yangu ningependekeza kwamba katiba serikali ijayo iwe na katiba ambayo itakuwa kwa upande wa mashamba.

Kwa upande wa mashamba, wezangu wameguzia lakini pia mimi naongezea vile vile. Kwa upande wa mashamba, ikiwa kuna sehemu fulani mkoa fulani, wilaya fulani, kuna sehemu ambayo inagawanywa basi mwananchi ule ambaye ni mzaliwa wa hapo

aaze kugawanyiwa iwe ile kama ikiwa kama sehemu mia moja, sehemu tisaini ziwe zigawanyiwe wale wazaliwa wa hapo. Kwa sababu mashamba ni kitu cha kunufaisha mwananji. Na ikiwa mimi kwa mfano ni mzaliwa wa hapa na ile sehemu ambayo nilikalia kutoka babu, mpaka baba, mpaka kwa wakati huu, anakuja mtu mwengine kutoka mkoa mwengine, mbali kabisa. Anakunja na number ambayo imelenga pale shambani kwangu ambapo ni uridhi wa babu na hata baba. Hiyo itakuwa ni kama uonevu. Kwa hivyo ikiwa ni upande wa mashamba yanagawangwe sehemu fulani, mwananchi ule ambaye ni mzaliwa wa hapo akumbukwe zaidi kuliko yule ambaye anatoka mkoa mwingine.

Jambo la pili ningependelea tume ifikirie hivi. Katiba ijae serikali ambayo itakunja itashika mamlaka wakati unaokuja, kuwe na katibu ambayo mtoto akimalizia form four ama akimaliza darasa la nane, na amepita vizuri sana, amepata national school, lakini anatoka jamii maskini, mtoto yule aweze kuchukuliwa na serikali asaidiwe ili kwamba elimu iweze kusambaa kila mahali.
Kwa hivyo, mimi sitaendelea sana lakini nasikitiza zaidi mambo ya mashamba. Ikiwa kuna sehemu fulani inagawanywa, yule mzaliwa wa hapo akumbukwe zaidi ya mwengine. Mtoto anapomaliza darasa la nane, akiwa amepita vizuri sana amepata sikuli ya kitaifa na anatoka jamii maskini, aweze kusaidiwa na serikali mpaka amalize form four. Kwa hivyo, maoni yangu ni hayo. Asanteni.

**Com. Abida Aroni:** Asante. Joo kwa huku. Kenga Kilomo Chai.

**Kenga Kilomo Chai:** Asante bwana mwenye kiti. Mimi jina langu naitwa Kenga Kilimo Chai, kutoka Kauma location, Ganze division. Asante.
Chairman wa tume hii, maombi yangu kuhusu ardhi. Wezangu wamezungumuza za kutosha, nami ninaongezea na kutoa maombi yangu ofisi ya kutoa title deed iwe Mombasa kwetu pwani hapa. Kwa sababu tunaenda Nairobi wengine hatuuji Nairobi, tunapotea tunafika wiki nzima hatujajua. Tunarudi hapa. Wazee wengine hata wanaaga dunia mbila kujua title deed ni kitu gani. Twaomba iwe mukoani hapa. Ikiwezekana hata kwa wilaya.

Jambo la pili, twaomba kituo kikuu hapa kwetu pwani. Ikiwezekana hata Kilifi. Tuna chuo hapa cha agriculture, Kilifi Institute of Agriculture kibadilishwe basi tupate university hapa pwani. Kitaweza kusaidia watoto wetu kwa karibu, na kitaweza kufanya huduma hata watoto wetu wale ambao hawezi kwenda huko Nairobi watasaidika hapa. Kati hii ya wakati ujau serikali hiyo ione mambo haya kwamba yametekelezwa. Nasisi tafaidike.

Jambo la tatu. Mambo ya afya. Tunahitaji vituo vya afya. Zile health centres ziweko kwa malocation. Kwa matatizo haya yametukumba sana hasa wilaya hii ya Kilifi. Mtu atakuwa anamatatizo. Pengine ni ya uzazi mpaka kubemba na kitanda, kupeleka zaidi ya maili kuma na tano, ndio kupata basi na kwenda naye Kilifi. Kwa hivyo vituo hivi vikiwako kwa malocation, vita tusaidia sana Bwana Chairman.

Jambo la nne. Viwete. Walemavu, wale hawajiwezi, wale watoto, weweze pia kusaidika na shule, maana wamekaa

manyumbani hawa wamechukuliwa wale ni watu hawafai kabisa wamebwagwa tu na wazazi wao. Na wazazi wao hawajiwezi. Wawe na shule zao za walemavu katika division hadi malocation.

Jambo la tano. Tunarundi hapo shule hizi primary. Pia kuna watoto ambao ni mahekima. Wameachwa, wazazi wao wame enda kwa Bwana. Lakini sasa kulitoka amri ya kwamba primary ni bure. Lakini ukirudi shule yale pesa za majengo zimetatiza wale ambao wanawasaidia mpaka watoto wale wanakosa shule. Twaomba serekali itakayo kuja ibebe mzigo huu wa shule hizi za primary. Kuwasaidia maanake ni mzigo mkubwa na wengi wanakosa kusoma na kuweza kule kujifaidisha na wao katika maisha yao katika Jamhuri hii ya Kenya.

Number sita. Mnazi. Mnazi, hauna makosa, serikali ijao ipitishe katiba hii ipitishe mnazi tembo halina makosa. Ndio uchumi wetu wa hapa pwani, ndio kahawa. Na haini makosa. Maana ile ni jasho la mti. Si kitu cha kupikwa. Ile ni kwamba ni tembo haramu. Ni jasho la mti wenyewe.

Safi. Hauna makosa. Utambuliwe kama mmea mwingineo unaopelekwa hata America. Kahawa, majani. Na hapa napo mafuta yetu, bata yetu itambulike nayo iende ngambo. Katiba ijao pia iupitishe mnazi kazi zake iende ngambo.

Number saba. Maji inamatatizo sana katika wilaya hii ya kilifi. Hasa division ya Ganze. Maji yamepita kweli hapa yameenda Mombasa lakini hayakufanya vitagaa vya kwenda huko vitongojini. Maji ni tabu. Afya nzuri utaipata wapi?. Tunapata maji ya kwenye mapenezi. Typhoid zinatusumbua tumechoka. Katiba ijao ilekebishe mipango ya maji vitongonjini pia yafike.

Number nane. Madiwani wale waliyosema mpaka wafike form four hivi na vile, hata yule ambayo hakufia form four anafanya kazi nzuri zaidi kushida yule aliye soma kwenda mpaka form four. Kwa hivyo wapewe nafasi kwa wakati ujao. Manadiwani wachaguliwa na mwananchi. Hachaguliwi na wale waliosoma, huko vitongonjini ndiye anayejua shinda iko wapi? Waliyosoma, wengi wamechaguliwa sasa wamekaa town hata huko vitongonjini hawaonekani. Je wale si waliosoma? Bona hatuwaoni? Na kazi haziendi. Kwa hivyo si lazima aliyesoma. Tufanye kazi tuiinjenge Kenya.

Case hizi za mtu amepata accident na sasa case imeenda mahakamani, bado hapati malipo. Inambiwa mpaka akashike advocate, ndiye atafute malipo yake. Twaomba serikali ubebe mzigo huo ijayo. Case inapoendelea, ikimalizika judge amalize kabisa hata malipo. Judge wa government ambaye atakuwako wakati huo. Badala ya nikatafute wakili yule ambaye hanapesa anadhofika na anapoteza mambo yote. Kwa hivyo, tunaomba serikali ijayo. Naona wapiga piga basi wacha nimalize. Wacha ni malize.

Mengi sana yakusema hatuna kwa sababu umesemani dakika tano na muda ni mchache, lakini majimbo, majimbo utaibwa wimbo huo na serikali ijayo utekelezee. Majimbo tunataka. Maana tukiwa na majimbo, hata hivyo vikwazo vya title deed kuifuata Nairobi nitaipata hapa. Kila jimbo litakuwa linajitengemea maanake, hata kama ni elimu kuna matatizo gani badala ya

kwenda Nairobi itakuwa ni hapa. Ama ikizidi ni hapa Kilifi. Njee, tunafauru hatutafaulu. Nii maendeleo si maendeleo. Asante hata mimi ni mwananchi wa Kenya jamhuri hii. Asanteni, hii ni mara ya pili. Najua mara ya kwanza aliye kuja pale aliwakuwa ni huyo Bwana Mwenyewe Professor Ghai na hilo jambo tulilizungumzia na hivi tumetia nina pili, haki maoni yawezangu yote yaliyopitia hapa Mungu atayabariki, nanyi mtayabeba mzigo huu, mtaupeleka malali unapohuzika. Asanteni, kwa hayo yote. (clapping)

**Com. Abida Aroni :** Japheth Kanana Zaro

**Japeth Kanana Zaro:** Asante san bii Mwenye Kiti. Mimi ninaongea kwa niaba ya vijana wa hapa Ganze Neigbourhood Youth Group.

Kwanza nitaongea juu ya powers za Raisi. Tunataka zipunguzwe. Tuweze kuwa na Rais ambaye anaweza stakiwa ili kwa sababu akifanya makosa awe anaweza tolewa mamlaka. Mamlaka ambayo pia Rais amepewa ni mengi mno. Kugusia gusia yale ambayo tunataka itolewa ni kama yafuatayo.

Kutewa mawaziri. Mawaziri tunaona yakwaba yani kuna ministries tofauti tofauti zingine zinapewa mawaziri ambao hawastahili. Tunaweza imagine kama pengine mtu kana Mulu Mutisya apewe wizala ya elimu kuongoza. Haongoza je mtu kama huyo.

Pia Rasi anauwezo wakuvunja mbunge akipenda. Hiyo kitu lazima iodolewe. Rais hatakikani awe anaweza vunja mbunge wakati wowote anaotaka. Pia Rais awe anawe kua-ppoint majudge. Tunataka kuwa mbunge liwe linapewa uwezo wa majudge ili iwe inaweza kuappoint. Pia power za Rais za kutewa mahawa watu wakubwa wakubwa serikalini kama vile Permanent Secretary, Governor wa central bank, parastatal chiefs, our electral commissiners. Hizo zote tunataka ziwe kuna kiwango fulani ambavyo kuna body fulani ambayo inaweza husika na kuwajili watu kama hawa. Halafu pia Raisi hatutaki kuwa awe na pia ni Commander in chief of the Armed Forces. Kwa sababu anaweza tumia vibaya mamlaka yale hata ikiwa mmemutoa huku nje anaweza chukua mamlaka ya kuwa yeye ni Commander in Chief wa Armed Forces, ili aendelee kuongonza. Rais pia tunataka ahudumie vipindi viwili. Na Rais pia tunataka azuiwe kuteua watu ambao hawatakikani. In other words kwa kizungu, people with questionable characters.

Kuguzia economy kama kwanza tutaongea kuhusu elimu. Elimu ni msingi wa maendeleo yoyote katika nji yoyote. Tunataka wanafunzi wote wadogo wasome bure katika mashule yao. Na ile tume ya Koech. Ile report ya Koech iwe adapted.

Tukiendelea kwa afya. Tunataka hii mambo ya cost sharing kwa hivi, kwa iwe hii afya itolewe. Tunataka hizi madawa pia ambazo zinatibu kama hizi ugojwa wa ukimwi abazo zilikuja hivi juzi juzi. Ziwe provided kwa wananchi kwa cheaper prices. Halafi hizi health centres zetu kama hapa constituency ya Ganze tunaona kuna health centres kidogo sana. Tunataka ziongweze ili wananchi wafaidike zaidi.

Tukiingilia kwa agriculture, kuna mimea hapa pwani kama cashewnuts ambayo ni mkorosho na mnazi. Hivi tunataka ziwe

classified kama cash crops. Tukiclassify hizi mimea kama cash crops nikuwezesha kuwa yaani tutakuwa tunaweza kuform boards kama vile coffee board of kenya. It means tutakuwa tunaweza pia kuform Cocunut Board of Kenya ambayo itaingilia hii mambo ya mnazi vile itaendelea.

Tukiangalia pia huko agricultural hivo hivo tunaona viwada vingi pia vimefifia kama Kenya cashwnuts, kama mwenzangu vile alivyosema. Kuna hii K.C.C., Ramisi. Halafu kitu kabisha cha kisikitisha sasa ni hii Kilifi plantation pia nayo inauwawa. Maziwa yetu tutapelekewa wapi? Tunapokuywa kila kitu chetu. Kwanini?

Tunataka pia hizi mambo za ujira ziangaliwe. Oke watu wa pwani tunasemekana hatukusoma. Ni sawa hatukusoma. Yule mpagiani pia, yule ambaye anaweza fagia kule mahotelini, kule viwadani kwa nini utoke bara. Sisi hatuna watu ambao hawawezi fagia pia huku kwetu? Tunataka basi katika hizi hotel industries, na zile kama KPA na hizi viwada vingine ziko hapa tunataka percentage kubwa iwe inatumika kudevelop hizi areas zetu. Kwa sababu ukiangalia ukiajiri wale watu wakule mbali wanakunja huku kwetu wanakula, wanachukua zile pesa ambazo wanata kana wawe wanasaidia huku kwetu wanazichukua wanaenda wakasaidie kule kwao. Kwa hivyo inatakikana hivi vitu zetu tuwe tunazi-manage wenyewe.

Barabara. Kuna ile inaitwa fuel levy. Tunajua kila constituency ilipewa milioni tano ili idevelop hizi barabara zetu. Lakini tukiangalia jamani, constituency zile ambazo ziko kule Rift Valley. Kama ile ya Baringo ambapo hata barabara zinawekwa mahindi, kwa nini wapewe milioni tano. Ile milioni tano si tungepewe sisi tutengeneze zetu barabara jameni.

Energy. Moto tulileteaw kweli. Lakini ukiangalia umekuja barabarani tu peke yake. Kwa nini isiende mpaka mijini na huko ndani ndani. Ili tuite maendeleo. Tafadhali katiba yetu tunayotaka yangalie mambo haya.

Nikiingilia pia hizi non-governmental organisations. Tunaangalia non government organsations kama hapa Ganze tuko na bili peke yake, ambayo ni Plan International na KDDP. Kusema ule ukweli plan international imefanya kazi nzuri. Ijapo kuwa tunataka waendelee. Lakini kuna vitu ambavyo vilioneka wazi wazi. Plan international imefanya hapa Ganze. Tunataka zile non-governmental organisations ambazo hazifanyi kitu chochote ama ni mbaya zitolewe kabisa ama ziwe de-registered. Hii KDDP ambao ni non governmental organisation ya pili, tungali bado tunataka kuona yale manufaa yake zaidi.

Mishahara. Tunantaka – kido nimalize. Tunakaka hii mishahara ya watu ambao wako chini kabisa iongezwe. Kusema ukweli hizi elfu kama nne mtu anazopata ni kidogo sana kwa watu ambao wako chini.

Tukiingilia political parties, hii number ya political parties is very high. Tunataka ipunguzwe kuwe na vyama vitatu ama vinne. Halafu na hawa political gangs ambao wanatumiwa wakati wa kura tunataka Katiba iangalie kuwa wanaweza shikwa na wawe punished accordingly. Pia kuwe na kipengele cha provision ya independent candidates. Unaweza kuwa wewe hutaki chama chochote kile vile viko pale, lakini kama kuna kipengele cha independent candidate iwe iko ili tuweze kugombania pia.

Halafu electro commission, wakati wa ile kura ikifika hawa youths wengi huwa wanaandikwa kazi na Electral Commission. Sasa tunaomba pia Katiba iangalie kuwa wale ambao wanaadikwa kazi na electro commission wawe wanaweze piga kura. Halafu pia hawa majeshi. Kuna vitu vingine majeshi huwa wanafuzwa kule. Kama vile utengenezaji wa barabara, kamahawa hizi

health centres. Tunaomba kama inawezekena hawa wanajeshi wawe wanaweza tumiwa kututengenezea kama barabara zetu kama hakuna pesa.
Ziwe wanaweza tengeneza barabara zetu kama bridge vile zimepotea. Kama zimekatika na maji, wawe wanaweza tumiwa pia ili kupunguza zile garama.

Kuhusu corruption tunaomba harsh penalties kwa wale ambayo wanapatikana wakilarushwa. Na pia wasi kubaliwe kabisa kuhold public office.

Form of government. Tungependelea government of national unity. Yaani hata kama ni serikali ambayo imeshinda inaweza pia kuchukuwa wabunge hata kwa hivi vyama vingine vya upinzani, ili waunde serikali.

Child abuse. Harsh penalties ziwe imposed. Representation of women in Government. Women should be - yani wanawake wawe na usawa na wanaume. Kwa hivo hii idea yakuwa tuona reserve seats kwa wanawake hatuitaki. Tunataka wote wawe pamoja wachukuliwe kwa sababu wote wako sawa, wawe pamoja. Asanteni

**Com. Abida Aroni:** Gumbao Kadenge? Jonathan Mivilu? Charo Menza Lungo?

**Charo Menza Lungo:** Kwa jina langu mimi naitwa Charo Menza Lungo, Dungisha Location. Nakaa katika sehemu hiyo ya sub location Dungisha. Mimi shinda yangu ni kwamba, nikiongeza nikiongezea wale kama wazee wa vijiji. Niongezee kabisa wao wapate mshahara kwa sababu wao ndio wanatumikia zaidi hasa sehemu hiyo ya sub chief. Kwa hivo sina mengi sana yakuongezea. Ni hayo tu. Asante.

**Com. Abida Aroni**: Karisa Maitha? Kazungu Hamadi**?**

**Kazungu Hamadi**: Mimi kwa jina naitwa Kazungu K. Hamadi. Maoni yangu ninaomba katiba mpya inayokuja ya Kenya. Hapa tuko na madini. Madini yetu ni kwamba hapa tuna waisilamu, tuna wakristo, na walevi. Ninacho omba ni kwamba haya madini yasiingiliane. Maana kuingiliana ndiyo kunaleta vita.

Maoni yangu mengine ni kwamba hapa kwetu mtu anaweza kupata accident. Anapopata accident anapopeleka kesi kotini anatakikana apate wakili. Na wakili huyo baadaye badala yake amsaidie, anamuibiya. Asanteni.

**Com. Abida Aroni:** Karisa Maitha? Bakari Kisau?

**Bakari Kisau:** Asante sana. kwa jina naitwa Bakari Kisau kutoka Petanguo. Nashukuru sana siku hii ya leo kwa sababu ni siku ambayo sitaisahau maishani mwangu. Nilikuwa ninahamu sana na hii mambo ya katiba. Mambo ya katiba madam imeletwa

kwa raiya wa kawaida. Hili ni jambo ambalo nalitilia maanani sana. Nashukuru. Chungu zangu yani machungu yale ambayo yamenitegemea ndani ya moyo siku nyingi sana, nikuhusu mashamba.

Sisi zote ni wazaliwa wa hapa Kenya, na utakuta wengine wana mashamba makubwa yaliyo na title deed na wengine hawana. Ingekuwa sawa kila moja wetu awe na haki sawa kwa mashamba na apewe title deed yake.

Hapa pwani hatutaki serikali ya umoja, kwa maana hakuna lolote wametusaidia nalo. Tunahitaji serikali ya majimbo, ili tuweze kujitawala wenyewe.

Tukienda kwa upande wa afya, utakuta kwamba hapa kwetu pwani, hatuna mahospitali ya kutosha, na hata zile ziko, hali yake ni mbaya zaidi, hatuna madawa na madakitari wa kutosha. Hata hapa kwetu Ganze, tunaona kuna health centers kidogo sana. Pendekezo langu ni kwamba tunahitaji hospitali za kutosha katika kila sehemu ya pwani, na mambo ya cost sharing yatolewe, na tupate matibabu ya bure.

Kwa upande wa elimu, elimu ya msingi hati secondary iwe ya bure na ya lazima kwa kila mtoto.

**Com. Abida Aroni:** Johnson Nyache, Johson? Kama hayuko anayemfuata ni Nzingo Mganga.

**Nzingo Mganga:** Asante mwenye kiti, kwa majina naitwa Nzingo Mganga. Sina mengi ya kuzungumza kwa maana yale niliyokuwa nayo mengi yashazungumzwa, kwa hivyo nina mawili tu.

La kwanza, hapa kwetu pwani kuna shida nyingi sana, umasikini ni mwingi zaidi na ndivyo unapata kwamba watoto wengi wetu hawamalizi masomo yao kwa sababu ya ukosefu wa karo. Kwa hivyo ningependekeza kwamba elimu ya msingi iwe bure ili wale ambao hawana huwezo wa kulipa karo, watoto wao wataweza kusoma.

Sina mengi mwenye kiti.

**Com. Abida Aroni:** Salim Kazungu

**Salim Kazungu:** Kwa jina naitwa Salim Kazungu. Na maoni yangu ni yafuatayo.

Kwa upande wa mashamba, wenzangu wamezungumzia lakini pia nitaongezea kidogo. Tuwe na ofisi ya kutoa title deed hapa kwetu pwani kwa sababu Nairobi ni mbali na wengi wetu tunapata shida ya kusafiri mara kwa mara.

Upande wa rasilimali, ningependekeza kila jimbo liweza kutumia rasilimali zao kuwafaidi wenyewe kwanza na kama kuna zaidi,

basi, wapeleke kwenye serikali kuu.

Ni hayo tu.

**Com. Abida Aroni:** Haya, asanteni sana wananchi wale ambao wamevumilia kutoka asubuhi mpaka saa hii. Sasa tumefika mwisho wa kikao hiki cha leo. Na tutafunga kwa maombi.

**Shem Chalo Nyare:** Basi na natuombe. Tunakushukuru Mungu wetu kwa wakati mwema ambao tumekuwa mahali hapa, wakati wa amani, wakati ambapo Baba umetupa nafasi ya kuongea yale ambayo umetuwesha kuongea, tunaomba Bwana, ukapate kuwa pomoja na kila moja wetu na hata mwana uakazidi kutabariki kama Wananchi wa Kenya ili Bwana katika kurekebisha Katiba yetu, umoja wetu baba kama taifa ukapate kuendelea kuonekana.

Na Bwana ukabariki ma-Cmmissioners wetu katika kazu ngumu hii, Bwana ukawape hekima ambayo mwana inatoka juu, ili kuwa mapenzi wakatengeze yote kwa ajili ya utukufu wa jina lako. Uwe pamoja nasi zote na ni katika jina la Yesu aliye ni Bwana na Mkozi tumeomba. Amen

The meeting ended at 4.45 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&